# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

# MKAKATI WA TAIFA WA KISEKTA WA KUTOKOMEZA UKEKETAJI WA MWAKA

# 2025/26 – 2029/30



JULAI 2025

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

## MKAKATI WA TAIFA WA KISEKTA WA KUTOKOMEZA UKEKETAJI WA MWAKA 2025/26 – 2029/30

**Julai 2025**

**YALIYOMO**

VIFUPISHO ........ iii
DIBAJI ........ iv
USULI ........ v
TAFSIRI YA DHANA ........ vi
MUHTASARI WA MKAKATI ........ 1
SURA YA KWANZA: KUHUSU MKAKATI HUU ........ 4
1.1 Utangulizi ........ 4
1.2 Umuhimu wa Mkakati ........ 5
1.2.1 Umuhimu wa Mkakati Kijamii na Kiuchumi ........ 6
1.2.2 Ulinganifu wa Mkakati Kisera na Kisheria ........ 7
1.2.3 Ulinganifu wa Kikanda na Kimataifa ........ 8
1.2.4 Mafunzo Kutokana na Afua za Awali ........ 8
1.2.5 Hitaji la Mbinu Jumuishi ........ 8
1.2.6 Mabadiliko ya Kimkakati ........ 9
1.3 Mbinu za Uandaaji wa Mkakati huu ........ 9
1.4 Mpangilio wa Mkakati ........ 11
SURA YA PILI: UCHAMBUZI WA HALI NA MUKTADHA ........ 13
2.1 Utangulizi ........ 13
2.2 Juhudi Zilizotekelezwa Chini ya Mkakati wa Mwaka 2020/21–2024/25 ........ 14
2.2.1 Mafanikio Makuu ........ 14
2.2.2 Hatua muhimu za Kisera na Kisheria ........ 14
2.2.3 Kujenga uwezo na ushirikishwaji wa Jamii ........ 15
2.3 Mafunzo muhimu yaliyopatikana ........ 15
2.3 Tathmini ya Kisiasa, Kiuchumi, Kijamii, Kiteknolojia, Kimazingira na Kisheria ........ 17
2.4 Uchambuzi wa Uwezo, Vikwazo, Fursa na Changamoto ........ 22
2.5 Uchambuzi wa Wadau ........ 24
2.6 Maendeleo na Muelekeo ........ 26
2.7 Mambo Muhimu ya Kuhakikisha Mafanikio ya Mkakati wa Mwaka 2025/26–2029/30 ........ 27

2.7.1 Mifumo Imara ya Kisera na Kisheria ..... 27

2.7.2 Ushirikishwaji wa Jamii ..... 28

2.7.3 Ushirikiano wa Kisekta Ulio Imara: ..... 28

2.7.4 Maamuzi Yanayotegemea Tafiti na Uwajibikaji ..... 28

2.7.5 Huduma Jumuishi Zinazomlenga Manusura ..... 29

2.7.6 Ushirikishwaji wa Watoto wa Kike, wa Kiume, Wanawake na Wanaume . 29

2.7.7 Kukabiliana na Ukeketaji wa Kuvuka Mipaka ..... 29

2.7.8 Kukabiliana na Ukeketaji wa Kificho ..... 29

2.8 Vipimo Muhimu vya Mafanikio ya Mkakati ..... 30

2.8.1 Ufuatiliaji na tathmini ya ufanisi wa mkakati ..... 30

SURA YA TATU: MSINGI WA MKAKATI ..... 35

3.1 Utangulizi ..... 35

3.2 Dira, Dhima, Lengo Kuu, Malengo ya Kimkakati na Kanuni Elekezi za Mkakati35

3.2.1 Dira ..... 35

3.2.2 Dhima ..... 35

3.2.3 Lengo Kuu ..... 35

3.3.4 Malengo ya Kimkakati ..... 35

3.3.5 Kanuni Elekezi ..... 35

SURA YA NNE: MFUMO WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI ..... 39

4.1 Utangulizi ..... 39

4.2 Malengo ya Kimkakati, Matokeo Tarajiwa na Afua za Kimkakati ..... 39

4.3 Matokeo Muhimu na afua za Kimkakati ..... 41

4.4 Nadharia ya mabaadiliko ..... 49

SURA YA TANO: UTEKELEZAJI, URATIBU, UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MKAKATI ..... 53

5.1 Utangulizi ..... 53

5.2 Mipangilio na Mikakati ya Utekelezaji ..... 53

5.2.1 Uratibu wa Jumla wa Mkakati ..... 53

5.2.2 Mfumo ulioandaliwa kwa ajili ya mgawanyo wa madaraka na utekelezaji wa mkakati kulingana na mazingira halisi ..... 53

5.3 Muundo wa Uratibu na Majukumu ..... 54

5.4 Ushirikiano wa Kisekta: Mikakati ya Ushirikishwaji wa Wadau ..... 54

5.5 Rasilimali Fedha za Mkakati ........ 59
5.5.1 Dhamira ya Bajeti ya Serikali: ........ 59
5.5.2 Ushirikiano na Wadau wa Maendeleo wa Kimataifa: ........ 59
5.5.3 Uhamasishaji wa Rasilimali za Ndani: ........ 59
5.5.4 Usimamizi wa Fedha kwa Uwazi: ........ 59
5.6 Mpango jumuishi wa kujenga uwezo wa rasilimali watu ........ 60
5.7 Mpango Wa Usimamizi wa Takwimu, Taarifa na Mawasiliano ........ 60
5.8 Ufuatiliaji, tathmini, ujifunzaji na uboreshaji ........ 61
5.8.1 Mbinu za Ufuatiliaji ........ 61
5.8.2 Taratibu za Tathmini ........ 62
5.8.3 Ujifunzaji na Uboreshaji wa Utekelezaji wa Mkakati ........ 63
5.8.4 Uchambuzi wa Hatari za Kimkakati na Hatua za Kukabiliana Nazo ........ 65
VIAMBATISHO ........ 71
Kiambatisho Na. 1: Jedwali la Matokeo ........ 71
Kiambatisho Na. 2: Mpango Kazi Wenye Makadirio ya Gharama ........ 82
Kiambatisho Na. 3: Muhtasari wa Bajeti ........ 87

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **AZAKI** | Asasi za Kiraia |
| **CEDAW** | Mkataba wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake |
| **EAC** | Jumuiya ya Afrika Mashariki |
| **EMK** | Eneo la Matokeo ya Kimkakati |
| **LK** | Lengo la Kimkakati |
| **MSM** | Mamlaka za Serkali za Mitaa |
| **MTAKUWWA** | Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto |
| **OWM - SBUW** | Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu |
| **OWM -TAMISEMI** | Ofisi ya Waziri Mkuu -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **SDGs** | Maendeleo ya Malengo ya Maendeleo Endelevu |
| **TDHS-MIS** | Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria |
| **UDHR** | Azimio la Ulimwengu la Haki za Binadamu |
| **UNCRC** | Mkataba wa Haki za Mtoto |
| **UNFPA** | Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu |
| **UNICEF** | Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto |
| **WMJJWM** | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum |

# DIBAJI

Kuandaliwa kwa Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30 kunadhihirisha dhamira ya Tanzania ya kumaliza kabisa vitendo vya ukeketaji, ambavyo ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Duniani kote ukeketaji unatambulika kuwa ni aina ya ukatili ambao husababisha madhara makubwa ya kiafya, kisaikolojia na kiuchumi, jambo linalozuia wanawake na watoto wa kike kutimiza malengo yao hivyo kuathiri maendeleo ya Taifa. Kupitia mkakati huu, Serikali ya Tanzania inaonesha nia yake thabiti ya kujenga jamii ambayo kila mtoto wa kike anaishi bila hofu ya kukeketwa.

Mkakati huu umeandaliwa kufuatia kukamilika kwa tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2020/21–2024/25, ukiboresha jitihada za mkakati uliopita kwa kuzingatia mafanikio na changamoto zilizojitokeza. Dhamira kuu ni kuhakikisha kuwa hatua zinazochukuliwa zinaendana na mahitaji halisi ya jamii, zinafanya kazi kwa ufanisi na ni endelevu. Mafunzo na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mkakati uliopita zimesaidia kuboresha mbinu za utekelezaji, matumizi ya takwimu na mifumo ya uwajibikaji, ili kuhakikisha kuwa ukeketaji unatokomezwa kwa kasi zaidi kote nchini.

Mkakati huu unaendana kikamilifu na vipaumbele vya maendeleo ya taifa, ahadi za kikanda na mifumo ya kimataifa ya haki za binadamu, ikiwemo Itifaki ya Maputo ya Umoja wa Afrika na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa, hususan Lengo la 5.3 linalolenga kutokomeza vitendo vyote vyenye madhara kwa wanawake na watoto wa kike. Mkakati unatumia mbinu jumuishi ukitegemea tafiti, ambapo ushirikiano wa kisekta ni msingi wake mkuu. Kupitia ushirikishwaji wa wadau mbalimbali, wakiwemo wizara za kisekta, Asasi za Kiraia, pamoja na viongozi wa kimila na kidini, mkakati huu unalenga kujenga mshikamano na nguvu ya pamoja katika kutokomeza vitendo vya ukeketaji.

Chanzo cha mkakati huu ni mfumo mahususi wa utekelezaji unaobainisha kwa uwazi malengo ya kimkakati na hatua madhubuti katika maeneo muhimu. Maeneo hayo yanajumuisha kuimarisha mifumo ya kisera na kisheria iliyopo, kuiwezesha jamii kubadili mitazamo na mienendo kupitia afua zinazozingatia muktadha wa kitamaduni, kuboresha upatikanaji wa huduma bora kwa manusura na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi, pamoja na kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini. Kila hatua imebuniwa kushughulikia visababishi vya msingi vya ukeketaji na kuwezesha mabadiliko ya mitazamo kwenye jamii.

Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30 sio tu waraka wa kisera, bali ni tamko la dhamira ya pamoja na wito wa kuchukua hatua kwa Watanzania wote, unasisitiza ushirikishwaji wa jamii kama nguzo muhimu ya mafanikio. Tanzania inalenga kuharakisha jitihada za kuwa na jamii isiyo na ukeketaji ifikapo mwaka 2030 na hivyo kuhakikisha ustawi, usalama na usawa kwa kila mwanawake na mtoto wa kike.

Mhe. Dkt. Dorothy O. Gwajima (Mb)

**Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

# USULI

Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji kwa kipindi cha 2025/26–2029/30 unaakisi dhamira ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutokomeza ukeketaji, ambayo ni mila yenye madhara makubwa, inayokiuka haki za msingi za binadamu za wanawake na watoto wa kike, inayokwamisha maendeleo yao ya jumla na kuathiri maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Taifa. Uaandaaji wa Mkakati huu unaashiria kwamba Serikali imeazimia kulinda heshima, afya na mustakabali wa kila mwanamke na mtoto wa kike nchini.

Katika muktadha wa kimataifa, ukeketaji bado unaendelea kuwaathiri mamilioni ya wanawake na watoto wa kike, huku viashiria vya uwezekano wa kuendelea au kujirudia kwa vitendo hivyo katika baadhi ya jamii vikiongezeka. Hali hii huchangiwa na mchanganyiko wa watu wenye mila na desturi tofauti tofauti, changamoto za kijamii na kiutamaduni, uhamaji wa kuvuka mipaka, pamoja na ongezeko la idadi ya watu. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kupitia utekelezaji wa hatua za awali za kitaifa, kasi ya kupungua kwa kiwango cha ukeketaji bado haitoshi kufikia lengo la kutokomeza kabisa mila na desturi hii ifikapo mwaka 2030, kama ilivyoainishwa katika Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa, hususan Lengo la 5.3. Hivyo basi, mkakati huu wa awamu ya pili ni hatua ya kimakusudi ya kuharakisha juhudi za pamoja zilizoandaliwa kukabiliana na changamoto zinazoibuka na kuimarisha kwa kiwango kikubwa mwitikio wetu wa kutokomeza ukeketaji.

Mkakati huu unaakisi mabadiliko ya kimfumo yanayokusudiwa katika kuelekea hatua jumuishi zaidi, zinazoratibiwa vyema na zinazotekelezwa kwa ushirikiano wa kisekta. Umeandaliwa kwa umakini kupitia mashauriano ya kina na wadau mbalimbali, ukijumuisha uzoefu uliopatikana kutokana na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2020/21-2024/25 na kuzingatia matumizi ya tafiti katika kubuni afua. Kwa kutambua kwamba kutokomeza ukeketaji kunahitaji mshikamano wa kitaifa, mfumo uliobainishwa katika mkakati huu unasisitiza umuhimu wa kuimarisha ushirikiano kati ya wizara, idara na taasisi za serikali, pamoja na asasi za kiraia, wadau wa maendeleo, viongozi wa kimila, kidini na jamii kwa ujumla.

Mkakati huu, umeweka malengo na hatua mahususi za kimkakati kushughulikia visababishi mbalimbali vya ukeketaji. Hatua hizo zinajumuisha kuimarisha mifumo ya kisera na kisheria ili kuhakikisha ulinzi, uwajibikaji na nakuiwezesha jamii kuachana na mila zenye madhara kupitia afua za uhamasishaji zinazozingatia muktadha wa kiutamaduni, kuboresha upatikanaji wa huduma jumuishi za kinga na huduma kwa manusura wa ukeketaji, pamoja na kuimarisha mifumo ya takwimu kwa ajili ya ufuatiliaji na kufanya maamuzi yanayotegemea tafiti. Afua hizi zimekusudiwa kuweka mazingira wezeshi yatakayosaidia jamii kulinda haki na ustawi wa watoto wa kike.

Kwa msingi huo, ninawasihi wadau wote ikiwemo taasisi za Serikali, wadau wa maendeleo, asasi za kiraia, viongozi wa kijamii, familia na watu binafsi kuuchukulia mkakati huu kama jukumu la pamoja na kujitolea kikamilifu katika utekelezaji wake. Mafanikio ya juhudi hizi yanategemea mshikamano, uwajibikaji na dhamira ya pamoja. Kwa kushirikiana, tunaweza kuharakisha kutokomezwa kwa vitendo vya ukeketaji na kuhakikisha kwamba kila mtoto wa kike na mwanamke nchini anapata fursa ya kuishi bila hofu ya ukatili, kutimiza malengo yake na kuchangia kikamilifu katika maendeleo na ustawi wa Taifa. Tushirikiane kujenga mustakabali ambao ukeketaji utabaki kuwa historia.

Dkt. John A. K. Jingu
**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

# TAFSIRI YA DHANA

| Dhana | Tafsiri | Marejeo |
|---|---|---|
| **Ukeketaji** | Ni kitendo cha kuondoa sehemu au viungo vyote vya nje vya uzazi wa mwanamke au mtoto wa kike au kuumizwa kwa viungo vya uzazi kwa sababu zisizo za kitabibu. Kitendo hiki ni mila na desturi chenye madhara na kinatambuliwa kitaifa na kimataifa kama ukiukwaji wa haki za binadamu kwa wanawake na watoto wa kike. | WHO, 2022. https://www.who.int/newsroom/ fact-sheets/detail/female-genital-mutilation |
| **Manusura wa ukeketaji** | Mwanamke au mtoto wa kike aliyepitia ukeketaji na anayeendelea kuishi na athari za kimwili, kihisia au kisaikolojia. tafsiri hii itatumika kumtambua "mwathirika" wa ukeketaji | |
| **Ngariba** | Mtu yeyote anayetenda, kushiriki, kuwezesha au kusaidia utekelezaji wa ukeketaji, ikiwemo wahusika wa kimila au katika baadhi ya matukio anaweza kuwa mhudumu wa afya. | StatPearls. (2024). Female genital mutilation or cutting. National Center for Biotechnology Information. Retrieved from https://www.ncbi.nlm.nih.gov /books/NBK606106/ |
| **Ukeketaji wa kitabibu** | Ni kitendo cha ukeketaji kinachofanywa na mtoa huduma za afya, ikiwemo daktari, muuguzi au mkunga, kwa imani potofu kwamba ni salama au hupunguza madhara. Kitendo hiki ni ukiukwaji wa maadili ya taaluma ya afya na haki za binadamu. | WHO, 2010. "Global strategy to stop health-care providers from performing FGM." |
| **Mila mbadala za kuvusha rika** | Ni taratibu au sherehe mbadala zisizo na madhara na zinazotambuliwa na kukubalika na jamii zenye maadili ya kitamaduni ya mpito wa utoto kuelekea utu uzima bila kuhusisha ukeketaji au kusababisha madhara ya kimwili, kisaikolojia au kijamii. | Population Council, 2020. "Evidence to End FGM/C: ARP Evaluation in Kenya." |
| **Ukatili wa kijinsia** | Ni kitendo chochote chenye madhara kinachofanywa dhidi ya mtu kwa misingi ya jinsia yake bila ridhaa yake, ikijumuisha ukatili wa kimwili, kingono, kisaikolojia na kiuchumi. Ukeketaji ni mojawapo ya aina za ukatili wa kijinsia. | UNHCR, 2021. https://www.unhcr.org/gender-based-violence.html |
| **Mtoto** | Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto, Sura ya 13, Kifungu cha 4(1), mtoto ni mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na minane (18). | UNCRC, 1989. Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto |
| **Ulinzi wa mtoto** | Ni mifumo, afua na shughuli zinazolenga kuzuia, kutambua na kukabiliana na unyanyasaji, unyonyaji, utelekezwaji na vitendo vyote vya ukatili dhidi ya mtoto, ikijumuisha ukeketaji. | UNICEF, 2020. "Child Protection Strategy." |
| **Kamati ya Ulinzi wa wanawake na watoto** | Ni timu ya wadau mbalimbali iliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuzuia, kutambua na kushughulikia matukio ya vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ikiwemo ukeketaji. | Save the Children, 2019. "Community-Based Child Protection Mechanisms." |
| **Ushirikishwaji wa Jamii** | Ni mchakato shirikishi unaohusisha jamii katika hatua zote za msingi za kutokomeza vitendo vya ukeketaji. Jamii inatarajiwa ihusike kwenye | UNICEF, 2020. "Community Engagement Standards." |

| | | |
|---|---|---|
| | kubuni, kupanga, kutekeleza na kufanya tathimini. | |
| **Mbinu inayozingatia Haki za Binadamu** | Ni dhana inayozingatia haki za binadamu kuwa chanzo cha upangaji na utekelezaji wa programu na afua zote. Unasisitiza ushiriki, uwajibikaji, usawa na kutokubagua kama misingi mikuu ya utekelezaji. | OHCHR, 2006. "Frequently Asked Questions on a HRBA to Development Cooperation." |
| **Mila na Desturi za kijamii** | Ni imani, matarajio na kanuni zinazokubalika kijamii na kuongoza mienendo ya watu ndani ya kundi au jamii. Katika muktadha wa ukeketaji, hurejelea matarajio ya kijamii yanayodumisha au kuhalalisha desturi hiyo. | UNICEF Office of Research, 2020. "Social Norms and Harmful Practices." |
| **Ukeketaji wa Kuvuka Mipaka** | Ni kitendo cha kuwavusha wanawake au watoto wa kike nje ya mipaka ya kitaifa kwa lengo la kufanyiwa ukeketaji katika maeneo ambayo udhibiti wa sheria ni dhaifu au hazitekelezwi kikamilifu. | UNFPA & UNICEF, 2021. "Accelerating Change to End FGM." |
| **Ridhaa** | Ni kukubali kwa hiari kushiriki katika kitendo fulani, kinachotolewa na mtu mwenye uwezo wa kisheria na kiakili kufanya uamuzi. Katika muktadha wa ukeketaji, ridhaa ya mtoto haina uhalali wa kisheria na haiwezi kutumika kuhalalisha kitendo hicho. | UNFPA, 2020. "Consent in Sexual and Reproductive Health." |
| **Kupinga Ukeketaji** | Ni msimamo wa kitaifa na kimataifa unaotaka kutokomeza kabisa ukeketaji katika hali zote bila ubaguzi au sababu yoyote. | UN Resolution A/RES/67/146, 2012 |
| **Eneo Salama** | Ni mazingira ambayo mtu anajihisi salama, anaheshimiwa na analindwa dhidi ya ukatili. Maeneo haya ni muhimu kwa wanawake na watoto wa kike waliopitia ukeketaji na aina nyingine za ukatili wa kijinsia. | UN Women, 2018. "Creating Safe Spaces for Women and Girls." |
| **Unyanyapaa** | Ni mtazamo hasi au ubaguzi unaoelekezwa kwa waliofanyiwa ukeketaji au familia zinazokataa desturi hiyo. Hali hii inaweza kusababisha kutengwa katika jamii, upweke au hisia za aibu. | WHO, 2018. "Mental Health and FGM." |
| **Mifumo ya Ulinzi** | Taratibu za kisheria, kijamii, kiafya zilizobuniwa kuzuia ukeketaji na kuwalinda watu walio katika hatari. | Plan International, 2019. "Strengthening Child Protection Systems." |
| **Uwezeshaji** | Ni mchakato unaowajengea uwezo wanawake na watoto wa kike kufanya maamuzi yanayohusu miili yao, afya, elimu na maisha ya kiuchumi. Uwezeshaji huimarisha uwezo wa kujilinda dhidi ya mila na desturi zenye madhara ikiwemo ukeketaji. | UN Women, 2020. "Women's Empowerment Principles." |
| **Nyumba Salama** | Ni makazi ya muda yanayotoa hifadhi salama kwa wanawake na watoto wa kike wanaokimbia vitendo vya ukeketaji, ndoa za utotoni na vitendo vingine vya ukatili. | Equality Now, 2021. "Safe Houses in East Africa." |
| **Wafanya Maamuzi** | Ni taasisi au watu wenye dhamana kisheria au kimaadili ya kulinda, kuheshimu na kutekeleza haki za binadamu, hususan kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi. | OHCHR, 2006. "Frequently Asked Questions on HRBA." |
| **Mila na desturi zenye Madhara** | Ni imani na kanuni zinazokubalika katika baadhi ya jamii zinazosababisha madhara ya kimwili au kisaikolojia, hasa kwa wanawake na watoto wa kike, ikiwemo ukeketaji, ndoa za utotoni na vitendo vingine vinavyokiuka haki za binadamu. | UNCRC General Comment No. 13, 2011. |

| | | |
|---|---|---|
| **Ushirikishwaji wa Sekta mbalimbali** | Ni mkakati wa ushirikiano wenye uratibu wa pamoja unaohusisha wizara na taasisi za serikali, Asasi za Kiraia, sekta binafsi, jamii na wadau wa maendeleo, kwa kutambua kuwa jukumu la kutokomeza ukeketaji linahitaji afua jumuishi. | UNFPA–UNICEF Joint Programme, 2020 |
| **Kinga** | Ni hatua na programu zinazolenga kuzuia ukeketaji kabla haujatokea, ikiwemo elimu kwa umma, kampeni za uhamasishaji, majadiliano ya jamii, utekelezaji wa sheria na kukuza mila mbadala za kuvusha rika. | UN Women, 2021. UN Women, 2021. "FGM Prevention Toolkit." |
| **Huduma za Mwitikio** | Ni huduma na msaada unaotolewa kwa watu waliopitia ukeketaji au walio katika hatari, ikiwemo makazi ya muda, huduma za afya, msaada wa kisaikolojia, msaada wa kisheria na huduma za ulinzi. | WHO, 2016. WHO, 2016. "Health Care for Women and Girls Subjected to FGM." |
| **Malengo ya Maendeleo Endelevu** | Ni orodha ya malengo 17 ya kimataifa yaliyoanzishwa na Umoja wa Mataifa mwaka 2015, yakilenga kutokomeza umaskini, kulinda mazingira na kuhakikisha amani na ustawi kwa wote ifikapo mwaka 2030. Lengo la 5.3 linahusu kutokomeza vitendo vyote vyenye madhara, ikiwemo ukeketaji na ndoa za utotoni. | United Nations, 2015. "Transforming Our World: 2030 Agenda for Sustainable Development." |
| **Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto** | Ni vitendo vyote vinavyosababisha au vinavyoweza kusababisha madhara ya kimwili, kingono, kisaikolojia au kiuchumi kwa wanawake na watoto | UN Women, 2022. UN Women, 2022. "VAWC Programming Essentials." |

# MUHTASARI WA MKAKATI

Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30 ni nyaraka ya kimkakati inayoainisha upya dhamira ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na mwelekeo wa kitaifa katika kutokomeza vitendo vya ukeketaji. Muhtasari huu unaeleza kwa jumla muundo, maudhui, sambamba na mpangilio wa mkakati. Aidha, mkakati umebainisha kuendelea kuwepo kwa vitendo vya ukeketaji licha ya juhudi mbalimbali zilizofanyika sambamba na dhamira ya nchi ya kufikia malengo ya kimataifa ya kutokomeza mila hii ifikapo mwaka 2030, kama ilivyoainishwa katika Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa.

Mkakati wa awamu ya pili umeandaliwa kutokana na mafanikio na mafunzo yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Mkakati wa kwanza wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2020/21–2024/25, ukibainisha mapungufu yaliyopo na changamoto zilizoibuka ikiwemo ukeketaji wa kuvuka mipaka na changamoto katika mifumo ya takwimu. Hivyo basi, mkakati huu unasisitiza hitaji la mwitikio wa haraka wa kitaifa, unaoratibiwa vyema na ambao ni endelevu.

Mkakati umezingatia maadili yanazozingatia haki za binadamu, mtazamo wa maslahi ya mtoto kwanza ushirikiano wa kisekta, ushirikishwaji wa jamii, usawa wa kijinsia na utekelezaji unaozingatia matokeo ya tafiti. Kanuni hizi zinahakikisha kuwa hatua zote za utekelezaji zinazingatia maadili, zina ufanisi na ni endelevu.

Pamoja na hayo, Mkakati huu umeandaliwa kupitia mchakato shirikishi na unaozingatia tafiti mbalimbali Kama vile; kikao cha awali na wadau wakuu, mapitio ya kina ya maandiko yaliyopo, mifumo ya kisera na kisheria ya kitaifa na kimataifa, pamoja na jitihada zilizotekelezwa awali kuhusiana na ukeketaji, mashauriano baina ya wizara za kisekta, asasi za kiraia, mashirika ya maendeleo, taasisi za kitaaluma na utafiti, viongozi wa kimila na kidini, pamoja na jamii zilizoathirika, ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za msingi kutoka mikoa tisa ya Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Mara, Pwani, Dar es Salaam, Manyara, Singida na Dodoma, pamoja na kufanya uchambuzi wa mambo mtambuka na tathmini ya hali ya nchi ili kuainisha vipaumbele vya kimkakati na hatua za utekelezaji.

Jitihada zilizotekelezwa chini ya Mkakati wa kwanza wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji (2020/21–2024/25) umeonesha mafanikio katika kupinga na kutokomeza vitendo vya ukeketaji. Mafanikio hayo yanatoa msingi muhimu wa uundaji wa Mkakati wa awamu ya pili. Sambamba na hilo changamoto za utekelezaji wa Mkakati uliopita ikiwemo mapungufu ya mifumo ya takwimu na taarifa, upungufu wa rasilimali fedha na ukeketaji wa kuvuka mipaka ya nchi. Maarifa haya yametumika kuunda suluhisho mahususi na kuboresha mbinu katika Mkakati wa 2025/26–2029/30 ili kushughulikia kwa ufanisi changamoto zilizojitokeza awali.

Lengo kuu la Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji ni Kupunguza kiwango cha ukeketaji nchini kwa 50% kutoka 8% mwaka 2024/2025 hadi 4% ifikapo mwaka 2029/30. Lengo hili linahakikisha kuwa wanawake na watoto wa kike wanakuwa salama dhidi ya ukeketaji na wanawezeshwa kutambua na kutimiza kikamilifu haki zao, utu wao na uwezo wao wa kijamii na kiuchumi. Katika kufanikisha lengo kuu la Mkakati ifikapo mwaka 2030 ni muhimu kuzingatia malengo matano ya kimkakati ambapo kila lengo linashughulikia eneo mahususi na muhimu katika jitihada za kitaifa za kutokomeza ukeketaji ambayo ni (i) Kuimarisha utekelezaji wa mifumo ya kisera na kisheria ya kutokomeza ukeketaji, (ii) Kuwezesha jamii na watu binafsi kuachana na ukeketaji, (iii) Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za kuzuia, utoaji taarifa na mwitikio, (iv) Kuimarisha uratibu, ushirikiano wa kisekta na uhamasishaji wa rasilimali na (v) Kuimarisha tafiti na kujifunza

Mkakati unatumia mbinu shirikishi ya utekelezaji kuanzia ngazi za kikanda na kitaifa, unabainisha majukumu ya wizara na taasisi za Serikali, asasi za kiraia, viongozi wa kimila na kidini, pamoja na jamii.

Aidha, Uratibu utafanyika kupitia mifumo rasmi iliyopo kama Kamati za Kitaifa na Vikundi Kazi vya Kisekta ili kuhakikisha ushirikiano wa matumizi bora ya rasilimali na ulinganifu wa afua.

Mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji ni msingi katika utekelezaji wa mkakati huu ambao unajumuisha; viashiria vinavyopimika na mifumo ya ukusanyaji na utunzaji wa takwimu, tathmini za mara kwa mara za utendaji, Utambuzi wa mafanikio, mapungufu na changamoto mpya na marekebisho ya wakati kulingana na mazingira yanayobadilika. Lengo likiwa kukuza uwazi, uwajibikaji na maboresho endelevu katika kipindi chote cha utekelezaji.

# 1


UNFPA
unicef
Sema
novo nordisk fonden
# Tokomeza Ukeketaji, piga namba
116

# SURA YA KWANZA: KUHUSU MKAKATI HUU

## 1.1 Utangulizi

Ukeketaji kwa wanawake na watoto wa kike bado ni mojawapo ya changamoto kubwa za kijamii na kiutamaduni nchini, unaoathiri maelfu ya wanawake na watoto wa kike. Kitendo hiki kinatambuliwa kimataifa kama ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na kinaendelea kujitokeza katika baadhi ya jamii kutokana na imani na mila zilizokita mizizi kwa muda mrefu. Ukeketaji unahusisha taratibu mbalimbali zikiwemo kuondolewa kwa sehemu au viungo vyote vya nje vya uzazi wa mwanamke au mtoto wa kike au kuumizwa kwa viungo hivyo kwa sababu zisizo za kitabibu. Shirika la Afya Duniani (WHO) linaainisha ukeketaji katika aina nne, kulingana na ukali na athari zake kiafya. Kitendo hiki hakina faida zozote za kitabibu na kinatambuliwa duniani kote kama ni ukatili.

Kwa mtazamo wa kimataifa, ukeketaji unapatikana zaidi katika nchi za Afrika, Mashariki ya Kati na baadhi ya maeneo ya Asia, huku viwango vya ueneaji vikibainika kutofautiana kati ya nchi na kanda. Takwimu za Shirika la Afya Duniani za mwaka 2021 zinaonyesha viwango vya juu sana katika nchi kama Somalia (asilimia 98), Guinea (asilimia 97) na Misri (asilimia 87). Kufikia mwaka 2024, inakadiriwa kuwa zaidi ya wanawake na watoto wa kike milioni 230 duniani kote wamepitia ukeketaji, ongezeko la takribani asilimia 15 tangu mwaka 2016. Ongezeko hili linaelezewa kwa kiasi kikubwa na ukuaji wa idadi ya watu, pamoja na mwenendo unaoleta wasiwasi wa ukeketaji kufanywa na baadhi ya wahudumu wa afya. Bara la Afrika linaendelea kubeba mzigo mkubwa zaidi, likiwa na takribani visa milioni 144, likifuatiwa na Asia (takribani milioni 80) na Mashariki ya Kati (takribani milioni 6). Inakadiriwa pia kuwa takribani asilimia 40 ya manusura wa ukeketaji wanaishi katika maeneo yenye migogoro au yaliyo katika hali tete, ambako upungufu wa rasilimali na vipaumbele vya dharura huathiri jitihada za kutokomeza desturi hii. Pamoja na changamoto hizi, mafanikio yameonekana katika baadhi ya nchi za Afrika, ikiwemo Ethiopia, Kenya na Tanzania, ambako viwango vya ukeketaji vimepungua kwa zaidi ya asilimia 30 katika miongo ya hivi karibuni.

Kwa mujibu wa takwimu za UNICEF za mwaka 2024, Afrika inaendelea kuwa na idadi kubwa zaidi ya manusura wa ukeketaji duniani, ikikadiriwa kuwa na zaidi ya visa milioni 144. Desturi hii imejikita zaidi katika ukanda unaoanzia Afrika Magharibi hadi katika nchi za Pembe ya Afrika, huku nchi kama Somalia, Guinea, Mali, Sudan na Misri zikiwa na viwango vya juu sana vya ueneaji (zaidi ya asilimia 80). Hata hivyo, kama ilivyoelezwa awali, nchi kadhaa ikiwemo Tanzania zimeonesha maendeleo ya kupunguza kiwango cha ukeketaji katika kipindi cha miaka ya karibuni.

Nchini Tanzania, ukeketaji bado ni suala nyeti linalohitaji hatua za kimkakati. Kwa mujibu wa Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022 (TDHS-MIS), kiwango cha kitaifa cha ukeketaji kwa wanawake wenye umri wa miaka 15 - 49 ni asilimia 8, ikiwa ni pungufu kidogo ikilinganishwa na tafiti za awali. Mikoa ambayo ukeketaji umepungua kwa jitihada kubwa waliyoionesha. Mikoa ambayo ukekeketaji umeshuka kati ya mwaka 2015/16 hadi 2022/23 ni pamoja na Mkoa wa Manyara ambapo, kiwango cha ukeketaji kimepungua kutoka 58% hadi 43%, Mkoa wa Dodoma kutoka 41% hadi 18%. Aidha, Mikoa ya Mara kutoka 32% hadi 28% na Singida kutoka 31% hadi 20%. Serikali inaendelea na juihada za kukabiliana na ukeketaji kwa Mikoa ambayo kiwango kimeongezeka ikiwa ni pamoja na Arusha ambapo, ukeketaji umeongezeka kutoka 41% hadi 43%, Tanga kutoka 14% hadi 19%, Iringa kutoka 8% hadi 12% na Morogoro kutoka 9% hadi 10%. Ukeketaji unajitokeza zaidi miongoni mwa jamii za Wamasai, Wakurya, Wanyaturu, Wairaqw, Warangi na Wagogo na kwa kiasi kikubwa hufanywa na wazee wa kimila kwa kushirikiana na mangariba kwa kutumia zana za jadi. Aina ya pili ya ukeketaji (kukatwa na kuondolewa kwa nyama) ndiyo inayojitokeza zaidi. Aidha, kumekuwepo na mwelekeo wa kutisha wa ukeketaji kufanywa kwa watoto wa kike wenye umri mdogo zaidi, wakiwemo hata watoto wachanga. Mwelekeo huu unalenga kukwepa ufuatiliaji wa kisheria, kupunguza upinzani kutoka kwa watoto na kuepuka hatari za kisheria. Takwimu zinaonesha kuwa watoto wa kike wanaoishi vijijini wana uwezekano wa kufanyiwa ukeketaji mara 2.5 zaidi ikilinganishwa na wenzao wa

mijini (asilimia 12.7 dhidi ya asilimia 5.3). Taswira hii inatoa funzo la umuhimu wa kuwekeza katika Mikoa ya kipaumbele ambayo ukeketaji bado upo kwa kiwango kikubwa.

Jedwali lifuatalo linaonesha muhtasari wa aina nne za ukeketaji zilizopo nchini Tanzania, kwa kuzingatia uainishaji wa Shirika la Afya Duniani na kubainisha tofauti za kikanda katika utekelezaji wa desturi hii.

**Jedwali Na. 1: Aina za Ukeketaji kwa Mikoa Iliyochaguliwa**

| **Na.** | **Mkoa** | **Aina za Ukeketaji Zinazotekelezwa** |
|---|---|---|
| 1 | Dar es Salaam | Aina ya I (*Clitoridectomy* - kukata au kuondoa sehemu ya juu ya uke ijulikanayo kama kisimi); Aina ya IV (*symbolic pricking, reinfibulation* - kuchoma choma eneo la uke au kuparua kwa ajili ya kutoa damu au kuchoma moto).wanaokeketwa ni wahamiaji kutoka nje ya mkoa wa Dar es salaam |
| 2 | Pwani | Aina ya I na II (*Excision* - kuondoa kisimi pamoja na mashavuya ndani na wakati mwingine ya nje ya uke); aina hii ni ya ukeketaji ipo zaidi kwa wahamiaji kutoka nje ya mkoa wa Pwani |
| 3 | Tanga | Aina ya I na IV; mara nyingi huwa sehemu ya unyago |
| 4 | Singida | Aina ya II na III (*Infibulation*- Kushona na kuziba tundu la uke); hutekelezwa kwa zana za jadi zisizo za kitabibu |
| 5 | Arusha | Aina ya I, II na IV huhusishwa na mila za jamii za wafugaji |
| 6 | Dodoma | Aina ya I na II; hutekelezwa zaidi vijijini kwa kutumia zana za jadi |
| 7 | Mara | Aina ya II na III; hutekelezwa kama sehemu ya unyago na tohara |
| 8 | Kilimanjaro | Aina ya I na II; pamoja na aina ya IV katika mila za maandalizi ya kupevuka |
| 9 | Manyara | Aina ya II na III; inahusishwa na misingi ya mila na desturi na kuvusha rika. Aidha , aina hizi mbili za ukeketaji huwa kali zaidi kwa jamii hii na imeshikamana vyema na mila na desturi |

Nchini Tanzania, ukeketaji ni kosa la jinai kwa mujibu wa Kifungu cha 160 (1) na (2) cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, Toleo lililofanyiwa Marejeo la mwaka 2025. Adhabu kwa mkosaji ni faini isiyopungua shilingi milioni mbili za Kitanzania, kifungo cha miaka mitano hadi kumi na tano au adhabu zote kwa pamoja. Mahakama pia inaweza kuamuru fidia kwa aliyeathiriwa. Tanzania imeendelea kuthibitisha dhamira yake ya kutokomeza ukeketaji kupitia majukwaa ya kikanda na kimataifa, ikiwemo kuridhia Itifaki ya Maputo ya Umoja wa Afrika na kutekeleza Lengo la Maendeleo Endelevu la Umoja wa Mataifa namba 5.3, linalolenga kutokomeza vitendo vyote vyenye madhara ifikapo mwaka 2030. Aidha, Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto unaunga mkono jitihada hizi.

Pamoja na juhudi za Serikali, mchango wa Asasi za Kiraia na wanamabadiliko wa kijamii ni muhimu katika kuhamasisha jamii, kuendeleza mila mbadala za kupevuka na kutoa msaada kwa manusura wa ukeketaji. Hata hivyo, maendeleo bado yanakabiliwa na changamoto za imani za jadi zilizojengeka kwa muda mrefu, pamoja na upungufu wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa sheria na elimu kwa umma. Katika maeneo mengi, ukeketaji bado unaonekana kama sharti la kupevuka au ndoa, hali inayodumisha ukosefu wa usawa wa kijinsia na kudhoofisha mamlaka na haki za watoto wa kike.

## 1.2 Umuhimu wa Mkakati

Kuandaliwa kwa Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30 ni hatua muhimu na ya kimkakati katika juhudi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kutokomeza kabisa ukeketaji ifikapo mwaka 2030. Mkakati huu umeandaliwa ili kutoa mwitikio wa kitaifa ulio jumuishi, endelevu na unaoratibiwa vyema katika kushughulikia madhara ya kiafya, kijamii, kiuchumi na kisaikolojia yanayotokana na ukeketaji kwa wanawake na watoto wa kike, pamoja na visababishi vya msingi vinavyoendeleza desturi hii.

Kwa ujumla, ukeketaji wa wanawake na watoto wa kike husababisha madhara makubwa na ya muda mrefu ambayo mara nyingi hayarekebishiki na huathiri kwa kiasi kikubwa afya ya kimwili, kingono, uzazi na afya ya akili kwa manusura. Wanawake na watoto wa kike waliokeketwa wako katika hatari kubwa ya kupata maambukizi sugu ya njia ya mkojo, matatizo ya hedhi, pamoja na changamoto kubwa wakati wa ujauzito na kujifungua. Changamoto hizo ni pamoja na uchungu wa muda mrefu wakati wa kujifungua, kutokwa damu nyingi baada ya kujifungua, kutokea kwa fistula ya uzazi, kuongezeka kwa uwezekano wa upasuaji wa kujifungua, pamoja na vifo vya mtoto wakati au baada ya kuzaliwa. Madhara haya si tu yanahatarisha maisha ya mama na mtoto, bali pia yanaongeza mzigo mkubwa kwa mfumo wa huduma za afya ya uzazi nchini Tanzania, ambao tayari unakabiliwa na upungufu wa rasilimali.

Aidha, manusura wa ukeketaji mara nyingi hukumbwa na matatizo ya muda mrefu ya afya ya uzazi, ikiwemo maumivu na kutokuridhika wakati wa kujamiiana, hali inayoweza kusababisha migogoro ya kifamilia na msongo wa mawazo. Kwa upande wa afya ya akili, ukeketaji unahusishwa na athari mbalimbali za muda mfupi na muda mrefu, ikiwemo wasiwasi mkubwa, mfadhaiko msongo wa mawazo unaotokana na tukio la kutisha pamoja na majeraha ya kudumu ya kisaikolojia. Athari hizi hujitokeza kwa kiwango kikubwa zaidi miongoni mwa wanawake na wasichana waliokeketwa wakiwa katika umri mdogo, mara nyingi bila ufahamu wala ridhaa yao. Madhara haya ya kiafya yanawakilisha ukiukwaji wa moja kwa moja wa haki ya kufurahia kiwango cha juu kabisa cha afya ya mwili na afya ya akili, kama inavyotambuliwa chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu, ikiwemo Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto na Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (*CEDAW*).

Mkakati huu umeandaliwa kwa kuzingatia misingi saba kiutendaji ambayo imeainishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 2: Misingi ya uandaaji wa Mkakati**

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Suluhisho endelevu na linaloweza kushughulikia madhara ya ukeketaji** | **Ulinganifu wa nyenzo na mifumo muhimu ya kisheria ya kikanda** | **Kuchangia juhudi na ahadi zinazoendelea za Tanzania za kutokomeza ukeketaji na aina nyingine za ukatili dhidi ya wanawake na watoto** | **Husaidia kukabiliana na changamoto za kijamii na kiuchumi zinazosababishwa na ukeketaji kwa watu binafsi, familia na jamii ya Tanzania kwa ujumla** | **Kujifunza na kutokana na utekelezaji wa afua na mikakati ya awali, ikiwemo Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2020/2021–22024/025,** | **Kushughulikia mbinu mpya za ukeketaji, ikiwemo ukeketaji unaofanywa na watoa huduma za afya na ukeketaji wa kuvuka mipaka ya nchi.** | **Kuhakikisha ulinganifu wa mkakati na Lengo la Maendeleo Endelevu namba 5, shabaha ya 5.3, inayolenga kutokomeza vitendo vyote hatarishi ifikapo mwaka 2030.** |

### 1.2.1 Umuhimu wa Mkakati Kijamii na Kiuchumi

Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26-2029/30 ni muhimu kwa kuwa unatoa suluhisho jumuishi la kushughulikia changamoto za kijamii na kiuchumi zinazosababishwa na ukeketaji kwa watu binafsi, familia na jamii. Katika ngazi ya kaya, kushughulikia madhara yatokanayo na ukeketaji ikiwemo maambukizi, kulazwa hospitalini kwa muda mrefu, changamoto wakati wa kujifungua na madhara ya kisaikolojia hugharimu fedha nyingi, hususan kwa familia za vijijini na zenye

kipato cha chini. Shinikizo hili la kifedha hulazimisha kaya kuelekeza rasilimali kwenye matibabu badala ya mahitaji ya msingi kama elimu, lishe na makazi, hali inayoongeza umaskini na kuongezeka kwa ukosefu wa usawa wa kijinsia.

Katika ngazi ya taifa, ukeketaji huongeza changamoto za afya ya Jamii kwa kuongeza mahitaji ya huduma ghali kama huduma za dharura za uzazi, huduma za afya ya akili na upasuaji wa kurekebisha madhara. Huduma hizi mara nyingi hukabiliwa na upungufu wa rasilimali ndani ya mfumo wa huduma za afya nchini. Changamoto hii hudhoofisha uwezo wa taifa kutoa huduma za afya zilizo jumuishi na zenye usawa kwa wananchi wote.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani, gharama za kushughulikia madhara ya kiafya ya ukeketaji duniani kote zingefikia takribani dola za Marekani bilioni 1.4 kwa mwaka endapo mahitaji yote ya matibabu yangetimizwa. Hapa Tanzania, gharama hizi zinaweza kuchukua sehemu kubwa ya bajeti ya kila mwaka ya afya, zikikaribia wastani wa asilimia 10 na kufikia hadi asilimia 30 katika baadhi ya nchi. Bila kuchukua hatua za haraka, gharama hizi zinakadiriwa kuongezeka kwa zaidi ya asilimia 50 ifikapo mwaka 2050 kutokana na ongezeko la idadi ya watu na kuendelea kwa vitendo vya ukeketaji. Kinyume chake, endapo ukeketaji utatokomezwa sasa, gharama za huduma za afya zitaokolewa kwa asilimia 60 ifikapo mwaka 2050. hivyo basi, utekelezaji wa mkakati huu unaweza kuiletea sekta ya afya unafuu wa kifedha nchini.

Ukeketaji husababisha kupungua kwa ufaulu na kushindwa kumaliza masomo miongoni mwa watoto wa kike, kwani wengi huacha shule baada ya kufanyiwa ukeketaji. Aidha, mila hii huchochea ndoa za utotoni na kupunguza ushiriki wa wanawake katika soko la ajira. Matokeo haya huendeleza umaskini wa kizazi hadi kizazi, hupunguza uzalishaji wa Taifa na kukwamisha maendeleo endelevu. Kwa mantiki hiyo, ukeketaji unakinzana moja kwa moja na matarajio ya maendeleo ya Taifa kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA Toleo la Pili 2024/25–2028/29), pamoja na mifumo ya kimataifa ikiwemo Lengo la Maendeleo Endelevu namba 5 (usawa wa kijinsia) na Lengo namba 8 (ukuaji wa uchumi jumuishi).

### 1.2.2 Ulinganifu wa Mkakati Kisera na Kisheria

Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30 umeandaliwa ili kuimarisha shughuli za kutokomeza ukeketaji na aina nyingine za ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Mkakati huu unaendana na mifumo mbalimbali ya kisera na kisheria ya kitaifa inayolenga kulinda haki za binadamu na kukuza usawa wa kijinsia.

Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 Kifungu 160 (1) na (2) kinaeleza kuwa, adhabu ya mtu atakayekiuka kifungu cha sheria, adhabu yake ni faini isiyopungua milioni 2 au kifungo kisichopungua miaka 5 lakini kisichozidi miaka 15 au vyote kwa pamoja na kuamriwa kulipa faini isiyozidi shilingi milioni 1 au vyote kwa pamoja. Vile vile Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kifungu cha 169A (1) na (2) kinaeleza kuwa, adhabu yake ni kifungo cha miaka isiyopungua 5 na isiyozidi miaka 15 au faini isiyozidi shilingi milioni 1 au vyote kwa pamoja na kuamriwa kulipa fidia ya kiasi kitakachoamriwa na mahakama kwa yule aliyetendewa kosa hilo kwa maumivu aliyosababisha mtu huyo.

Mkakati huu pia unaendana na Sheria ya Mtoto, Sura ya 13, inayotoa mfumo imara wa kisheria wa ulinzi wa watoto kwa kuthibitisha haki yao ya kuishi salama na kuwalinda dhidi ya vitendo vyenye madhara kama ukeketaji. Vilevile, mkakati unaunga mkono utekelezaji wa sheria ndogo za serikali za mitaa zinazoshughulikia ukeketaji katika ngazi ya jamii kwa kuimarisha uwajibikaji na hatua za kijamii. Aidha, mkakati umeoanisha utekelezaji wake na jitihada zilizopo chini ya Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2021–2025 na Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA Toleo la Pili 2024/25-2028/29). Kupitia kuimarisha mifumo ya Kisera na Kisheria na kuunganisha afua ndani ya mwitikio mmoja wa kitaifa, mkakati wa 2025/26-

2029/30 unaweka Tanzania katika nafasi nzuri ya kupiga hatua kubwa kuelekea kutokomeza ukeketaji ifikapo mwaka 2030.

### 1.2.3 Ulinganifu wa Kikanda na Kimataifa

Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26-2029/30 unaendana kwa karibu na nyenzo muhimu za kisheria na mifumo ya kikanda na kimataifa inayosisitiza dhamira ya Tanzania ya kutokomeza ukeketaji. Kikanda, mkakati huu unaongozwa na Itifaki ya Maputo, Mkataba wa Afrika ya Haki na Ustawi wa Mtoto, pamoja na ahadi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mifumo hii ina mchango muhimu katika kushughulikia changamoto ya ukeketaji wa kuvuka mipaka, ambapo watoto wa kike husafirishwa kuvuka mipaka ya kitaifa ili kufanyiwa ukeketaji katika maeneo yenye udhaifu wa utekelezaji wa sheria au uangalizi hafifu.

Katika ngazi ya kimataifa, mkakati huu unachangia moja kwa moja utekelezaji wa Lengo la Maendeleo Endelevu namba 5, shabaha ya 5.3, linalotaka kutokomeza vitendo vyote vyenye madhara ikiwemo ukeketaji ifikapo mwaka 2030. Aidha, mkakati unaongozwa na kanuni za mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu, ikiwemo Mkataba wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (*CEDAW*), Mkataba wa Haki za Mtoto (*UNCRC*) na Azimio la Ulimwengu la Haki za Binadamu (*UDHR*). Ulinganifu huu unaonesha dhamira thabiti ya Tanzania katika kukuza usawa wa kijinsia, kulinda afya ya Jamii na kuendeleza maendeleo ya binadamu.

### 1.2.4 Mafunzo Kutokana na Afua za Awali

Uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa Mkakati wa awali wa Kutokomeza Ukeketaji (2020/21–2024/25) umeonesha wazi umuhimu wa kujifunza endelevu na kubuni afua zinazoweza kuendana na mabadiliko ya mazingira ya utekelezaji. Kutokana na msingi huo, Mkakati wa Awamu ya Pili (2025/26–2029/30) umejengwa kwa kuzingatia mafunzo yaliyopatikana, ukijumuisha matumizi ya mbinu bora na ubunifu uliotokana na ushirikiano wa wadau mbalimbali, ikiwemo Mpango wa Pamoja wa UNFPA–UNICEF wa Kutokomeza Ukeketaji, ili kuongeza ufanisi na matokeo ya utekelezaji. Aidha, mafunzo hayo yakisaisiwa na takwimu za Tafiti za Kitaifa (TDHS-MIS), yameuwezesha mkakati huu kubaini kwa usahihi maeneo ya kipaumbele, hususan katika mikoa 13 yenye viwango vya juu vya ukeketaji ambayo ni Arusha, Manyara, Mara, Singida, Dodoma, Iringa, Tanga, Iringa, Morogoro, Kilimanjaro, Njomba, Pwani na Dar Es Salaam.  Mwelekeo huu unalenga kuimarisha matokeo kupitia uwekezaji makini wa rasilimali pamoja na kuendeleza mifumo madhubuti ya ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji endelevu.

### 1.2.5 Hitaji la Mbinu Jumuishi

Licha ya kuwepo kwa mifumo ya kisera na kisheria pamoja na jitihada zinazoendelea, ukeketaji bado unaendelea kutokana na imani za jamii zilizokita mizizi, mila na desturi zinazoendeleza mfumo dume, udhaifu wa mifumo ya uwajibikaji pamoja na mwelekeo unaoibuka wa ukeketaji unaofanywa na wahudumu wa afya. Takwimu zinaonyesha kuwa, ingawa kiwango cha kitaifa cha ukeketaji kimepungua kutoka asilimia 10 mwaka 2016 hadi asilimia 8 mwaka 2022, ukeketaji unaofanywa na wahudumu wa afya bado ni changamoto kubwa. Mangariba wanakadiriwa kuhusika na takribani asilimia 75 ya visa, huku wahudumu wa afya wakihusishwa na takribani asilimia 18 ya visa vya ukeketaji nchini.


Hatari ya mwelekeo huu inatokana na dhana potofu kwamba ukeketaji unaofanywa katika mazingira ya kitabibu ni "salama", ilhali bado husababisha madhara makubwa  ya kimwili na kisaikolojia, ni ukiukwaji wa maadili ya taaluma ya afya na hudhoofisha juhudi za jamii za kuachana kabisa na desturi hii. Kwa msingi huo, mkakati huu unasisitiza mbinu jumuishi inayotegemea haki za binadamu na tafiti, inayoshughulikia visababishi vya kijamii na kitamaduni, kukabiliana na mienendo mipya ya ukeketaji na kuweka kipaumbele katika ushirikiano wa kisekta, elimu kwa umma na mifumo madhubuti ya uwajibikaji.

### 1.2.6 Mabadiliko ya Kimkakati

Kuandaliwa kwa Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30 si mwendelezo wa afua zilizopita, bali ni muhimu katika mwitikio wa kitaifa. Mkakati huu umechochewa na kuhitimishwa kwa mkakati uliopita pamoja na uharaka wa kufikia lengo la kimataifa la mwaka 2030 kama ilivyoainishwa katika Malengo ya Maendeleo Endelevu. Kupitia kushughulikia visababishi vya msingi vya ukeketaji, kuimarisha mifumo ya ulinzi na kukuza usawa wa kijinsia, mkakati huu unatumia mbinu ya ushirikiano wa kisekta inayohusisha wadau mbalimbali katika ngazi za kikanda, kitaifa na jamii.

Mkakati umeandaliwa ili kufikia matokeo chanya na endelevu kupitia malengo yafuatayo yaliyounganishwa: utekelezaji madhubuti wa mifumo ya kisera na kisheria; kinga na mwitikio unaoongozwa na jamii; uwezeshaji wa kiuchumi wa familia na manusura; usimamizi wa maarifa na ujifunzaji; ushiriki wa watoto na vijana; ushirikishwaji wa wanaume na vijana wa kiume; pamoja na kuimarisha uratibu kati ya Asasi za Kiraia na wizara, idara na taasisi za Serikali ili kuhakikisha mwitikio wa pamoja wenye matokeo.

## 1.3 Mbinu za Uandaaji wa Mkakati huu




Uandaaji wa Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30 uliongozwa na mbinu jumuishi, shirikishi na inayotegemea tafiti. Mbinu hii ilihakikisha kuwa mkakati unajengwa juu ya hali halisi na uzoefu wa jamii zilizoathirika, unaendana na vipaumbele vya kitaifa pamoja na ahadi za kimataifa na unazingatia mafunzo yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua za awali. Mbinu mseto za utafiti na takwimu zilitumika, zikiwa zimepangwa katika awamu saba kuu kama ifuatavyo:

#### a) Mapitio ya Nyaraka na Uchambuzi wa Takwimu

Uandaaji wa Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30 ulihusisha mapitio ya kina ya sera, sheria, mikakati na taarifa zilizopo katika ngazi ya kitaifa na kimataifa. Mchakato huu ulilenga mifumo inayohusiana na ukeketaji, ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto, nyaraka za kitaifa zilizopitiwa zilijumuisha Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2020/21–2024/25, Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (Toleo la Pili 2024/25–2028/29), pamoja na Sheria ya Mtoto ya Mwaka Sura ya 13. Aidha, rejea za kikanda na kimataifa zilihusisha Mpango wa Kikanda wa Gharama wa Kutokomeza Ukeketaji wa Kuvuka Mipaka, Miongozo ya Kiufundi ya Mpango wa Pamoja wa UNFPA - UNICEF, pamoja na Taarifa za Maendeleo ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Mapitio haya yaliwezesha kubainisha mapungufu katika afua zilizopo, kuonesha muelekeo unaoibuka na vichocheo vya kijamii na kitamaduni vya ukeketaji, kutathmini juhudi na changamoto zilizopo pamoja na kuingiza mbinu bora katika usanifu na utekelezaji wa mkakati.

### b) Mashauriano ya Wadau na Ushirikishwaji wa Ngazi Mbalimbali

Uandaaji wa mkakati huu ulihusisha mashauriano na wadau pamoja na mbinu shirikishi. Kwa kutambua kuwa ukeketaji ni suala lililokita mizizi katika muktadha wa kijamii na kitamaduni, uandaaji wa mkakati ulihusisha ushirikishwaji wa wadau katika ngazi ya taifa, mikoa, halmashauri na jamii. Mashauriano haya yalihusisha makundi mbalimbali yakiwemo wizara, idara na mamlaka za Serikali, Asasi za Kiraia, mashirika ya kidini, viongozi wa kimila na kidini, mitandao ya vijana na ya kijamii, pamoja na manusura na watetezi wa ngazi ya jamii. Ushirikishwaji huu uliwezesha kupata uelewa wa kina wa visababishi ukeketaji na kuchangia katika usanifu wa mkakati kwa kuingiza maoni ya jamii, kuzingatia uelewa wa utamaduni na kuimarisha umiliki na mifumo ya uwajibikaji katika ngazi ya jamii.

### c) Mbinu Shirikishi zinazojumuisha Jamii

Katika kuhakikisha kuwa mkakati unaakisi kikamilifu uhalisia wa maisha ya jamii zinazoathirika zaidi na ukeketaji, mbinu shirikishi katika ngazi ya jamii zilitumika kwenye mikoa yenye viwango vya juu vya ukeketaji, ikiwemo Manyara, Dodoma, Singida na Mara. Mchakato huu ulijumuisha mahojiano ya kina na wadau muhimu na wenye ushawishi, wakiwemo viongozi wa kimila, viongozi wa kidini, walezi, mangariba na watekelezaji wengine wa kimila pamoja na manusura wa ukeketaji. Ushirikishwaji wa makundi hayo umewezesha kupatamitazamo ya jamii kuhusu masuala yanayohamasisha ukeketaji na fursa zinazoweza kuchochea mabadiliko. Maoni yaliyokusanywa yalichangia kwa kiasi kikubwa katika kuunda dira, malengo ya kimkakati, kanuni elekezi na nguzo za afua za Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30.

### d) Kikundi Kazi cha Wataalamu

Ili kuratibu na kuongoza mchakato wa uandaaji wa Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30, Kikundi Kazi cha Kitaifa cha Kiufundi cha Kutokomeza Ukeketaji ambacho kinajumuisha wataalamu kutoka wizara, idara ,Taasisi na Serikali, wadau wa maendeleo, kilitoa mwelekeo wa kimkakati pamoja na usimamizi wa kitaalamu katika hatua zote za uandaaji mkakati ili kuongeza ufanisi na utaalamu. Kikundi Kazi kiligawanywa katika vikundi vidogo vya kimaudhui vilivyoshughulikia maeneo muhimu ya mkakati, yakiwemo mifumo ya kisera na kisheria, ushirikishwaji wa jamii, utoaji wa huduma, mifumo ya uratibu, mienendo ya ukeketaji wa kuvuka mipaka, pamoja na ufuatiliaji na tathmini. Aidha, kila kikundi kidogo kilifanya uchambuzi wa kimaudhui, kuandaa sehemu husika za mkakati na kutoa mapendekezo ambayo yaliunganishwa kupitia vikao vya uthibitisho ili kuhakikisha mshikamano, ulinganifu na umiliki wa wadau. Katika mchakato wote, Kikundi Kazi kilihakikisha mkakati unaendana na kanuni za mabadiliko ya kijinsia, mbinu zinazozingatia haki za binadamu na viwango vinavyohakikisha ujumuishaji wa watu wenye ulemavu.

### e) Uchambuzi wa Hali Halisi

Uchambuzi wa kina wa hali halisi ulifanyika ili kutathmini mazingira ya sasa ya ukeketaji nchini Tanzania, kwa kuangalia viwango vya ukeketaji, muelekeo, visababishi vya msingi, tofauti za kikanda na mifumo iliyopo ya mwitikio. Uchambuzi huu ulitumia takwimu kutoka tafiti za kitaifa, ikiwemo Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria na Utafiti wa Viashiria Katika Makundi (*Multiple Indicator Cluster Survey - MICS)*, pamoja na tathmini za programu, taarifa za Asasi za Kiraia na taarifa za kimaelezo zilizokusanywa kupitia mashauriano ya jamii.

### f) Vikao vya kuthibitisha na kuboresha

Rasimu za mkakati ziliwasilishwa katika mfululizo wa vikao vya uthibitisho katika ngazi ya Taifa. Vikao hivi viliwakutanisha wadau kutoka sekta mbalimbali kwa lengo la kupitia, kujadili na kuboresha Mkakati. Msisitizo uliwekwa katika utekelezekaji wa afua zilizopendekezwa, upatikanaji wa rasilimali pamoja na kupima mafanikio kupitia viashiria. Maoni yaliyopatikana kupitia vikao hivyo yaliingizwa katika rasimu ya mkakati ili kuhakikisha unawakilisha makubaliano ya wadau wote nchini.

**g) Uthibitisho na Uidhinishaji wa Mwisho**

Mbinu za uandaaji wa mkakati zilihitimishwa kwa mchakato rasmi wa uthibitisho na uidhinishaji. Baada ya mapitio ya kina na mashauriano, rasimu ya mwisho ya mkakati iliwasilishwa kwa vyombo husika vya Serikali, ikiwemo Menejementi ya Wizara kwa ajili ya kuthibitishwa na kuidhinishwa rasmi. Uidhinishaji huu uliupa mkakati uhalali wa kisheria, ukaunganisha utekelezaji wake ndani ya mifumo ya mipango ya Taifa na kuhakikisha dhamira ya kisiasa pamoja na rasilimali zinazohitajika kwa utekelezaji wake. Hivyo, mkakati huu unatambuliwa rasmi na kupitishwa kama mfumo wa kitaifa wa Tanzania wa kutokomeza ukeketaji.

## 1.4 Mpangilio wa Mkakati

Sehemu hii inaeleza muundo na mtiririko wa kimantiki wa Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30. Lengo lake ni kuwaongoza watekelezaji wa mkakati kwa kuonesha namna kila sura inavyojengwa ili kuwasilisha mpango thabiti, unaotekelezeka na unaoelekeza hatua za kutokomeza ukeketaji. Uelewa wa mpangilio huu ni muhimu kwa wadau wote ili kuweza kutumia mkakati kwa ufanisi, kuelewa uhusiano wa maeneo yake na kubainisha majukumu na uwajibikaji katika utekelezaji.

Mkakati unaanza na Sura ya Kwanza ambayo ni utangulizi, inayoweka msingi kwa kutoa taarifa za awali kuhusu hali ya ukeketaji nchini Tanzania. Sura hii inaeleza mantiki ya kuandaa mkakati wa toleo la pili, inabainisha umuhimu wake  na kuweka kanuni elekezi zitakazoongoza utekelezaji wa afua zote. Aidha, sura hii inaeleza mbinu zilizotumika katika uandaaji wa mkakati, hatua inayochangia uwazi na kuimarisha uhalali wa msingi wake wa kitaalamu. Sura ya Pili inawasilisha uchambuzi wa kina wa hali na muktadha wa ukeketaji nchini Tanzania, ikijumuisha viwango, muelekeo, visababishi vya msingi, tofauti za kikanda na mifumo iliyopo ya mwitikio. Uchambuzi huu unatoa msingi wa ushahidi wa kitaifa unaoelekeza maamuzi ya kimkakati.

Sura ya Tatu inajengwa juu ya uchambuzi wa hali halisi kwa kufafanua muelekeo wa kimkakati. Sura hii inaainisha dira na dhima ya mkakati kwa Tanzania isiyo na ukeketaji, pamoja na lengo kuu la mkakati. Aidha, inaeleza kwa kina Malengo ya Kimkakati na kuthibitisha upya kanuni elekezi zitakazoongoza utekelezaji wa afua zote. Sura ya Nne inahusu mfumo wa mkakati ambao ndiyo mhimili wa mkakati. Ingawa mwelekeo wa jumla wa mfumo unatambulishwa katika Sura ya Tatu, Sura ya Nne inaelezea kwa kina vipengele vya utekelezaji. Kila lengo la kimkakati linafafanuliwa kwa undani pamoja na maeneo ya matokeo muhimu, afua mahususi za kimkakati na viashiria vinavyopimika kwa ajili ya ufuatiliaji wa maendeleo na tathmini ya matokeo.

Sura ya Tano inaainisha Utekelezaji, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini na inaweka mkakati katika hatua za utekelezaji kwa vitendo. Sura hii inaeleza mipangilio ya utekelezaji, ikiwemo mifumo ya uratibu katika ngazi ya taifa na ngazi ya jamii, mikakati ya ushirikishwaji wa wadau, pamoja na mipango ya uhamasishaji wa rasilimali. Vilevile, inawasilisha mfumo wa Ufuatiliaji, Tathmini na Ujifunzaji ili kuhakikisha ufuatiliaji wa maendeleo kwa utaratibu, kujifunza kutokana na utekelezaji na kufanya maboresho kulingana na mazingira yanayobadilika katika kipindi chote cha mkakati.

Hivyo, mkakati unajumuisha masuala mtambuka yanayotekelezwa katika sura zote, yakiwemo haki za binadamu, usawa wa kijinsia, ulinzi wa watoto wa kike, ujumuishaji jamii na uzingatiaji wa muktadha wa kiutamaduni. Masuala haya yameunganishwa ndani ya malengo ya kimkakati na mifumo ya utekelezaji ili kuhakikisha afua zote zinabaki kuwa za kimaadili, jumuishi na zinazozingatia mazingira halisi ya jamii. Uhusiano wa karibu kati ya sura mbalimbali unaimarisha mshikamano wa mkakati, kwa kuruhusu misingi ya awali na uchambuzi wa hali halisi kuongoza mfumo wa mkakati, kuelekeza utekelezaji na kuboresha kupitia ufuatiliaji na tathmini endelevu. Maudhui ya ziada kama bajeti au mifumo ya utekelezaji yanawasilishwa katika viambatisho ili kuongeza ufanisi wa matumizi ya mkakati.

# 2



Mtoto wa kike kuwa mstari wa mbele kukataa ukeketaji

# SURA YA PILI: UCHAMBUZI WA HALI NA MUKTADHA

## 2.1 Utangulizi

Licha ya hatua zilizopigwa katika kupunguza kiwango cha jumla cha ukeketaji nchini, mila na desturi hii bado inaendelea katika baadhi ya mikoa. Kwa mujibu wa Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022, kiwango cha kitaifa cha ukeketaji miongoni mwa wanawake wenye umri wa miaka 15 - 49 ni asilimia 8, ikilinganishwa na asilimia 10 mwaka 2015/16. Hata hivyo, wastani huu wa kitaifa unaonyesha kupungua kwa vitendo vya ukeketaji kwa baadhi ya mikoa kutokana na tofauti kubwa za kikanda na kikabila.

Ukeketaji nchini Tanzania unaendelezwa na mwingiliano wa desturi za kitamaduni, kiuchumi na kijinsia. Imani za jadi bado zinaunganisha ukeketaji na dhana za usafi, ustahiki wa kuolewa, kukubalika kijamii na heshima ya mwanamke. Vichocheo vya kiuchumi pia vinaendeleza ukeketaji. Katika baadhi ya jamii, ukeketaji huonekana kama sharti la mazungumzo ya mahari, huku mangariba na watekelezaji wengine wa kimila wakitegemea ukeketaji kama chanzo kikuu cha kipato. Ingawa ukeketaji umetajwa kuwa kosa la jinai chini ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 na Sheria ya Mtoto Sura ya 13, utekelezaji wa sheria bado ni dhaifu, hususan katika maeneo ya vijijini na ya mbali ambako uelewa wa sheria na uwezo wa vyombo vya ulinzi ni mdogo. Changamoto inayoibuka kwa kasi ni ukeketaji unaofanywa na wahudumu wa afya, ambapo baadhi ya wahudumu hao, kinyume na sheria za nchi na maadili ya taaluma, hufanya vitendo hivi kwa kisingizio cha usalama. Aidha, ukeketaji wa kuvuka mipaka unaendelea kuleta changamoto kubwa za utekelezaji wa sheria. Familia katika mikoa inayopakana na Kenya na Uganda huzidi kuwavusha watoto wa kike nje ya mipaka ya taifa ili kukwepa adhabu za kisheria za Tanzania, hali iliyobainishwa katika Mpango wa Kikanda wa Gharama wa Kutokomeza Ukeketaji wa Kuvuka Mipaka.

Tanzania imepiga hatua muhimu za kisera na kimfumo katika juhudi za kutokomeza ukeketaji kitaifa, kikanda na kima taifa.Juhidi hizo zinahusisha makubaliano ya Itifaki ya Maputo, Hati ya Afrika ya Haki na Ustawi wa Mtoto, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa hususan Lengo la 5.3, pamoja na Mpango wa Kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Kutokomeza Ukeketaji wa Kuvuka Mipaka. Katika ngazi ya kitaifa, Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA Toleo la Pili II 2024/25 - 2028/29) unatoa uwanda mpana wa kuunganisha jitihada mbali mbali za kutokomeza vitendo vya ukeketaji ili kuleta usawa wa kijinsia na ulinzi wa watoto wa kike.

Hata hivyo, changamoto za utekelezaji bado zinaendelea kuwepo. Tathmini ya Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2020/21 - 2024/25 ilibainisha vikwazo kadhaa ikiwemo upungufu wa rasilimali ifedha, udhaifu wa ushirikiano wa kisekta, ushirikishwaji duni wa jamii, pamoja na mifumo duni ya takwimu. Afua nyingi hazikuwa na malengo na ratiba zilizoainishwa wazi na wadau muhimu kama wanaume, vijana wa kiume na viongozi wa kidini hawakuhusishwa kikamilifu.

Ili kushughulikia mapungufu haya, Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26 - 2029/30 unapaswa kuhusisha mbinu ya ushirikiano wa kisekta, inayomweka manusura katika kiini cha afua na inayotegemea tafiti. Mafanikio ya mkakati yatategemea kuimarishwa kwa uwezo wa utekelezaji wa sheria, kuongezwa kwa ushirikiano wa kuvuka mipaka, upatikanaji wa rasilimali endelevu za kifedha na kuimarishwa kwa ushiriki wa jamii, sambamba na ushirikishwaji wa wanaume, vijana na viongozi wa kidini kamamabalozi wa mabadiliko ya kijamii.

## 2.2 Juhudi Zilizotekelezwa Chini ya Mkakati wa Mwaka 2020/21–2024/25

Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2020/21–2024/25 uliweka mfumo jumuishi wa kitaifa uliolenga kuharakisha kutokomezwa kwa ukeketaji nchini. Mkakati huo ulikuwa na hatua muhimu katika mapambano dhidi ya ukeketaji. Kupitia ushirikiano wa kisekta, mkakati ulilenga kuoanisha afua za kisheria, kiafya, kielimu na za kijamii ili kushughulikia tatizo la ukeketaji kwa mtazamo mpana na jumuishi.

### 2.2.1 Mafanikio Makuu




**a) Huduma zinazolenga manusura na maeneo salama**

Mkakati huu uliimarisha kwa kiasi kikubwa katika utoaji wa huduma kwa manusura wa ukeketaji na watoto wa kike walio katika hatari. Jumla ya nyumba salama 18 zilianzishwa au kuungwa mkono katika mikoa yenye viwango vya juu vya ukeketaji, ikiwemo Mara, Singida na Manyara ambapo zilitoa hifadhi, ushauri nasaha na msaada wa kisaikolojia, msaada wa kisheria na fursa za kuendelea na elimu kwa watoto wa kike walioathirika. Kufikia mwaka 2025, zaidi ya manusura 57,000 walipata huduma za afya ya kimwili na ya kiakili, ongezeko la mara nane ikilinganishwa na viwango vya awali vya mwaka 2019. Aidha, zaidi ya wanawake 78,000 waliokeketwa walibainishwa kupitia vituo vya afya, hatua iliyowezesha watoa huduma kutoa huduma stahiki na kukusanya takwimu muhimu.

Katika kipindi cha utekelezaji wa mkakati uliopita, jumla ya watoto wa kike 6,065 waliwekwa katika nyumba salama, huku watoto wa kike 659 wakilindwa kupitia afua za Madawati ya Polisi ya Jinsia na Watoto. Mafanikio haya yanaonyesha hatua kubwa kuelekea mbinu zinazozingatia haki za binadamu na zinazomweka mwathirika katika kiini cha afua. Aidha, upanuzi wa Madawati ya Polisi ya Jinsia na Watoto hadi kufikia zaidi ya 420 umeimarisha kwa kiasi kikubwa mifumo ya ulinzi na upatikanaji wa haki.

### 2.2.2 Hatua muhimu za Kisera na Kisheria

Katika nyanja ya kisheria, mkakati uliimarisha utekelezaji wa sheria zilizopo na kuunga mkono hatua za utekelezaji katika ngazi ya jamii. Kanuni ya Adhabu (Kifungu cha 169A) inaainisha adhabu kali kwa waarifu wanaohusika na vitendo vya ukeketaji, ikiwemo kifungo cha maisha kwa baadhi ya makosa. Katika kipindi cha mkakati, kesi 100 zinazohusiana na ukeketaji ziliripotiwa na kusababisha hukumu 88, ongezeko kubwa ikilinganishwa na hukumu moja pekee mwaka 2020. Halikadhalika, zaidi ya wataalamu 236 kutoka sekta za sheria, ustawi wa jamii na afya walipatiwa mafunzo kuhusu ushughulikiaji wa kesi za ukeketaji, hatua iliyoboresha ufanisi wa mashtaka na utoaji wa huduma kwa manusura.

Sheria ndogo ndogo za serikali za mitaa ziliandaliwa au kurekebishwa katika baadhi ya halmashauri, ikiwemo Manyara na Singida, hatua iliyoongeza uwezo wa utekelezaji wa sheria katika ngazi ya jamii. Baadhi ya halmashauri zilianzisha adhabu za faini na matamko ya hadharani ya mangariba kuomba radhi kama njia ya kuzuia vitendo hivyo. Aidha, kuingizwa kwa ahadi za kutokomeza vitendo vya

ukeketaji katika mipango na bajeti za serikali za mitaa angalau halmashauri saba kulionesha kuongezeka kwa umiliki wa kitaasisi katika mapambano dhidi ya ukeketaji.

#### 2.2.3 Kujenga uwezo na ushirikishwaji wa Jamii

Mkakati uliweka kipaumbele katika kujenga uwezo katika sekta mbalimbali na katika jamii. Zaidi ya watoto wa kike na wanawake 1,450 walipatiwa mafunzo ya haki zao kuhusiana na ukeketaji, afya ya uzazi na jinsia, usawa wa kijinsia na mifumo ya kisheria ya ulinzi. Mafunzo haya yalilenga mabaraza ya watoto, madawati ya ulinzi wa watoto na vilabu vya vijana, ingawa baadhi ya malengo ya kuwajengea uwezo walimu na familia zilizoainishwa kama "familia salama" hayakufikiwa kikamilifu.

Mkakati uliunga mkono usambazaji wa jumbe 20 muhimu kupitia nyenzo za Habari, Elimu na Mawasiliano na vipindi vya redio. Ingawa idadi hii ilikuwa chini ya lengo la awali, iliweka msingi wa ujumbe unaozingatia muktadha wa jamii na usikivu wa kitamaduni. Ushirikiano na Asasi za Kiraia, ikiwemo asasi ya Network Against Female Genital Mutilation (NAFGEM), Children's Dignity Forum (CDF) na C-Sema, uliwezesha uhamasishaji wa jamii, utekelezaji wa mila mbadala za kupevuka na mijadala ya wazi kwa kijamii, ambayo ni muhimu katika kubadili mila na desturi hatarishi. Zaidi ya mangariba 579 walitangaza hadharani kuachana na ukeketaji, hatua iliyoashiria mabadiliko muhimu ya kitamaduni kutokana na ushawishi wao katika jamii zinazozingatia mila za jadi.

### 2.3 Mafunzo muhimu yaliyopatikana

Tathmini ya Mkakati wa Kutokomeza Ukeketaji wa mwaka 2020/21-2024/25 ilibainisha masuala mbalimbali ambayo yalisaidia kujifunza katika kuandaa mkakati huu. Masuala hayo ni kama yalivyoorodheshwa katika mchoro ufuatao na maelezo yake hapa chini:

1. Uratibu madhubuti wa kisekta unahitaji mifumo na mipango ya kudumu iliyorasimishwa
2. Ushirikishwaji wa jamii unaoungwa mkono kwa dhati huleta mabadiliko endelevu ya kitabia
3. Mifumo ya kisheria ni muhimu iendane na uelewa wa jamii, uwezo wa kusimamia sheria na upatikanaji wa haki
4. Mifumo ya elimu na afya bado haijatumika kikamilifu kama majukwaa ya kuzuia na kutoa mwitikio kwa wakati
5. Kutokomeza vitendo vya ukeketaji kunapaswa kwenda sambamba na kushughulikia hali za kiuchumi, mila na desturi zinazochochea vitendo hivyo.
6. Uwekezaji wa muda mrefu ni muhimu katika huduma zinazozingatia manusura, mifumo ya takwimu na ujifunzaji.

#### a) Uratibu madhubuti wa kisekta unahitaji mifumo na mipango ya kudumu iliyorasimishwa

Utekelezaji wa mkakati uliopita ulionyesha wazi umuhimu wa ushirikiano wa kisekta katika kushughulikia visababishi tata vya ukeketaji. Hata hivyo, utekelezaji wake ulidhoofishwa na kukosekana kwa muundo wa kitaifa wa uratibu wenye mamlaka ya kisheria na kiutendaji. Wizara nyingi zilifanya kazi kwa kujitegemea, huku afua nyingi zikitekelezwa bila kuzingatia mpango wa pamoja wa utekelezaji, hali iliyosababisha kufanya shughuli zinazofanana katika eneo moja, matumizi yasiyo na ufanisi ya

rasilimali na mapungufu katika mifumo ya uwajibikaji. Katika baadhi ya mikoa, ushiriki wa sekta muhimu kama afya, elimu, haki na ustawi wa jamii ulikuwa wa vipindi na usio thabiti.

Zaidi ya hayo, kutokufanya kazi ipasavyo kwa baadhi ya majukwaa ya ufuatiliaji yaliyopaswa kuunganisha juhudi katika baadhi ya mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kulisababisha kukosekana kwa fursa za kuimarisha mshikamano wa utekelezaji katika maeneo hayo. Miundo hii inapaswa kuwajibika kwa upangaji wa kimkakati, ufuatiliaji wa utekelezaji na uratibu wa rasilimali kwa kuainisha wazi majukumu, ratiba na matokeo yanayotarajiwa kwa wadau wote.

**b) Ushirikishwaji wa jamii unaoungwa mkono kwa dhati huleta mabadiliko endelevu ya kitabia**

Jamii zilizoshirikishwa kikamilifu kupitia mbinu shirikishi kama vile mijadala ya vijiji, mila mbadala za kuvusha rika na ushiriki wa vinara wa mabadiliko wa ndani ya jamii zilionesha maendeleo dhahiri katika kubadili desturi za kijamii. Kwa mfano, mikoa ya Singida na Mara iliripoti ongezeko la ngariba waliotoa shuhuda za kutokuendelea na ukeketaji, pamoja na kuongezeka kwa utoaji wa taarifa za matukio ya ukeketaji kupitia mifumo ya ufuatiliaji wa jamii. Mafanikio haya hayakuonekana katika maeneo ambako afua zilikuwa za muda mfupi au ziliendeshwa kwa msukumo wa nje bila kujengwa juu ya mifumo ya jamii.

Funzo muhimu ni kwamba mabadiliko ya kudumu yanahitaji kuingiza afua za kutokomeza vitendo vya ukeketaji ndani ya mifumo iliyopo ya utawala kama vile halmashauri za vijiji, mabaraza ya watoto na kamati za ulinzi wa wanawake na watoto. Msaada unapaswa kwenda zaidi ya ushirikishwaji wa kawaida na kujumuisha kujenga uwezo, mipango midogo ya ruzuku, majukwaa ya kutambua mchango wa jamii na ushirikishwaji mahsusi wa makundi maalum yakiwemo vijana, wanaume na watu wenye ulemavu. Ushirikishwaji wa viongozi wenye ushawishi wa ndani kama wazee wa kimila, ngariba walioacha kukeketa na wanawake viongozi wanaoheshimika ni muhimu katika kubadilisha mtazamo wa kijamii katika kuhamasisha mbinu mbadala zisizo na madhara.

**c) Mifumo ya kisheria ni muhimu iendane na uelewa wa jamii, uwezo wa kusimamia sheria na upatikanaji wa haki**

Uwepo wa mifumo imara ya  kisera na kisheria inayokataza vitendo vya ukeketaji umechangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza vitendo vya ukeketaji katika maeneo mengi, hata hivyo bado utekelezaji ni changamoto katika maeneo yenye viwango vya juu vya ukeketaji. Changamoto za kijamii, rushwa, masuala ya usimamizi wa sheria, pamoja na utendaji vilichangia kudhoofisha uchunguzi na uendeshaji wa mashauri ya ukeketaji.

Katika kipindi cha mkakati uliopita, jamii ilihamasika kutoa taarifa za vitendo vya ukeketaji ingawa kwa kiwango kidogo. Kwa kipindi cha utekelezaji, takribani kesi 112 za vitendo vya ukeketaji viliripotiwa. Hata hivyo bado kesi nyingi zilitupiliwa mbali au hazikufikishwa mahakamani kutokana na mapungufu ya taratibu za kisheria. Vilevile, wigo mdogo kisheria katika kushughulikia kesi za wanawake watu wazima wanaokubali kufanyiwa ukeketaji kwa hiari unaacha mianya muhimu katika ulinzi na uwajibikaji.

Funzo jingine ni kuwepo kwa ukeketaji unaofanywa na baadhi ya wahudumu wa afya, unaotekelezwa kwa siri na kuifanya kazi ya utekelezaji wa sheria kuwa ngumu zaidi. Katika muktadha huo, adhabu na wajibu wa utoaji taarifa kisheria kwa wahudumu wa afya bado haujaainishwa kwa uwazi, hali inayoathiri mifumo ya uwajibikaji na kuzuia jitihada za kutokomeza kabisa ukeketaji.

**d) Mifumo ya elimu na afya ni majukwaa muhimu ya kuzuia na kutoa mwitikio kwa wakati**

Sekta za elimu na afya zina nafasi ya kimkakati katika kuzuia vitendo vya ukeketaji, kama zikitumiwa ipasavyo. Uingizwaji wa maudhui ya ukeketaji katika mitaala ya kitaifa na ujengeaji uwezo kwa walimu utawezesha kutambua au kukabiliana na hatari za ukeketaji. Vituo vya afya ni jukwaa muhimu la

upatikanaji wa huduma jumuishi, ikiwemo huduma za afya ya akili, rufaa za kisheria na huduma za matibabu, katika kipindi cha utekelezaji, takriban wanawake 78,000 waliobainika kuwa manusura wa ukeketaji walitambuliwa kupitia vituo vya afya. Hali hii inaonesha umuhimu wa kuimarisha mafunzo yanayohusu ukeketaji katika mitaala ya kada na mafunzo kazini kwa walimu na wahudumu wa afya. Majukwa haya ni fursa muhimu ya kuwafikia wanawake na watoto wa kike katika maeneo yote ya nchini.

**e) Kutokomeza vitendo vya ukeketaji kunapaswa kwenda sambamba na kushughulikia hali za kiuchumi, mila na desturi zinazochochea vitendo hivyo.**

Kuendelea kwa ukeketaji si kwa sababu za kimila pekee, bali ni matokeo ya ukosefu wa usawa wa kijinsia. Katika jamii ambayo watoto wa kike hutazamwa kama chanzo cha mahari au heshima ya familia, misukumo ya kijamii na kiuchumi ya kuendeleza ukeketaji hubaki kuwa imara. Mangariba wengi waliendelea kutegemea ukeketaji kama chanzo kikuu cha kipato. Afua zilizotumia mbinu za mabadiliko ya kijinsia, kuwashirikisha wanaume na wavulana na kuimarisha uwezo wa wanawake zilionyesha mafanikio makubwa zaidi katika kubadili mitazamo ya jamii. Hata hivyo, afua za uwezeshaji wa kiuchumi kwa waliokuwa mangariba zinapaswa kuongezeka. Kwa siku zijazo, mikakati ya kutokomeza ukeketaji inapaswa kuunganisha maeneo mahsusi ya ushiriki wa wanaume, kuingiza ajenda ya kutokomeza ukeketaji katika mipango ya usawa wa kijinsia na kujumuisha afua za kipato kwa familia na waliokuwa mangariba. Aidha, Ulinganifu wa sera za kitaifa ikiwemo Sera ya Uwezeshaji Kiuchumi na mipango ya hifadhi ya jamii utaongeza matokeo na kutoa motisha kwa mabadiliko endelevu.

**f) Uwekezaji wa muda mrefu ni muhimu katika huduma zinazozingatia manusura, mifumo ya takwimu na ujifunzaji.**

Huduma zinazomlenga manusura zilikuwa miongoni mwa mafanikio makubwa ya mkakati uliopita, hususan kupitia ongezeko la nyumba salama na Dawati za Polisi Jinsia na Watoto. Hata hivyo, msisitizo mkubwa uliwekwa katika huduma za mwitikio wa dharura, huku ufuatiliaji wa muda mrefu wa urejeshwaji kwenye jamii, huduma endelevu za msaada wa kisaikolojia na uwezeshaji wa kiuchumi ukiwa mdogo. Manusura wengi waliondoka katika mifumo ya ulinzi bila njia madhubuti za kurejea katika mfumo wa elimu au kupata ajira, hali iliyowaweka katika hatari ya unyanyapaa na madhara ya kisaikolojia ya muda mrefu.

Ukosefu wa mifumo imara ya kuandika na kuhifadhi kumbukumbu za afua, kufuatilia na kuchambua takwimu, pamoja na kutumia ujifunzaji unaobadilika ulipelekea ukosefu wa muendelezo wa utekelezaji na kushindwa kupanua utekelezaji wa afua za mfano zilizothibitika kuwa na mafanikio. Funzo kuu lililobainika ni haja ya kuasisi programu zinazomlenga kumsaidia manusura kurejea katika maisha ya kawaida kupitia mifumo ya muda wa kati na mrefu, pamoja na kuunganisha kikamilifu mifumo ya Ufuatiliaji, Tathmini na Ujifunzaji inayowezesha matumizi ya takwimu kwa wakati halisi na ujifunzaji wa pamoja. Utaratibu wa uhifadhi wa taarifa, majukwaa ya kidijitali ya usimamizi wa maarifa, pamoja na mikutano ya kila mwaka ya kujifunza na kubadilishana uzoefu, vinaweza kuchochea uboreshaji endelevu wa utekelezaji na kuwezesha udurufishaji wa mbinu bora zilizothibitishwa kufanya kazi katika mikoa mbalimbali ya nchi.

## 2.3 Tathmini ya Kisiasa, Kiuchumi, Kijamii, Kiteknolojia, Kimazingira na Kisheria

Vitendo vya ukeketaji bado ni tatizo kubwa hapa nchini vikiwaathiri wanawake na watoto wa kike, huku vikikiuka haki zao za msingi na uhuru wao wa kibinadamu. Dhamira ya Tanzania ya kutokomeza ukeketaji inaakisiwa kupitia makubaliano yake na mifumo ya kitaifa, kikanda na kimataifa, ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu, hususan Lengo la 5, linalolenga kufikiwa ifikapo mwaka 2030, pamoja na Ajenda ya Umoja wa Afrika 2063. Mkakati huu wa 2025/26 – 2029/30 umeandaliwa kwa kuzingatia hali ya mazingira ya sasa ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiteknolojia, kimazingira na kisheria.

**Mazingira ya Kisiasa**

Katika kudhamiria kuimarisha juhudi za kutokomeza vitendo vya ukeketaji, Serikali imekuwa mstari wa mbele katika kupitia, kuandaa, kushiriki na kutekeleza mikakati Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Serikali imesaini, kuridhia na kuoanisha sheria za nchi na nyenzo muhimu za Kikanda na Kimataifa kama vile Itifaki ya Maputo, Lengo la Maendeleo Endelevu namba 5.3 na Mpango wa Kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Kutokomeza Ukeketaji wa Kuvuka Mipaka. Juhudi hizi zinaonyesha utambuzi rasmi wa kutokomeza ukeketaji kama suala la maendeleo na haki za binadamu.

Katika ngazi ya Kitaifa, Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA Toleo la Pili 2024/25–2028/29) unatoa mfumo jumuishi wa jitihada za kutokomeza ukeketaji. Hata hivyo, dhamira ya kisiasa bado hutofautiana kati ya ngazi za kiutawala. Wakati viongozi wa ngazi ya Taifa huonyesha dhamira ya dhati, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinahitaji kuongeza juhudi katika upangaji na utengaji wa bajeti kwa ajili ya afua za kutokomeza vitendo vya ukeketaji. Aidha, juhudi za ziada zinahitajika katika mijadala ya Bunge na ujumuishwaji kwenye ajenda za vyama vya siasa ili kuwa na uendelevu wa sera na utetezi wa muda mrefu katika ngazi zote.

**Mazingira ya Kijamii na Kitamaduni**

Ukeketaji bado umejikita katika mifumo ya kijamii na kitamaduni ya baadhi ya jamii hapa nchini. Aidha, katika baadhi ya jamii, ukeketaji hutazamwa kama sehemu ya kuvusha rika, alama ya utambulisho wa kijamii na sharti la kijamii kwa ajili ya ndoa. Watoto wa kike wasiofanyiwa ukeketaji mara nyingi hukabiliwa na unyanyapaa, ubaguzi au kutengwa kijamii.

Licha ya kuongezeka kwa kampeni za uhamasishaji, mila na desturi zenye mfumo dume zinachochea vitendo vya ukeketaji katika familia nyingi. Katika maeneo yenye misimamo mikali ya kimila na ukimya kuhusu matukio ya ukeketaji huimarisha usiri na kurithisha desturi hii kizazi hadi kizazi. Hata hivyo, dalili za mabadiliko ya kijamii zinaanza kuonekana, hususan katika maeneo ambako viongozi wa jamii, waliokuwa ngariba walioacha kukeketa na vijana wameshirikishwa kikamilifu katika afua za mabadiliko.

**Mazingira ya Teknolojia**

Kuongezeka kwa matumizi ya simu za mkononi, redio na mtandao wa intaneti hapa nchini kunatoa fursa mpya za kuimarisha mikakati ya kutokomeza vitendo vya ukeketaji. Majukwaa ya kidijitali kama Huduma ya Simu ya bure kupitia namba 116 inawezesha utoaji wa taarifa za matukio na upatikanaji wa huduma za ushauri nasaha na rufaa. Serikali na Asasi za Kiraia zimeanza kutumia ujumbe mfupi wa maandishi, makundi ya WhatsApp na redio za jamii katika kueneza taarifa za kutokomeza mila na desturi zenye kuchochea vitendo vya ukeketaji katika kijamii.

Baadhi ya vituo vya afya vimeanza kuingiza viashiria vinavyohusiana na ukeketaji katika Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Huduma za Afya ili kusaidia ufuatiliaji wa kesi. Upatikanaji mdogo wa intaneti na uelewa mdogo wa matumizi ya teknolojia katika maeneo ya vijijini ambako vitendo vya ukeketaji hufanyika na kupunguza ufanisi wa afua za kutokomeza vitendo hivyo.

**Mazingira ya Kisheria**

Tanzania ina mifumo ya Kisera na Kisheria inayokataza vitendo vya ukeketaji. Sheria ya Mtoto Sura ya 13 inakataza vitendo vya ukeketaji na kutambua kama aina mojawapo ya ukatili dhidi ya watoto, ikiweka adhabu kuanzia kifungo cha miaka 15 hadi kifungo cha maisha kwa wahusika. Aidha, baadhi ya halmashauri zimepitisha kanuni ndogo za kuimarisha utekelezaji wa sheria za nchi.

Hata hivyo, utekelezaji bado ni changamoto kubwa kutokana na uelewa mdogo miongoni mwa jamii kuhusu sheria zilizopo . Nyaraka nyingi za kisheria zinapatikana kwa lugha ya Kiingereza pekee, hali inayozuia upatikanaji wake kwa wananchi wengi. Mapungufu pia yanaonekana katika kushughulikia

masuala yanayoibuka, kama vile vitendo vya ukeketaji unaofanywa katika baadhi ya mikoa, ambao bado haujawekewa adhabu mahsusi, pamoja na kufanyika kwa vitendo vya ukeketaji kwa wanawake watu wazima wanaokubali kwa hiari. Ukosefu wa mafunzo maalum kwa askari polisi, mahakimu na wahudumu wa afya pia hupunguza ufanisi wa mashtaka na huduma kwa manusura.

**Mazingira ya Kijiografia**

Upatikanaji wa huduma za kutokomeza ukeketaji, hususan maeneo ya vijijini hutegemea uwepo wa miundombinu rafiki na hali ya kijiografia. Miundombinu hii ni pamoja na nyumba salama zinazofanya kazi, barabara, usafiri wa uhakika, vituo vya afya na taasisi za utoaji haki zenye rasilimali watu wa kutosha. Katika misimu ya ukeketaji, ambayo mara nyingi huendana na likizo za shule, watoto wa kike hukabiliwa na hatari kubwa zaidi zakufanyiwa vitendo vya ukeketaji inayosababisha kutoroka nyumbani.

Hali ya mazingira kama vile uhamaji wa watu, ukame na matukio yanayohusiana na mabadiliko ya tabianchi huongeza hatari zaidi, hasa kwa jamii za wafugaji na wahamiaji. Hata hivyo, taasisi za kijamii kama shule na vituo vya afya zinaendelea kuwa lango muhimu la afua za kinga na ulinzi dhidi ya vitendo hivyo. Huduma mkoba za afya na utoaji haki, pamoja na mifumo ya kijamii kama Nyumba Kumi, zina fursa kubwa ambayo bado haijatumika kikamilifu katika kuimarisha ufikiaji wa huduma. Jedwali lifuatalo linaonyesha Uchambuzi wa Kisiasa, Kiuchumi, Kijamii, Kiteknolojia, Kisheria na Kimazingira kwa kuzingatia mahitaji na rasilimali za jamii

**Jedwali Na. 3: Uchambuzi wa Kisiasa, Kiuchumi, Kijamii, Kiteknolojia, Kisheria na Kimazingira kwa kuzingatia Mahitaji na Rasilimali za Jamii**

| ENEO HUSIKA | RASILIMALI ZA KIJAMII | MAHITAJI YA KIJAMII |
|---|---|---|
| Kisiasa | • Kuwepo kwa mifumo ya kisera na kisheria ya kitaifa inayokataza vitendo vya ukeketaji (mf. Kanuni ya Adhabu sura ya 16).<br>• Dhamira ya Serikali kupitia Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA).<br>• Kuwepo kwa madawati ya jinsia na watoto katika vituo vya polisi na kamati za ulinzi wa watoto katika ngazi ya wilaya.<br>• Dhamira ya kisiasa iliyoimarishwa kupitia uwepo wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii ambayo husimamia haki na ustawi wa mtoto. | • Kuimarishwa kwa dhamira ya kisiasa na utekelezaji katika ngazi za wilaya na kata.<br>• Uongozi unao onekana zaidi kutoka kwa wanaume vinara na viongozi wa kimila.<br>• Ulinganifu mkubwa wa mipango ya maendeleo ya mikoa na halmashauri na mikakati ya kitaifa ya kutokomeza ukeketaji.<br>• Kupitishwa kwa Sheria ya Mfano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu ukeketaji na kuandaliwa kwa muswada wa sheria wa kitaifa wa kutokomeza ukeketaji ili kuwasilishwa Bungeni. |
| Kiuchumi | • Kuwepo kwa vikundi vya wanawake vya kijamii, vikundi vya kuweka na kukopa na programu za uwezeshaji wa kiuchumi kwa vijana katika maeneo yanayofanya vitendo vya | • Uwezeshaji wa kiuchumi kwa watoto wa kike na wanawake vijana ili kupinga ndoa za utotoni zinazohusishwa na ukeketaji. |

| ENEO HUSIKA | RASILIMALI ZA KIJAMII | MAHITAJI YA KIJAMII |
|---|---|---|
| | ukeketaji (mf. Manyara, Mara, Dodoma, Arusha na Singida).<br>• Msaada wa asasi zisizo za kiserikali kwa upatikanaji wa njia mbadala za kipato kwa waliokuwa mangariba wa ukeketaji.<br>• Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290.<br>• Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2021 zinazowezesha mikopo isiyo na riba ya asilimia 10 kupitia mamlaka za serikali za mitaa. | • Ufadhili wa shughuli za uhamasishaji wa jamii katika ngazi ya chini.<br>• Bajeti mahsusi ya utekelezaji wa afua za ukeketaji katika ngazi ya taifa na serikali za mitaa.<br>• Njia mbadala za kuinua kipato na za kiuchumi kwa ngariba. |
| **Kijamii** | • Mitandao imara ya wanamabadiliko wa ndani, mashirika ya haki za wanawake na asasi za kijamii kama C-SEMA, NAFGEM na Children's Dignity Forum (CDF).<br>• Kuwepo kwa vinara wa mabadiliko chanya ya kijamii wakiwemo manusura na waliokuwa mangariba waliobadilika wanaopinga ukeketaji hadharani.<br>• Mikusanyiko ya kijamii na ibada (mf. mikutano ya vijiji, ibada za kanisa/msikiti) inayoweza kutumika kubadili mila nadesturi zenye madhara katika kijamii.<br>• Kuwepo kwa makundi muhimu ya kijamii kama viongozi wa kidini, watu wa kuaminika, makundi yenye ushawishi, watu mashuhuri, vijana na viongozi wa kimila.<br>• Kuwepo kwa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. | • Mila na tamaduni mbadala za kuvusha rika katika baadhi ya makabila (mf. Wakurya, Wamaasai, Wagogo).<br>• Hitaji la afua jumuishi za mabadiliko ya tabia zinazolenga wazazi, wazee na makundi rika.<br>• Kuimarishwa kwa vikundi vya msaada kwa manusura ya vitendo vya ukeketaji na watoto wa kike walio katika hatari.<br>• Kamati zilizoanzishwa kufanya kazi kikamilifu baada ya kuanzishwa.<br>• Ushirikishwaji wa wanaume. |

| ENEO HUSIKA | RASILIMALI ZA KIJAMII | MAHITAJI YA KIJAMII |
|---|---|---|
| Kiteknolojia | • Kuongezeka kwa matumizi ya simu za mkononi kwa uhamasishaji (mf. kampeni za jumbe fupi za maandishi, makundi ya WhatsApp).<br>• Kuwepo kwa Namba simu ya bure namba 116 kwa ajili ya utoaji wa taarifa na ushauri nasaha.<br>• Vyombo vya habari vya kijamii (redio za jamii, runinga za jamii) vinavyotumika tayari katika utetezi wa afya ya uzazi na jinsia.<br>• Upatikanaji wa Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Huduma za Afya wenye kipengele cha ukeketaji kinachowezesha ukusanyaji wa takwimu ngazi ya taifa. | • Uboreshaji wa upatikanaji wa intaneti na teknolojia za kidijitali katika maeneo ya vijijini yenye kufanya vitendo vya ukeketaji.<br>• Maudhui ya ndani zaidi kwa Kiswahili na lugha za makabila kwa kampeni za redio/televisheni/mtandaoni.<br>• Mifumo ya kidijitali ya utoaji taarifa na usimamizi wa kesi itumike kikamilifu.<br>• Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Huduma za Afya uunganishwe na sekta nyingine. |
| Kisheria | • Kifungu cha 158A cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, kinatoa adhabu kwa makosa yanayohusiana na ukeketaji, ikiwemo faini isiyopungua shilingi milioni mbili au kifungo cha miaka mitano hadi kumi na tano au vyote, pamoja na fidia kwa manusura.<br>• Kuwepo kwa sheria zinazokataza ukeketaji na matumizi yake kuongezeka (Kanuni ya Adhabu ilirekebishwa mwaka 1998).<br>• Vitengo vya Ulinzi wa Watoto katika vituo vya polisi.<br>• Kanuni ndogo za serikali za mitaa katika baadhi ya maeneo zinazosaidia utekelezaji. | • Utekelezaji madhubuti wa sheria za kutokomeza ukeketaji dhidi ya rushwa na shinikizo la mila na desturi katika jamii.<br>• Utoaji wa Elimu ya sheria miongoni mwa jamii na viongozi wa maeneo husika.<br>• Kuimarisha uratibu kati ya jeshi la polisi, maafisa ustawi wa jamii na Asasi za Kiraia kwa mwitikio wa haraka.<br>• Uwepo wa mifumo ya kisheria inayoshughulikia wanawake walio na umri wa zaidi ya miaka 18 wanaokubali kufanyiwa ukeketaji kwa hiari.<br>• Uelewa wa sheria katika jamii;<br>• Uwepo wa sheria katika lugha ya Kiswahili. |
| Kimazingira | • Nyumba salama na vituo vya uokoaji katika baadhi ya mikoa (mf. Kituo cha Masanga - Tarime).<br>• Shule na vituo vya afya vinavyotumika kama majukwaa ya uhamasishaji wa kutokomeza ukeketaji. Kama vile mabaraza ya | • Uwepo wa nyumba salama ikiwemo zinazomilikiwa na Serikali katika maeneo yenye ukeketaji, hususan wakati wa misimu ya ukeketaji.<br>• Miundombinu rafiki ya kusaidia rufaa na uokoaji katika maeneo ya vijijini na yaliyo mbali na miji. |

| ENEO HUSIKA | RASILIMALI ZA KIJAMII | MAHITAJI YA KIJAMII |
|---|---|---|
| | watoto na klabu za watoto zilizopo shuleni.<br>• Kuwepo kwa kona rafiki kwa vijana katika baadhi ya vituo vya afya. | • Watoto wa kike kuzifikia huduma rafiki kwa vijana kwa ukaribu. |

## 2.4 Uchambuzi wa Uwezo, Vikwazo, Fursa na Changamoto

**Uwezo**

Jitihada za Serikali za kutokomeza ukeketaji zimejengwa juu ya mifumo imara ya kisera, kisheria na kitaasisi. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 na Sera ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake Toleo la 2023. Kwa upande wa sheria, Serikali imepiga marufuku ukeketaji kupitia Sheria ya Mtoto Sura ya 13 na Kanuni za Adhabu Sura ya 16 na kuutambua ukeketaji kama aina ya ukatili dhidi ya Wanawake na watoto wa kike. Sera na Sheria hizi zinaimarishwa na mikakati ya kitaifa kama Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA Toleo la Pili 2024/25-2028/29), Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023-2033) na Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2020/21–2024/25, ambayo imeunganisha suala la ukeketaji ndani ya ajenda pana za ulinzi, jinsia na haki za binadamu. Jitihada za Serikali kwa kushirikana na Asasi za Kiraia kumechangia kuanzishwa na kuimarishwa kwa Madawati zaidi ya 420 ya Jinsia na Watoto la Polisi na nyumba salama takribani 18 zimeongeza upatikanaji wa huduma kwa manusura na mifumo ya ulinzi. Ushiriki wa Tanzania katika mifumo ya kikanda na kimataifa, ikiwemo mifumo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kutokomeza ukeketaji na Mpango wa Pamoja wa UNFPA-UNICEF, unaonesha dhamira ya kisiasa pamoja na upatikanaji wa msaada wa kitaalamu na kifedha.

**Vikwazo**

Licha ya uwezo ulioainishwa hapo juu, vikwazo kadhaa vimeendelea kuathiri ufanisi wa afua za awali za kutokomeza vitendo vya ukeketaji. Uboreshaji wa ushirikiano madhubuti wa kisekta unahitajika kati ya wizara za kisekta ili kuimarisha uratibu wa pamoja na kupunguza kujirudia kwa utekelezaji wa afua katika eneo moja. Hatua hii itasaidia uwajibikaji wa pamoja wa kimfumo. Baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa bado hazijajumuisha ipasavyo masuala ya ukeketaji katika mipango na bajeti zao, jambo lililoathiri wigo wa afua katika ngazi ya jamii. Ingawa sekta za kimkakati za afya na elimu zina nafasi muhimu katika kuzuia na mwitikio wa mapema, uwepo wa mada za ukeketaji katika mitaala na mafunzo ya vyuoni na kazini pia haukujitosheleza. Uboreshaji unahitajika katika kuboresha mitaala ya kitaifa, taasisi za elimu na uwepo wa mafunzo ya kutosha vyuoni na kazini. Ubora na ufanisi wa mifumo ya ukusanyaji na utunzaji wa takwimu za vitendo vya ukeketaji unahitaji kuimarishwa. Aidha, mifumo ya kijamii kama Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto na Familia za Kuaminika mara nyingi zinahitaji kuboreshwa ili zifanye kazi kikamilifu kwa kutoa mafunzo, kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali na ufuatiliaji endelevu.

**Fursa**

Kuongezeka kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia, ikiwemo matumizi ya simu za mkononi, mitandao na redio za kijamii kumechangia gharama nafuu za uhamasishaji, utoaji wa taarifa za matukio kwa wakati na upatikanaji wa mrejesho wa jamii kuhusiana na ukeketaji. Kuongezeka kwa mitandao ya vijana na wanawake kunatoa majukwaa ya kuhamasisha manusura, vijana na wanaume vinara wa mabadiliko chanya kupinga mila na desturi zenye madhara katika kubadili mitazamo ya jamii.

Mifumo ya kikanda kama Mpango wa Kikanda unaoonyesha Gharama za Kutokomeza Ukeketaji wa Kuvuka Mipaka na ahadi za kisiasa chini ya kampeni ya Umoja wa Afrika ya Kutokomeza Kabisa vitendo vya ukeketaji ("*Getting to Zero*") zinatoa fursa za kuimarisha ushirikiano wa mipakani katika utekelezaji wa pamoja wa sheria na kubadilishana uzoefu. Kanuni za Serikali za Mitaa kuhusu Mfuko wa Maendeleo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu unatoa fursa za kiuchumi kwa waliokuwa ngariba na vijana wa kike walio katika hatari za kukeketwa. Aidha, kuna ulinganifu unaoongezeka kati ya jitihada za kutokomeza ukeketaji na ajenda za maendeleo, kama usawa wa kijinsia, elimu kwa watoto wa kike na afya ya uzazi, hali inayowezesha ujumuishaji wa afua na uratibu wa rasilimali kati ya sekta mbalimbali.

**Changamoto**

Uendelevu na matokeo ya afua za kutokomeza ukeketaji nchini Tanzania unaweza kuathiriwa na upinzani wa kimila katika jamii zenye viwango vya juu vya ukeketaji. Aidha, mila ya ukeketaji inatafsiriwa kama utambulisho wa jamii, kupata ndoa na hadhi ya kifamilia. Shinikizo kutoka kwa kundi rika na wazee wa kimila linaendelea kuimarisha utii wa tamaduni hizi, hususan miongoni mwa watoto wa kike walio katika rika balehe.

Kuongezeka kwa ukeketaji unaofanywa kwa siri ni tishio linaloongezeka, hasa katika mazingira ambayo hakuna adhabu mahususi au hatua za kinidhamu katika jamii. Ukeketaji wa kuvuka mipaka pia ni changamoto kubwa, ambapo familia katika maeneo ya mpakani huwapeleka watoto wa kike katika nchi jirani kama vile Kenya na Uganda ili kukwepa sheria za Tanzania. Kukosekana kwa uhakika wa upatikanaji wa rasilimali fedha kutokana na utegemezi mkubwa wa wadau wa maendeleo na mgao mdogo wa bajeti za ndani kunaweza kusababisha kudorora kwa mafanikio yaliyopatikana na jitihada zilizofanyika. Mabadiliko ya kisiasa, mwelekeo mpya wa sera au vipaumbele vingine vya kitaifa vinaweza pia kupunguza umakini kwa suala la vitendo vya ukeketaji. Ushiriki mdogo wa wanaume na uelewa mdogo wa sheria miongoni mwa jamii unaendelea kuwa changamoto kwa juhudi za kutokomeza ukeketaji.

**Jedwali Na. 4: Uchambuzi wa Uwezo, Vikwazo, Fursa na Changamoto**

| Uwezo | Fursa |
|---|---|
| i. Kuwepo kwa sera, sheria, mipango na miongozo inayoshughulikia ukeketaji<br>ii. Kuwepo kwa watumishi wenye ujuzi na uwezo<br>iii. Utayari wa kisiasa katika kutokomeza vitendo vya ukeketaji<br>iv. Kuwepo kwa Kikundi Kazi cha Wataalamu ngazi ya Taifa cha kuratibu masuala ya kutokomeza ukeketaji<br>v. Kuwepo kanuni ya adhabu sura ya 16, kifungu cha 169A<br>vi. Sheria ya mtoto sura ya 13, kifungu cha 160 | i. Kuwepo kwa itifaki, mikataba na mifumo ya kisheria ya kikanda na kimataifa inayokataza ukeketaji<br>ii. Utayari wa ushirikishwaji wa jamii<br>iii. Uwepo wa Wadau wa Maendeleo wenye utayari wa kuunga mkono juhudi za kutokomeza ukeketaji<br>iv. Upatikanaji wa rasilimalifedha katika ngazi ya kimataifa<br>v. Kuongezeka kwa matumizi ya mitandao ya kijamii kuelimisha masuala ya kutokomeza ukeketaji<br>vi. Muungano na utayari wa Asasi za Kiraia |

| Vikwazo | Changamoto |
|---|---|
| i. Sera zilizopitwa na wakati, mfano sera ya Maendeleo ya Mtoto (haijafanyiwa mapitio kwa zaidi ya miaka 15)<br>ii. Utekelezaji hafifu wa sheria zilizopo<br>iii. Mifumo isiyo madhubuti ya kielektroniki ya takwimu za ukeketaji<br>iv. Ufuatiliaji na tathmini usioridhisha<br>v. Ukeketaji kutopatiwa kipaumbele katika Mpango na Bajeti katika wizara, mamlaka za serikali za mitaa na miongoni mwa wadau wa maendeleo<br>vi. Baadhi ya miongozo kutotafsiriwa kwa Kiswahili na kutosambazwa ipasavyo | i. Uwepo wa mila na desturi zinazounga mkono ukeketaji<br>ii. Vitendo vya ukeketaji vinavyofanyika kwa siri<br>iii. Matumizi yasiyo sahihi ya mila mbadala ya kuvusha rika<br>iv. Kukosekana kwa usawa wa kijinsia na kuendelea kwa desturi za mfumo dume<br>v. Ufadhili mdogo wa ndani na wa nje<br>vi. Uelewa mdogo kuhusu madhara ya ukeketaji miongoni mwa wanajamii |

## 2.5 Uchambuzi wa Wadau

Kutokomeza ukeketaji nchini Tanzania ni changamoto inayohitaji ushiriki hai na uratibu wa juhudi kutoka kwa wadau mbalimbali. Wadau hawa ni pamoja na taasisi za Serikali, mashirika ya kimataifa na jamii za maeneo husika. Wadau hawa, wana viwango tofauti vya maamuzi, ushawishi na uwezo, huku kila kundi likichangia kwa namna yake katika utekelezaji wa afua za kutokomeza vitendo vya ukeketaji. Uelewa wa kina wa majukumu yao, maslahi na uwezo wao ni muhimu katika kuandaa na kutekeleza mkakati wa kitaifa ulio thabiti, jumuishi na wenye ufanisi.

**a) Wizara, Idara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, Idara, Taasisi za Serikali na Serikali za Mitaa zinasimamia na kuratibu wadau wa kutokomeza ukeketaji nchini. Aidha, jukumu la msingi la Wizara, Idara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa ni pamoja na uandaaji wa sera, mikakati, miongozo, utekelezaji wa sheria na ujumuishaji wa masuala ya kutokomeza ukeketaji katika programu za kitaifa. Vilevile, zina wajibu wa kuweka kipaumbele kwa masuala ya ukeketaji katika upangaji wa bajeti pamoja na utekelezaji katika ngazi za chini.

**b) Wadau wa Maendeleo na Mashirika ya Kimataifa**

Wadau wa maendeleo na mashirika ya kimataifa kama UNFPA, UNICEF, UN Women, WHO na Umoja wa Ulaya (EU) ni kati ya wadau muhimu katika juhudi za kutokomeza vitendo vya ukeketaji nchini Tanzania. Wadau hawa huchangia rasilimali za kifedha, utaalamu wa kiufundi na msaada wa utekelezaji wa programu za kukabiliana na vitendo vya ukeketaji nchini. Mchango wao unaonekana katika kuongeza afua za kutokomeza vitendo vya ukeketaji, kujenga uwezo na upatikanaji wa takwimu muhimu kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini.

**c) Asasi za Kiraia na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

Asasi za kiraia, mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika ya kidini ni mhimili wa utekelezaji wa afua katika ngazi ya jamii. Ushirikiano wa asasi kama LHRC, C-Sema, DSW, CDF, ATFGM, Hope for Women and Girls, NAFGEM, CCT, ESTL, ELCT, HIMD, Sauti ya jamii kipunguni na wengineo wanachangia kutekeleza afua za moja kwa moja katika jamii. Ushawishi wao unatokana na ukaribu wao kwa jamii unaowawezesha kuaminika na kuwa na nafasi ya kutekeleza afua zinazozingatia muktadha wa kitamaduni, kuendesha kampeni na kuhamasisha mila mbadala za kuvusha rika. Wadau hawa

wanachangia katika kuleta mabadiliko ya mwenendo wa jamii, maboresho ya sera na kutoa msaada kwa manusura.

**d) Jamii wakiwemo watoto wa kike**

Jamii za maeneo husika wakiwemo watoto wa kike na wanawake ni walengwa wakuu na wana nafasi kubwa ya kuwa chachu ya mabadiliko. Viongozi wa kijamii wana nafasi kubwa kutokana na ushawishi wao wa kupinga mila na desturi zenye madhara. Ushiriki wao ni muhimu katika kuimarisha afua zinazoongozwa na jamii za kuzuia, kutoa taarifa na kukabiliana na vitendo vya ukeketaji.

**e) Wasimamizi na Watekelezaji wa Sheria**

Vyombo vya usimamizi wa sheria ni muhimu katika kutekeleza sheria za kutokomeza ukeketaji. Mamlaka yao ya kuchunguza, kukamata na kufikisha wahusika kwenye vyombo vya sheria huwapa nafasi muhimu katika kuimarisha ulinzi wa kisheria. Mchango wao utaimarishwa zaidi kwa uwepo wa kipaumbele cha kutosha kwa kesi za ukeketaji, hali inayoweza kuimarisha idadi ya kesi zinazofikia hatua ya mashtaka na hukumu.

**f) Manusura wa ukeketaji na vijana vinara**

Manusura wa ukeketaji na makundi yanayoongozwa na vijana vinara, ni wadau muhimu wa mabadiliko. Ushuhuda wa manusura umeonesha kuwa na nguvu kubwa katika kubadili mitazamo ya jamii. Vijana vinara wa mabadiliko wakiwemo wa kike na wa kiume hutumia majukwaa ya kidijitali, makundi rika, vilabu vilivyopo ndani ya shule vya kupinga ukeketaji na kutetea usawa wa kijinsia. Uimarishaji wa huduma endelevu za manusura ni muhimu hasa huduma za kisaikolojia, uwezeshaji wa kiuchumi na maeneo salama ya uponyaji na usaidizi. Kuwekeza katika utetezi wa manusura na vijana kupitia mafunzo, huduma na majukwaa kutaimarisha sauti zao na kujenga harakati jumuishi za kizazi hadi kizazi na hasa iwapo unyanyapaa utadhibitiwa na uwepo wa rasilimali ukiimarika.

**g) Wazee wa kimila, wazee wa koo na mamlaka za kidini**

Viongozi wa kimila, wazee wa koo na viongozi wa kidini wana ushawishi mkubwa juu ya mila na desturi zinazoendeleza ukeketaji. Katika jamii, viongozi hawa hutazamwa kama walinzi wa utamaduni na walinzi wa uhalali wa kijamii. Baadhi yao wamekuwa washirika muhimu katika mapambano dhidi ya vitendo vya ukeketaji, huku wengine wakibaki na upinzani au ukimya. Nguvu yao ya kijamii inaweza kuharakisha au kuzuia mabadiliko ya kitabia. Ushirikishwaji wao wa kimkakati kupitia majadiliano yenye heshima ya kitamaduni, ujenzi wa uwezo na ushawishi wa rika ni muhimu. Ushiriki wao katika kuunga mkono mila mbadala za vusha rika na matamko ya hadhara ya kuachana na ukeketaji umeonesha mafanikio katika maeneo kama Singida na Manyara na hivyo kuwafanya kuwa wadau wenye ushawishi mkubwa katika mkakati wowote jumuishi.

**h) Ngariba, wazazi na walezi**

Wazazi na walezi katika mikoa yenye viwango vya juu vya ukeketaji, wana maamuzi ya mwisho iwapo mtoto wa kike afanyiwe ukeketaji au la. Programu za malezi chanya zinalenga kuwawezesha kuwa na ujuzi wa kujenga mazingira salama na yenye msaada ndani ya familia. Mangariba na wakunga wa jadi, ambao awali walikuwa wahamasishaji wa mila hii, sasa wanachukuliwa kama wadau wenye uwezekano mkubwa wa kuwa vinara wa mabadiliko. Kuwapatia njia mbadala na endelevu za kiuchumi kupitia afua za uzalishaji wa kipato kunawawezesha kuachana kabisa na mila hii na kuwa watetezi wa kuutokomeza ukeketaji.

**Jedwali Na. 5: Uchambuzi wa Wadau**

| Wadau | Uwezo | Ushawishi | Athari |
|---|---|---|---|
| **Wizara, Idara, Taasisi na MSM** | Wana mamlaka ya kisheria, uwezo wa kiutawala, rasilimali | Uundaji wa sera, utekelezaji wa sheria, uwekaji wa vipaumbele vya kitaifa | Huweka mazingira wezeshi, mazingira wezeshi ya kisheria na hutenga bajeti |
| **Wadau wa maendeleo** | Uchangiaji wa rasilimali fedha, utaalamu wa kiufundi na kiunganishi kwenye majukwaa ya kimataifa | Kushawishi vipaumbele vya kitaifa, hutoa msaada wa kiufundi na kujenga uwezo | Huongeza wigo wa programu, kukuza mbinu bora, huchangia kuzalisha takwimu |
| **Asasi za Kiraia na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali** | Uhamasishaji wa jamii, utetezi, utoaji wa huduma za moja kwa moja | Hujenga uaminifu katika ngazi ya jamii, hutetea mabadiliko ya sera | Huhamasisha mabadiliko ya kitabia, hutoa huduma kwa manusura, hutekeleza afua kama mila mbadala za kuvusha rika |
| **Wanajamii ikiwemo Viongozi wa Kimila/Dini na Mashirika ya Kidini** | Kuendeleza au kupinga desturi, ushawishi wa kijamii katika maamuzi ya eneo | Huathiri moja kwa moja kuendelea au kuachwa kwa ukeketaji, huunda mitazamo ya jamii | Huamua uendelevu wa mabadiliko, ni muhimu kwa mifumo ya utoaji taarifa na mwitikio |
| **Vyombo vya utekelezaji wa Sheria** | Uchunguzi, ukamataji, uendeshaji wa mashtaka | Kuzuia kupitia hatua za kisheria, utoaji wa haki kwa manusura | Usimamizi wa mashtaka na hukumu kwa ngariba na washiriki wa ukeketaji |
| **Wazazi na Walezi** | Maamuzi kuhusu watoto wa kike na familia | Wanaweza kuzuia au kuendeleza ukeketaji ndani ya familia | Hufanya maamuzi kuhusiana na mtoto wa kike kufanyiwa au kutofanyiwa ukeketaji |
| **Mangariba na Wakunga wa Jadi** | Wanaendeleza mila na desturi, hadhi ya kijamii | Wanaweza kushawishi kuendelea au kuachwa kwa ukeketaji | Hushawishi uhitaji au wanaweza kubadilika na kuwa vinara wa kutokomeza ukeketaji |

## 2.6 Maendeleo na Mueleko

Uandaaji wa Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30 umechochewa kwa kiasi kikubwa na mafanikio yaliyojitokeza katika kipindi cha utekelezaji wa mkakati uliotangulia. Katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, Tanzania imeshuhudia kupungua kwa kiwango cha kitaifa cha ukeketaji, hususan miongoni mwa makundi ya watoto wa kike na wanawake, hali inayoashiria mabadiliko ya taratibu lakini yenye maana katika mitazamo na mienendo ya kijamii. Kwa mujibu wa Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa mwaka 2022, kiwango cha ukeketaji miongoni mwa wanawake wenye umri wa miaka 15-49 kilipungua hadi kufikia asilimia 8, kutoka asilimia 10 mwaka 2015/16. Upungufu huu unaonekana zaidi katika baadhi ya maeneo yenye kiwango kikubwa cha tatizo, ukionesha mchango wa uhamasishaji endelevu wa jamii, utekelezaji wa sheria na ongezeko la upatikanaji wa huduma za ulinzi.

Kiwango cha vijana hasa wale walio na elimu ya sekondari au ya juu, kinaonesha ongezeko la kupinga mila na desturi za ukeketaji, vikisaidiwa na kuongezeka kwa afua zinazoongozwa na makundi rika na vijana vinara. Hata hivyo, mafanikio haya ya jumla hayaakisi hali halisi katika baadhi ya Mikoa nchini. Aidha, baadhi ya jamii bado zina viwango vya juu zaidi vya ukeketaji juu ya wastani wa Kitaifa. Hata hivyo, maeneo ya vijijini yanaendelea kuwa nyuma ukilinganisha na mijini katika upatikanaji wa taarifa na huduma. Sambamba na hilo, mienendo mipya na muingiliano wa kijamii unaendelea kuongeza mazingira mapya ya ukeketaji katika mikoa ambayo awali, takwimu hazikuonyesha uwepo wa ukeketaji. Vilevile, kuongezeka kwa ukeketaji wa kitabibu, ambapo baadhi ya wahudumu wa afya hasa katika mazingira ya binafsi au yasiyo rasmi hufanya ukeketaji kwa madai ya kupunguza madhara. Kitendo hiki kinakiuka maadili ya taaluma ya afya na sheria za kitaifa na kwa kufanya hivyo, kuna sababisha kufanya utambuzi na uchunguzi wa kisheria kuwa mgumu zaidi.

Vilevile, ukeketaji wa kuvuka mipaka unaendelea kuwa tishio linaloongezeka, hususan katika maeneo yanayopakana na Kenya na Uganda. Familia katika maeneo haya huwasafirisha watoto wa kike kuvuka mipaka ya kitaifa ili kukwepa adhabu za kisheria nchini Tanzania, hali inayodhoofisha mafanikio ya ndani ya utekelezaji wa sheria. Kuongezeka kwa uhamaji wa watu, mipaka iliyo wazi na udhaifu wa mifumo ya ushirikiano wa kikanda kumezidisha changamoto hii. Maendeleo haya yanahitaji juhudi mpya katika maboresho ya kisheria, uwajibikaji wa kitaaluma katika sekta ya afya na kuimarishwa kwa mifumo ya ufuatiliaji wa mipakani.

Wakati huo, fursa za kuharakisha mafanikio zinaendelea kuongezeka kupitia mabadiliko ya kiteknolojia, kisera na kidemografia. Kuongezeka kwa upatikanaji wa simu za mkononi, redio na mitandao ya kijamii kumeimarisha ufikiaji wa ujumbe, uhamasishaji na utoaji wa taarifa ya matukio ya ukeketaji, hususani miongoni mwa vijana katika maeneo ya mijini. Matumizi ya mifumo ya kidijitali ya usimamizi wa kesi na ujumuishaji wa viashiria vya ukeketaji katika mifumo ya kitaifa ya afya na ulinzi vimeanza kuziba pengo la takwimu.

Katika ngazi ya sera, ulinganifu wa Tanzania na mifumo ya kikanda kama Mpango wa Kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wa Kutokomeza Ukeketaji wa Kuvuka Mipaka, pamoja na ajenda za kimataifa ikiwemo kampeni ya Umoja wa Afrika ya "*Getting to Zero FGM*" na Lengo la 5.3 la Malengo ya Maendeleo Endelevu, unatoa mwelekeo wa kimkakati na fursa za uhamasishaji wa rasilimali. Aidha, kuna ongezeko la uungwaji mkono wa kisiasa na wa ngazi ya jamii kwa huduma zinazomlenga manusura na mbadala zinazozingatia muktadha wa kitamaduni, ikiwemo Mila mbadala za kuvusha rika.

Kwa ujumla, mwelekeo na maendeleo haya yanasisitiza hitaji la mwitikio wa kimkakati wa mabadiliko na kujifunza kwa wakati katika kipindi cha utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30.

## 2.7 Mambo Muhimu ya Kuhakikisha Mafanikio ya Mkakati wa Mwaka 2025/26–2029/30

Mafanikio ya Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30 yatategemea kwa kiasi kikubwa kuendelea kuwepo kwa dhamira thabiti ya kisiasa na uongozi endelevu katika ngazi zote za Serikali, kuanzia ngazi ya kitaifa hadi Mamlaka za Serikali za Mitaa. Dhamira hii inapaswa kuonekana kwa vitendo kwakuipa kipaumbele agenda ya kutokomeza ukeketaji katika mipango ya maendeleo ya taifa, kutenga rasilimali za kutosha na kuimarisha uungwaji mkono wa mara kwa mara kwa vyombo vya usimamizi na utekelezaji wa Sheria. Vinara wa kisiasa wana nafasi muhimu katika kuendeleza ajenda ya kutokomeza ukeketaji, kuhakikisha suala hili linaendelea kuwa kipaumbele cha sera na kujenga mazingira wezeshi ya utekelezaji wa afua. Bila uungwaji mkono madhubuti na endelevu wa kisiasa, jitihada za utekelezaji zinaweza kugawanyika, kukosa rasilimali na kushindwa kushughulikia kwa ufanisi mila na desturi zinazochochea vitendo vya ukeketaji katika jamii.

### 2.7.1 Mifumo Imara ya Kisera na Kisheria

Mojawapo ya nguzo kuu za mafanikio ya mkakati huu ni uwepo na uimarishaji endelevu wa mifumo imara ya Kisheria na kisera. Tanzania tayari ina mifumo ya kisheria kama vile Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 na Sheria ya Mtoto Sura ya 13, inayokataza ukeketaji na kulinda watoto wa kike dhidi ya vitendo vyenye madhara. Hata hivyo, ufanisi wa mifumo hii unategemea utekelezaji wake thabiti na usio na upendeleo. Uwezo wa vyombo vya usimamizi na utekelezaji wa sheria ikiwemo Polisi, Mahakama na Idara za Ustawi wa jamii unapaswa kuendelea kuimarishwa katika kuchunguza, kushtaki na kutoa maamuzi kuhusu kesi za ukeketaji. Changamoto kama vile rushwa, uelewa mdogo wa jamii kuhusu sheria na ugumu wa kupata ushahidi wa kuaminika zinapaswa kushughulikiwa. Mifumo ya uwajibikaji ikiwemo ufuatiliaji wa mashitaka na hukumu pamoja na kuimarisha Dawati la Jinsia na Watoto katika vituo vyote vya Polisi ni muhimu katika kuhakikisha haki kwa manusura na kuzuia vitendo vya ukeketaji.

Mkakati huu unaendeleza jitihada za kutetea maboresho ya kisheria ili kuziba mianya iliyopo, ikiwemo ukosefu wa adhabu mahsusi dhidi ya ukeketaji wa kitabibu na kuhakikisha ulinzi wa wanawake waliovuka umri wa utoto. Aidha, mkakati unalenga kuoanisha sera za kitaifa na mifumo ya kikanda kama sera za kijinsia za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na ahadi za kimataifa, hususan Lengo la 5.3 la Malengo ya Maendeleo Endelevu. Kupitia kuimarisha utekelezaji wa sheria, kuongeza uelewa wa kisheria kwa umma na kuboresha mwitikio wa vyombo vya haki, mkakati huu utaimarisha mazingira ya kisheria yanayozuia ukeketaji na kulinda haki na utu wa manusura.

### 2.7.2 Ushirikishwaji wa Jamii

Kutokomeza ukeketaji kwa njia endelevu kunahitaji mabadiliko ya kina katika imani, mitazamo na mienendo ya jamii. Ushirikii ni jambo la msingi, ikizingatiwa kuwa ukeketaji unaendelezwa zaidi na kanuni za kijamii na mila zilizozoeleka. Mkakati huu unapaswa kuachana na utaratibu wa utekelezaji kuanzia juu Kwenda chini na badala yake kuwezesha jamii kubaini suluhisho zao wenyewe na kuongoza mabadiliko kutoka ndani. Ushirikishwaji wa viongozi wa kimila na kidini ni muhimu kwa kuwa wana ushawishi mkubwa katika jamii na wanaweza kuwa mabalozi wa kutokomeza ukeketaji. Ushiriki wa wazee, vijana na viongozi wa jamii katika usanifu na utekelezaji wa afua ni nguzo muhimu ya mafanikio. Afua zinazotegemea tafiti kama mila mbadala za kuvusha rika, vikundi vya malezi chanya, mifano ya mienendo chanya na majadiliano ya kijamii zimeonesha uwezo wa kubadilisha mazoea ya kijamii. Mifumo ya kuzuia na mwitikio inayoongozwa na jamii, ikiwemo ufuatiliaji na mifumo ya ulinzi wa ngazi ya jamii, ni muhimu katika kujenga mabadiliko endelevu na yanayoheshimu muktadha wa kitamaduni. Mikoa kama Singida na Mara imeonesha mafanikio ya kupungua kwa ukeketaji kupitia uhamasishaji wa vinara wa kijamii na afua za majadiliano ya kijamii.

### 2.7.3 Ushirikiano wa Kisekta Ulio Imara:

Kutokomeza ukeketaji kunahitaji hatua zilizoratibiwa kati ya sekta na ngazi mbalimbali za utawala. Sekta za Afya, Elimu, Ustawi wa Jamii, Utekelezaji wa Sheria na Ulinzi wa Mtoto zinapaswa kufanya kazi kwa ushirikiano. Mkakati huu unatoa kipaumbele katika kuimarisha Kikosi Kazi cha Taifa cha Kutokomeza Ukeketaji, chenye majukumu yaliyoainishwa wazi kwa kila wizara, idara na taasisi katika kusimamia utekelezaji, ufuatiliaji na uwajibikaji. Katika ngazi za mikoa na almashauri, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaongoza afua zinazolingana na mazingira husika kupitia Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto. Zana muhimu kama mipango ya pamoja, mifumo ya kubadilishana takwimu na taratibu za rufaa za sekta mtambuka zitasaidia utoaji wa huduma jumuishi. Miundo madhubuti ya uratibu, ikiwemo Vikundi Kazi vya Kitaalamu na mifumo ya pamoja ya utoaji taarifa, itapunguza kujirudia kwa shughuli, kuboresha matumizi ya rasilimali na kuhakikisha afua zinatekelezwa kwa ufanisi.

### 2.7.4 Maamuzi Yanayotegemea Tafiti na Uwajibikaji

Upangaji wa afua unaotegemea tafiti ni msingi wa kufanya maamuzi sahihi ya kimkakati, kutenga rasilimali na kurekebisha afua kwa wakati. Mkakati unasisitiza matumizi ya takwimu zilizoainishwa kwa umri, eneo na aina ya ukeketaji ili kuelewa mienendo na kupima matokeo. Unapendekeza kuanzishwa

kwa dashibodi ya kitaifa ya takwimu za ukeketaji inayounganishwa na mifumo kama Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Huduma za Afya, Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto na kumbukumbu za Mahakama. Aidha, utaimarisha mifumo ya ukusanyaji wa takwimu za mara kwa mara kupitia mifumo ya afya na tafiti za kitaifa kama TDHS. Ufuatiliaji wa kesi kwa wakati na utoaji taarifa kwa kijamii utasaidia mwitikio lengwa. Zana za ufuatiliaji kama kadi za uwajibikaji kwa umma na tathmini ya kipindi cha kati zitaimarisha uwazi na kusaidia marekebisho ya sera na afua. Utafiti kuhusu aina mpya au ukeketaji wa kificho utakuwa muhimu katika kukabiliana na mienendo inayobadilika.

### 2.7.5 Huduma Jumuishi Zinazomlenga Manusura

Huduma jumuishi kwa manusura wa ukeketaji ni nguzo kuu ya mkakati huu. Hii inajumuisha ongezeko la nyumba salama, ongezeko la huduma za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia, kuimarisha mifumo ya rufaa kupitia vituo vya huduma za pamoja na kuongeza huduma ya upasuaji wa kurekebisha madhara. Taratibu zilizo wazi, wataalamu waliopata mafunzo na utengaji bajeti ya kutosha ni muhimu ili kuhakikisha ubora na uendelevu wa huduma hizi.

### 2.7.6 Ushirikishwaji wa Watoto wa Kike, wa Kiume, Wanawake na Wanaume

Kuwawezesha watoto wa kike na wanawake vijana kama vinara wa mabadiliko ni jambo la msingi. Hii inahusisha kuwajengea uwezo wa kutambua haki zao, kuwaelimisha kuhusu madhara ya ukeketaji na kuwaimarisha katika kufanya maamuzi sahihi kupitia mafunzo ya stadi za maisha na vilabu vya vijana. Afua zinazoongozwa na vijana kama elimu rika, kampeni za mitandao ya kijamii, mijadala ya shuleni na utetezi wa kijamii zina uwezo mkubwa wa kuharakisha mabadiliko ya kanuni za kijamii. Sambamba na hilo, watoto wa kiume na wanaume wanapaswa kushirikishwa kama vinara wa mabadiliko. Afua mahsusi kama majadiliano ya wanaume, warsha kwa viongozi wa kidini na kimila na programu za kuwajengea uwezo wanaume vinara wa mabadiliko zinaweza kubadilisha mitazamo na kuongeza uwajibikaji. Msaada wao katika mila mbadala za kuvusha rika na afua nyingine za kinga utachangia kujenga mazingira salama na yenye usawa kwa wote.

### 2.7.7 Kukabiliana na Ukeketaji wa Kuvuka Mipaka

Mojawapo ya kikwazo kikubwa katika kutokomeza vitendo vya ukeketaji hapa nchini ni kuendelea kwa ukeketaji wa kuvuka mipaka na aina zilizofichwa, ambazo vinadhoofisha utekelezaji wa sheria za kitaifa. Katika maeneo ya mipakani kama Tarime (Mkoa wa Mara) na Longido (Mkoa wa Arusha), familia husafirisha watoto wa kike kwenda nchi jirani kama Kenya na Uganda ili kukwepa sheria za Tanzania. Changamoto hii inazidishwa na tofauti za adhabu kati ya nchi. Nchini Tanzania, adhabu kwa kosa la ukeketaji zinaweza kufikia kifungo cha maisha, ilhali katika nchi jirani za Kenya na Uganda hutumika adhabu nyepesi zaidi. Tofauti hii ya kisheria hujenga mianya ya kisheria inayotumiwa na wahusika kukwepa uwajibikaji wa sheria. Kwa mfano, mwaka 2020 katika Wilaya ya Tarime, zaidi ya wasichana 50 walivushwa mipaka kupelekwa nchini Kenya wakati wa likizo za shule kwa ajili ya kufanyiwa ukeketaji na tukio hilo liligunduliwa na kuzuiwa baada ya tahadhari kutoka kwa jamii. Ili kushughulikia kwa ufanisi changamoto hizi, mkakati huu unatumia Mpango wa Kikanda wa Utekelezaji ulioainisha gharama za utekelezaji wa Kutokomeza Ukeketaji wa Kuvuka Mipaka. Mpango huo unaweka kipaumbele katika uundaji wa vikosi kazi vya pamoja vya kuvuka mipaka, uendanishaji wa mifumo ya kisheria, pamoja na makubaliano ya pande mbili za nchi ili kuwezesha urejeshaji wa watuhumiwa na ubadilishanaji wa taarifa baina ya nchi husika.

### 2.7.8 Kukabiliana na Ukeketaji wa Kificho

Ukeketaji wa kificho ni tishio linaloongezeka kutokana na mbinu zake za siri. Kadri uelewa na udhibiti wa kisheria unavyoongezeka, wahusika wanabadilisha mbinu kwa kuficha ukeketaji kama huduma za kawaida za afya au sherehe za kimila. Katika baadhi ya matukio, ukeketaji wa kitabibu hufanywa na wahudumu wa afya katika kliniki binafsi au majumbani, kinyume na maadili ya kitaaluma. Msimu wa likizo za shule (Juni na Desemba) umeonesha ongezeko la matukio katika mikoa yenye viwango vya

juu kama Manyara, Dodoma na Singida. Mkakati huu unajibu changamoto hii kwa kujenga mifumo ya tahadhari ya mapema kupitia walimu, maafisa ustawi wa jamii na walezi rika waliopata mafunzo ya kutambua vihatarishi na kutoa taarifa za matukio yanayoshukiwa. Mifumo ya ufuatiliaji wa kijamii, ikiwemo Mfumo wa Kaya Tano, itawekwa na kuimarishwa ili kufuatilia mienendo ya eneo husika na kusaidia utoaji taarifa na rufaa. Hatua hizi zitaambatana na kampeni za uhamasishaji wakati wa misimu ya hatari ili kuzuia matukio yaliyopangwa ya ukeketaji.

## 2.8 Vipimo Muhimu vya Mafanikio ya Mkakati

### 2.8.1 Ufuatiliaji na tathmini ya ufanisi wa mkakati

| | |
|---|---|
| **01** | **1. Kupungua kwa Kiwango cha Ukeketaji katika Mikoa Yenye Hatari Kubwa** |
| **02** | **2. Ongezeko la Jamii Zinazotangaza Hadharani Kuacha Ukeketaji** |
| **03** | **3. Kuimarika kwa Upatikanaji na Matumizi ya Huduma Zinazozingatia mahitaji ya Manusura** |
| **04** | **4. Kuimarika kwa Usimamizi wa Sheria, Ufunguaji wa Mashitaka na Hukumu katika Kesi za Ukeketaji** |
| **05** | **5. Uwepo wa mifumo yenye ufanisi ya ufuatiliaji wa vitendo vya ukeketaji wa kuvuka mipaka** |
| **06** | **6. Uingizaji wa Afua za Kupambana na Ukeketaji katika Mipango ya Sekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa** |
| **07** | **7. Utekelezaji Madhubuti wa Mifumo ya Ulinzi Mashuleni** |
| **08** | **8. Ufikiwaji na Matokeo ya Kampeni za Mawasiliano na Elimu kwa Umma** |
| **09** | **9. Uwezeshaji wa Kiuchumi kwa Makundi Yaliyo katika Hatari na Ngariba wa Zamani** |
| **10** | **10. Uimarishaji wa mfumo wa Kitaifa wa ufuatiliaji, ujifunzaji na tathmini wa maswala ya ukeketaji** |

Ufanisi na athari za Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30 zitapimwa kwa njia ya mfumo mahsusi wa Vipimo Muhimu vya Mafanikio, vinavyotoa viashiria bainifu vya kufuatilia maendeleo, kuimarisha uwajibikaji na kufanya maboresho ya afua kwa wakati katika kipindi chote cha utekelezaji wa mkakati. Vipimo hivi vitatumika kama rejea kuu ya tathmini ili kubaini kama mkakati unafikia malengo yaliyokusudiwa, ikiwemo kupungua kwa viwango vya ukeketaji, utekelezaji madhubuti wa mifumo ya Kisera na Kisheria, mabadiliko chanya ya kanuni za kijamii na kuimarika kwa uwezo wa mifumo ya kitaifa hususan sekta za elimu na afya kama majukwaa ya kinga na mwitikio wa mapema. Vipimo vya mafanikio vitazingatia kwa makini changamoto inayoibuka ya ukeketaji wa kitabibu, ili kuhakikisha afua zinakabiliana kikamilifu na mwelekeo huu hatarishi. Sehemu hii inaainisha viashiria mahususi na ushahidi wa kimaelezo vitakavyotumika kubaini mafanikio ya mkakati katika kulinda haki, ustawi na utu wa wanawake na watoto wa kike hapa nchini.

**1) Kupungua kwa viwango vya ukeketaji katika maeneo ya kipaumbele**

Kiashiria cha juu zaidi na cha Matokeo ya Muda Mrefu cha mafanikio ni kupungua kwa viwango vya ukeketaji katika ngazi ya taifa na Mikoa 13 ya kipaumbele. Ingawa takwimu za kitaifa zinaonesha kupungua kutoka asilimia 10 mwaka 2015/16 hadi asilimia 8 mwaka 2022, mikoa kama Manyara, Arusha na Mara ambayo imeingizwa katika Mpakati huu kama Mikoa ya Kipaumbele bado ina viwango vya juu. Mkakati utaweka kipaumbele kwa afua lengwa katika Mikoa hii 13 na kupima athari kwa

kutumia tafiti za kitaifa kama Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria pamoja na tafiti za kijamii. Mafanikio yataonekana kupitia mwelekeo endelevu wa kushuka kwa viwango vya ukeketaji miongoni mwa wanawake (miaka 15 - 49) na watoto wa kike (miaka 0-14). Takwimu zilizoainishwa kwa umri, kabila na eneo zitatumika kuhakikisha makundi yaliyo katika hatari kubwa yanafikiwa kwa ufanisi.

**2) Kuongezeka kwa jamii zinazotangaza hadharani kuachana na ukeketaji**

Mabadiliko ya kitabia katika ngazi ya jamii ni msingi endelevu wa kutokomeza vitendo vya ukeketaji. Kiashiria hiki cha matokeo ya Kati kitakuwa idadi ya jamii zinazotoa matamko rasmi na yaliyothibitishwa ya kuachana na ukeketaji, yanayotokana na majadiliano ya muda mrefu, kujifunza mbinu shirikishi na ushirikishwaji wa viongozi wa kimila na kidini. Mkakati unalenga kusaidia na kuthibitisha angalau matamko 300 yatakayotolewa na jamii katika kipindi cha utekelezaji. Ufuatiliaji utafanywa kupitia maafisa maendeleo ya jamii na Asasi za Kiraia. Mafanikio hayatapimwa kwa idadi ya matamko pekee, bali pia kwa ufuatiliaji endelevu wa jamii hizo, unaothibitishwa kupitia ziara za ufuatiliaji, uwajibikaji wa kijamii na kupungua kwa matukio ya ukeketaji baada ya matamko.

**3) Kuimarika kwa upatikanaji na matumizi ya huduma zinazomlenga manusura:**

Utoaji wa huduma jumuishi kwa manusura wa ukeketaji ni hitaji la kimaadili na la kivitendo kwa uponyaji na urejeshwaji kwenye jamii. Mkakati unalenga kupanua huduma za matibabu katika Mikoa 13 ya kipaumbele (ikiwemo upasuaji wa kurekebisha madhara), msaada wa kisaikolojia, msaada wa kisheria na huduma za hifadhi kupitia nyumba salama na vituo vya huduma jumuishi. Ushiriki wa manusura utafuatiliwa kupitia rejesta za rufaa, fomu za matumizi ya huduma na mifumo ya ufuatiliaji wa kesi kupitia Wataalamu wa Afya na Maafisa Ustawi wa Jamii. Takwimu za msingi zinaonesha kuwa hadi 2024/25 manusura 110 pekee walipata huduma jumuishi, kiwango hiki ni cha chini sana cha mahitaji. Mkakati unalenga kuongeza wigo wa huduma mara tatu na kuhakikisha upatikanaji katika wilaya zote zenye viwango vya juu. Tafiti za kuridhika kwa manusura waliopata huduma zitatumika kupima ubora, heshima na ufanisi wa msaada wa ufuatiliaji.

**4) Kuimarika kwa Utekelezaji wa Sheria, Mashitaka na Hukumu za Kesi za Ukeketaji:**

Hatua madhubuti za kisheria ni muhimu ili kushughulikia watuhumiwa wa vitendo vya ukeketaji na kuwezesha kutokomeza kabisa vitendo hivyo. Viashiria vitajumuisha ongezeko la idadi ya kesi zinazo tolewa taarifa katika Dawati la polisi la Jinsia na Watoto, uchunguzi uliofanikiwa na hukumu zinazotolewa. Mkakati pia unalenga kuongeza idadi ya maafisa wa usimamizi wa sheria wakiwemo polisi, waendesha mashitaka na mahakimu waliopata mafunzo kuhusu sheria zinazosimamia kutokomeza ukeketaji na taratibu rafiki kwa manusura. Takwimu zitatokana na taarifa za Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi, kumbukumbu za mahakama na Wizara ya Katiba na Sheria. Viashiria vya kimaelezo kama muda wa mashitaka, ulinzi wa manusura na matumizi ya mbinu zinazotegemea tafiti zitatathiminiwa. Mkakati unapendekeza mbinu za kisheria za kuzuia, ikiwemo kampeni za uelewa wa sheria, maagizo ya mahakama ya kuzuia ukeketaji unaotarajiwa, ushauri wa mapema kwa familia zilizo katika hatari na ulinzi kwa watoa taarifa. Kwa pamoja, hatua hizi zinalenga kuongeza kesi zinazo tolewa taarifa kwa asilimia 50 na hukumu kwa asilimia 60 ndani ya miaka mitano katika maeneo lengwa.

**5) Uwepo wa mifumo yenye ufanisi ya ufuatiliaji wa vitendo vya ukeketaji wa kuvuka mipaka:**

Ukeketaji wa kuvuka mipaka bado ni tishio kubwa, hususan katika wilaya kama Tarime na Longido. Mafanikio yatapimwa kupitia uanzishwaji na ufanisi wa mifumo ya ufuatiliaji, ikiwemo doria za pamoja, ufuatiliaji wa kesi kati ya mamlaka na ushirikiano na mamlaka za Kenya na Uganda. Viashiria vitajumuisha idadi ya watoto wa kike wanaozuiwa kabla ya kuvuka mipaka, kesi zinazotolewa taarifa

kwa pamoja na mashitaka yanayoratibiwa. Mifumo ya utoaji taarifa ndani ya shule na Balozi za nyumba kumi zitatumika kama sehemeu za kutambua na kuweka tahadhari za mapema. Mkakati utatekeleza majaribio ya angalau afua 10 za ushirikiano kati ya wilaya na afua 3 za ushirikiano katika kuvuka mipaka.

**6) Ujumuishaji wa afua za kutokomeza ukeketaji katika mipango ya Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa:**

Uendelevu utapimwa kwa kiwango ambacho afua za kutokomeza ukeketaji zimeingizwa katika mipango ya Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mikoa 13 ya Kipaumbele. Viashiria vitajumuisha idadi ya mipango ya Sekta za Afya, Elimu, Maendeleo ya Jamii na Sheria zenye malengo na bajeti mahsusi za kutokomeza ukeketaji. Mkakati unalenga angalau asilimia 60 ya halmashauri zote za Mikoa 13 zenye viwango vya juu vya ukeketaji zinaingiza afua za ukeketaji katika mipango ya maendeleo na zina mifumo ya ufuatiliaji ifikapo mwaka 2027/28 wa utekelezaji wa Mkakati huu. Uthibitisho utatokana na taarifa za utekelezaji wa bajeti, kumbukumbu za vikao vya halmashauri na mapitio ya sekta.

**7) Utekelezaji madhubuti wa mifumo ya ulinzi mashuleni:**

Shule ni majukwaa muhimu ya kinga na utambuzi wa mapema wa hatari. Viashiria vitajumuisha idadi ya shule zinazotekeleza elimu ya stadi za maisha, ushauri rika na miongozo ya ulinzi wa mtoto. Mkakati utafuatilia mafunzo ya walimu kuhusu ukeketaji, uanzishwaji na uimarishaji wa majukwaa yanayoongozwa na wanafunzi kuhusu afya ya uzazi na ukeketaji. Mfumo wa utoaji taarifa chini ya OWM-TAMISEMI utaandaa taarifa za matukio yanayoshukiwa au yaliyothibitishwa na hatua zilizochukuliwa. Ifikapo mwisho wa mkakati, angalau shule 1,000 katika Mikoa 13 ya kipaumbele zitakuwa zinatekeleza afua za ulinzi.

**8) Ufikiwaji na Matokeo ya Kampeni za Mawasiliano na Elimu kwa Umma**

Uhamasishaji wa umma ni msingi wa kuvunja ukimya na kubadili mitazamo. Wigo wa ufikiaji utapimwa kwa idadi ya watu waliofikiwa kupitia redio, runinga, mitandao ya kijamii, elimu-burudani na machapisho. Matokeo yatapimwa kupitia tafiti za Maarifa, Mitazamo na Mienendo kabla na baada ya kampeni. Ushiriki wa viongozi wa kidini, vijana na wanaume utapewa kipaumbele. Mkakati unalenga kufikia Watanzania milioni 10 kupitia vyombo vya habari na kushirikisha moja kwa moja watu milioni 1 kupitia majadiliano ya kijamii. Kuongezeka kwa utoaji wa taarifa za matukio, kupungua kwa uungwaji mkono wa ukeketaji na kuongezeka kwa matumizi ya mila mbadala za kuvuka rika zisizohusisha ukeketaji vitaonesha ufanisi wa kampeni.

**9) Uwezeshaji wa Kiuchumi kwa Makundi Yaliyo katika Hatari na Ngariba wa Zamani:**

Uwezeshaji wa kiuchumi ni nguzo muhimu katika kupunguza vichocheo vya kiuchumi vinavyoendeleza ukeketaji katika jamii. Kiashiria hiki kitapima kiwango ambacho makundi yaliyo katika hatari pamoja na ngariba wa zamani wamepata na kunufaika na fursa mbadala za kiuchumi kupitia mafunzo ya stadi za maisha, ujasiriamali na upatikanaji wa mitaji au ajira mbadala. Matokeo yatapimwa kwa kuzingatia idadi au asilimia ya wanufaika waliobadilisha vyanzo vyao vya kipato na kudumisha shughuli halali za kiuchumi, pamoja na uthibitisho wa kuacha kabisa kujihusisha na vitendo vya ukeketaji. Aidha, kiashiria kitaangalia kiwango cha kuboreshwa kwa hali ya maisha ya walengwa na mchango wao katika kuhamasisha jamii kuachana na ukeketaji. Mkakati unalenga kuongeza idadi ya wanufaika wanaojitegemea kiuchumi na kupunguza utegemezi wa kipato kinachotokana na ukeketaji, hali itakayochangia kupungua kwa vitendo hivyo na kuimarisha ustawi wa kijamii na kiuchumi katika jamii.

**10) Uimarishaji wa mfumo wa Kitaifa wa ufuatiliaji, ujifunzaji na tathmini wa maswala ya ukeketaji:**

Mfumo imara wa ufuatiliaji, ujifunzaji na tathmini ni muhimu katika kusimamia utekelezaji wa mkakati. Mfumo huu utaoanishwa na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini uliopo wa MTAKUWWA na utajumuisha

uimarishaji na kuhakikisha uwepo wa zana sanifu za takwimu, dashibodi za kidijitali, mapitio ya mara kwa mara na mrejesho kati ya jamii na watoa huduma. Aidha, mfumo utawezesha ufuatiliaji wa viashiria kwa wakati kwa kutumia takwimu zilizo changanuliwa, hivyo kuboresha upangaji wa rasilimali na maamuzi. Mfumo utasimamiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na vitengo vya ufuatiliaji na tathmini vya sekta husika. Lengo ni kuufanya mfumo ufanye kazi kikamilifu ifikapo mwaka wa pili (2026/27) na kuunganishwa kikamilifu katika mfumo wa kitaifa wa takwimu ifikapo mwaka wa tano (2029/30). Vikao vya kujifunza, nyaraka za mbinu bora na tathmini za katikati na mwisho wa kipindi cha utekelezaji vitahakikisha maboresho endelevu.

# 3



Huduma bora kwa manusura wa ukeketaji ni faraja na matumaini mapya

# SURA YA TATU: MSINGI WA MKAKATI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inalenga kutoa dira, dhima, lengo kuu na kanuni elekezi zitakazowaongoza wadau katika sekta mbalimbali, ili kuhakikisha mwitikio ulioratibiwa, unaoeleweka na wenye matokeo dhidi ya ukeketaji. Umuhimu wake upo katika kuweka msingi wa utekelezaji shirikishi na ulioboreshwa, unaolenga kulinda haki, utu na ustawi wa wanawake na watoto wa kike nchini Tanzania na kuharakisha jitihada za kutokomeza kabisa mila hii yenye madhara makubwa.

## 3.2 Dira, Dhima, Lengo Kuu, Malengo ya Kimkakati na Kanuni Elekezi za Mkakati

### 3.2.1 Dira

Kuwa Taifa ambalo wanawake na watoto wa kike wanaishi bila vitendo vya ukeketaji.

### 3.2.2 Dhima

Kuratibu juhudi za kitaifa, shirikishi na jumuishi za kuzuia ukeketaji kupitia ushirikiano wa kisekta unaozingatia haki za binadamu na usawa wa kijinsia.

### 3.2.3 Lengo Kuu


Kupunguza kiwango cha ukeketaji nchini kwa 50%, kutoka 8% mwaka 2024/2025 hadi 4% ifikapo mwaka 2029/30.

### 3.3.4 Malengo ya Kimkakati

| LK1 | LK2 | LK3 | LK4 | LK5 |
|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha utekelezaji wa mifumo ya kisera na kisheria ya kutokomeza ukeketaji | Kuwezesha jamii na watu binafsi kuachana na ukeketaji | Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za kuzuia, utoaji taarifa na mwitikio | Kuimarisha uratibu, ushirikiano wa kisekta na uhamasishaji wa rasilimali | Kuimarisha tafiti na kujifunza |

### 3.3.5 Kanuni Elekezi

Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26 -2029/30 utaongozwa kwa misingi thabiti ya mbinu jumuishi, zinazoutambua ukeketaji si kama suala linalosimama peke yake, bali kama mila iliyojikita kwa kina katika jamii na inayoathiriwa na mwingiliano wa maswala ya kijamii, kitamaduni, kiuchumi, kisheria na kiafya.



Kwa msingi huo, afua zote zimebuniwa, zitatekelezwa kwa njia shirikishi na zenye muingiliano na maswala mengine yenye athari kwa wanawake na mtoto wa kike. Mtazamo huu unajumuisha:

i) Mikakati madhubuti ya kuzuia na inayoshughulikia visababishi vya msingi vya ukeketaji;
ii) Huduma za kuzuia na ulinzi kwa watoto wa kike walio katika hatari;
iii) Utekelezaji thabiti wa mifumo ya kisera na kisheria ili kuwawajibisha wahusika;
iv) Huduma zinazopatikana kwa urahisi, zenye staha na utu kwa manusura wa ukeketaji.

Aidha, mkakati unatambua uhusiano wa karibu kati ya ukeketaji na mila na desturi nyingine zenye madhara kama ndoa za utotoni na ukosefu wa usawa katika elimu na hivyo kushughulikia mwingiliano ili kufanikisha kutokomeza ukeketaji. Kwa mantiki hii, Mkakati huu utazingatia:

**a) Mbinu inayozingatia mageuzi ya kijinsia**

Mbinu inayojikita kwenye mageuzi ya kijinsia inatumika si tu kushughulikia ukeketaji, bali pia kuvunja mila na desturi kandamizi za kijinsia na mifumo ya mamlaka isiyo na usawa inayodumisha desturi hiyo. Kanuni hii inalenga kukuza usawa wa kijinsia kama msingi wa afua zote kwa kuwashirikisha wanawake na wanaume, watoto wa kike na wavulana katika majadiliano ya kina kuhusu dhima hasi za kijinsia. Kupitia kuhimiza mahusiano yenye usawa, maamuzi ya pamoja na kupinga mfumo dume ndani ya familia na jamii, mkakati unalenga kuwawezesha wanawake na watoto wa kike kudai haki zao kamili , ikiwemo haki ya umiliki wa miili yao na hivyo kuondoa mazingira yanayoruhusu ukeketaji kuendelea.

**b) Ujumuishi wa watu wenye ulemavu**

Ujumuishi wa watu wenye ulemavu kwa kuhakikisha afua zote zinawafikia na kujibu mahitaji mahususi ya wanawake na watoto wa kike wenye ulemavu, ambao wako katika hatari kubwa ya kukumbwa na ukeketaji au ni manusura. Kanuni hii inasisitiza ukusanyaji wa takwimu zilizoainishwa ili kuelewa vyema ukubwa na athari za ukeketaji kwa kundi hili; uandaaji na usambazaji wa taarifa katika mifumo inayofikika kama lugha ya alama, maandishi ya nukta nundu au maandishi rahisi; pamoja na utoaji wa huduma rafiki kwa watu wenye ulemavu, ikiwemo vituo vya afya vinavyofikika, msaada wa kisaikolojia unaozingatia mahitaji ya mawasiliano na msaada wa kisheria wenye wataalamu waliobobea katika masuala ya watu wenye ulemavu.

**c) Ushirikishwaji wa jamii**

Ushirikishwaji wa jamii ni nguzo kuu ya mkakati huu, kwa kutambua kwamba kutokomeza ukeketaji, ili uwe endelevu, lazima utoke ndani ya jamii husika. Mkakati unasisitiza mbinu zinazoanzia chini kwenye jamii kuelekea ngazi za juu kwa kuimarisha ushirikiano na viongozi wa jadi na kimila, wazee wanaoheshimika, viongozi wa kidini, vikundi vya wanawake na mitandao ya vijana. Afua zitajumuisha majadiliano ya kina ya kijamii, kuunga mkono jamii kutoa matamko ya pamoja ya kuachana na ukeketaji na kukuza mila mbadala.

**d) Mbinu inayozingatia haki za binadamu**

Mbinu inayozingatia haki za binadamu kwa kutambua ukeketaji kama ukiukwaji mkubwa wa haki za msingi za wanawake na watoto wa kike na si suala la kitamaduni pekee. Afua zote zitaongozwa na viwango vya kitaifa na kimataifa vya haki za binadamu, ikiwemo Mkataba wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake, Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mifumo ya kisera na kisheria ya nchi.

**e) Mbinu inayozingatia mahitaji halisi ya manusura**

Mkakati utatumia mbinu inayozingatia mahitaji, sauti na uwezo wa manusura wa ukeketaji katika hatua zote za upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini. Huduma zote ikiwemo huduma za afya, msaada wa kisaikolojia na msaada wa kisheria zitatolewa kwa kuzingatia faragha, kutohukumu, kuzingatia athari

za kiwewe na heshima kwa maamuzi ya kila manusura. Mkakati pia unalenga kuunda mazingira salama na wezeshi kwa manusura waweze kushirikisha visa vyao, kujenga mitandao ya msaada wa rika na kuwa vinara wa mabadiliko ili kulinda utu wao, ustawi na kupona kabisa.

**f) Ushirikiano wa Kisekta**

Ushirikiano wa kisekta kati ya Wizara za Serikali, ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Utaibu na Wenye Ulemavu); Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; Wizara ya Afya; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Katiba na Sheria; Wizara ya Mambo ya Ndani; Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Asasi za Kiraia, taasisi za kidini na kimila, taasisi za kitaaluma, pamoja na wadau wa maendeleo. Ushirikiano huu unalenga kuhakikisha uratibu mzuri, matumizi bora ya rasilimali na utekelezaji unaolingana katika ngazi zote.

**g) Upangaji na utekelezaji unaozingatia tafiti**

Mkakati huu utajikita kikamilifu katika upangaji na utekelezaji unaozingatia tafiti inayotaka matumizi ya takwimu sahihi na za kuaminika pamoja na ujifunzaji unaotokana na utekelezaji wa afua za awali na zinazoendelea. Kanuni hii itasaidia katika kuongoza maamuzi yote ya kiprogramu, uandaaji wa sera na mgawanyo wa rasilimali. Hii ni pamoja na uimarishaji endelevu wa mifumo ya kitaifa ya ukusanyaji wa takwimu, mwelekeo mpya na ufuatiliaji kupitia dashibodi ya kanzi data jumuishi za kitaifa. Tathmini za mara kwa mara na zinazojitegemea zitapima matokeo ya programu na tija ya gharama, jambo litakalowezesha usimamizi wenye mabadiliko chanya na kutanua wigo wa utekelezaji wa kimkakati wa afua zilizothibitishwa kufanya kazi.

**h) Ubunifu na mabadiliko chanya**

Ubunifu na mabadiliko chanya vitazingatiwa katika mkakati kwa kukuza utamaduni wa ubunifu, unyumbulifu na ujifunzaji endelevu. Hii inajumuisha kutafuta teknolojia mpya kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa taarifa; ufuatiliaji na uwasilishaji wa takwimu kwa njia ya picha; kufanya majaribio ya mbinu mpya za mawasiliano kwa ajili ya mabadiliko ya tabia; kurekebisha afua mara kwa mara kulingana na ushahidi unaoibuka; sifa za kipekee za maeneo husika; na mabadiliko ya vitendo vya ukeketaji.

# 4




Sauti yetu ni mabadiliko; tokomeza ukeketaji

# SURA YA NNE: MFUMO WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inatoa mfumo wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26 - 2029/30. Inabainisha mwelekeo wa kimkakati na mfumo jumuishi utakaoongoza juhudi zote za Kitaifa za kutokomeza ukeketaji. Inaeleza kwa uwazi matarajio ya jumla ya mkakati, inafafanua kwa kina kila Lengo la Kimkakati (LK) na kubainisha matokeo yanayotarajiwa, maeneo ya matokeo pamoja na viashiria vya utekelezaji na ufuatiliaji.

## 4.2 Malengo ya Kimkakati, Matokeo Tarajiwa na Afua za Kimkakati

**Lengo la Kimkakati la Kwanza (LK1): Kuimarisha utekelezaji wa mifumo ya Kisera na Kisheria**

Lengo hili la kimkakati ni msingi wa kuunda mazingira wezeshi ya kuachana na ukeketaji nchini Tanzania. Pamoja na uwepo wa sera na sheria zinazokataza ukeketaji, bado kuna mianya katika ulinganifu wa mifumo ya kitaifa na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, pamoja na changamoto katika utekelezaji wa sheria. LK1 linalenga kuziba mianya hiyo kwa kuhakikisha kuwa mifumo ya usimamizi wa Sheria inaimarishwa kuweza kuboresha utekelezaji na kuzuia vitendo vya ukeketaji, kuwalinda watoto wa kike walio katika hatari na kutoa haki kwa manusura.

Lengo hili linaonesha dhamira ya Serikali kutumia mamlaka yake ya kisheria kama nyenzo ya mabadiliko ya kijamii na kulinda haki za wanawake na watoto wa kike. Utekelezaji wake unazingatia mbinu zifuatazo:

a) **Marekebisho ya Sera na Sheria:** Kwa kupitia na kuboresha Sera na Sheria za Kitaifa ili ziwe jumuishi, ziweke marufuku ya wazi dhidi ya ukeketaji na zijibu changamoto mpya kama ukeketaji wa mipakani na ukeketaji uiofichika. Hii inajumuisha uandaaji wa miongozo na Sheria ndogo ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Kitaifa katika ngazi za chini.

b) **Kujengewa uwezo:** Kuimarisha uwezo wa wadau katika utekelezaji wa Sheria. Itahusisha mafunzo mahsusi kwa Maafisa wa Mahakama, Polisi, Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Viongozi wa Kimila ili waweze kusaidia katika kubaini, kuchunguza, kufuatilia na maamuzi katika kesi za ukeketaji kwa weledi na kwa kuzingatia haki na usalama wa manusura.

Utekelezaji wa LK1 unatarajiwa kuanzisha juhudi za kudhibiti ukeketaji kwa kutoa ujumbe bayana kwamba ukeketaji haukubaliki kijamii na ni kosa kisheria. Kupitia uelewa wa Sheria na utekelezaji thabiti, lengo hili litachangia mabadiliko ya mila na desturi za kijamii, kuimarisha ulinzi wa watoto wa kike walio katika hatari na kuhakikisha manusura wanapata haki.

**Lengo la Kimkakati la Pili (LK2): Kuwezesha Jamii na Watu Binafsi Kuachana na Ukeketaji**

Lengo hili ni kiini cha mabadiliko ya mila na desturi za kijamii na lina umuhimu mkubwa katika kutokomeza ukeketaji na kuhakikisha jitihada endelevu zinazochochewa kutoka ndani ya jamii. Kwa kutambua kuwa ukeketaji umejikita katika mila na desturi, LK2 linalenga kuyawezesha makundi ya jamii na watu binafsi kuwa na maarifa, uelewa na uwezo wa kufanya maamuzi ya kutokomeza ukeketaji.

Lengo hili linakwenda zaidi ya uhamasishaji kwa kulenga mabadiliko ya mitazamo na mienendo. Litahusisha utekelezaji wa kampeni za mawasiliano ya mabadiliko ya tabia zinazozingatia muktadha wa eneo husika kwa kutumia vyombo mbalimbali vya habari na kuwashirikisha viongozi wa kidini na kimila, wanaume na wavulana kama vinara wa mabadiliko. Majadiliano ya wazi kuhusu madhara ya ukeketaji na haki za binadamu yatapewa kipaumbele. Aidha, LK2 litaimarisha mifumo ya msaada wa kijamii kwa manusura na kuimarisha miundo ya kijamii inayokuza uponyaji na ustahimilivu.

Kupitia uwezeshaji huu, jamii zitahamasishwa kutoa matamko ya wazi ya kuachana na ukeketaji, yakionesha dhamira ya pamoja ya kuwalinda watoto wa kike. Mafanikio ya LK2 yatadhihirika kupitia kupungua kwa kiwango cha ukeketaji kinachosukumwa na maamuzi ya jamii yenyewe pamoja na kuimarika kwa ustawi wa kijamii na kiuchumi kwa wale waliokuwa wakihusika au kuathiriwa na ukeketaji. Lengo hili linaweka msingi wa kizazi kipya kisicho na ukeketaji.

**Lengo la Kimkakati la Tatu (LK3): Kuimarisha Upatikanaji wa Huduma Bora za Kinga, Utoaji Taarifa na Mwitikio**

Lengo hili linahakikisha kuwa huduma muhimu zinapatikana kwa urahisi ili kuzuia ukeketaji na kutoa msaada wa kina kwa manusura. Linajibu hitaji la kuwepo kwa mfumo thabiti wa utoaji huduma unaokidhi mahitaji ya kiafya, kisaikolojia na kisheria ya watoto wa kike na wanawake walio katika hatari au manusura wa ukeketaji. Mkazo unawekwa katika mtazamo unaomlenga manusura kwa kuhakikisha huduma zinatolewa kwa ubora sambamba na juhudi za kuzuia ukeketaji usijitokeze.

Utekelezaji wa LK3 utahusisha kuimarisha uwezo wa watoa huduma katika sekta mbalimbali. Hii ni pamoja na kujumuisha elimu ya kuzuia ukeketaji katika mitaala ya shule na programu za vijana, kuwajengea uwezo Wahudumu wa Afya katika kuimarisha huduma stahiki kwa manusura na kuwawezesha Maafisa Ustawi wa Jamii kuimarisha msaada wa kisaikolojia na kisheria. Kuanzisha na kuimarisha vituo vya huduma jumuishi na nyumba salama ni hatua muhimu za kutoa ulinzi wa haraka kwa watoto wa kike walio katika hatari. Aidha, kuandaa miongozo ya usimamizi wa kesi kwa ushirikiano wa kisekta ni muhimu ili kuhakikisha huduma jumuishi na zenye uratibu zinapatikana.

Matokeo yanayotarajiwa ni kuimarika kwa usalama na ustawi wa watoto wa kike na wanawake pamoja na ongezeko la upatikanaji wa huduma za kuokoa maisha na kusaidia urejeshwaji. Lengo hili linaweka ukeketaji kama suala la Afya ya Umma na Ustawi wa Jamii linalohitaji mwitikio wa kitaalamu wa haraka na endelevu.

**Lengo la Kimkakati la Nne (LK4): Kuimarisha Uratibu, Ushirikiano wa Kisekta na Uhamasishaji wa Rasilimali**

Uratibu madhubuti wa kisekta na ushirikiano imara ni nguzo muhimu za mafanikio na uendelevu wa mkakati huu. LK4 linatambua kuwa ukeketaji ni suala linalogusa sekta nyingi na linahitaji mshikamano wa wadau kuanzia Wizara na Taasisi za Serikali, Wadau wa Maendeleo, Asasi za Kiraia na Taasisi za Kijamii. Bila mifumo thabiti ya uratibu, juhudi zinaweza kugawanyika, rasilimali kutumika isivyo tija na matokeo tarajiwa kutokufikiwa.

Lengo hili linatoa kipaumbele kwa kuanzishwa na kuimarishwa kwa kamati za uratibu wa kisekta katika ngazi za Taifa, Kanda, Mkoa, Wilaya na Kata ili kuhakikisha afua za kutokomeza ukeketaji zinaunganishwa katika mifumo ya Serikali za Mitaa. Ufafanuzi wa majukumu na wajibu wa kila mdau ni muhimu ili kuepusha kujirudia na kuongeza ufanisi. Aidha, LK4 linaweka mkazo katika uhamasishaji wa rasilimali za ndani na nje kwa kushawishi ongezeko la bajeti za Serikali na kuimarisha ushirikiano na wadau wa utekelezaji na ufadhili.

Mafanikio ya LK4 yataleta utekelezaji ulio bora na wenye matokeo zaidi, matumizi ya rasilimali yaliyopangwa vyema na uwekezaji endelevu wa wadau wote, hivyo kuharakisha kutokomeza ukeketaji nchini.

**Lengo la Kimkakati la Tano (LK5): Kuimarisha Tafiti na Ujifunzaji**

Lengo hili ni muhimu katika kuhakikisha mkakati unabaki kuwa unaotegemea tafiti na unaojiboresha kadri mazingira yanavyobadilika. Katika muktadha ambapo mbinu za ukeketaji zinaweza kubadilika, uwepo wa mifumo imara ya ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa ni jambo la lazima. LK5

linalenga kujenga msingi thabiti wa ushahidi kwa ajili ya kufanya maamuzi ya kisera, kuboresha muundo wa afua na kukuza ujifunzaji.


Shughuli kuu chini ya LK5 zitajumuisha tafiti za mara kwa mara za viwango vya ukeketaji, tafiti za ubora ili kuelewa mienendo na visababishi, pamoja na kuimarisha mifumo ya Kitaifa ya ukusanyaji wa takwimu zilizoainishwa. Aidha, lengo hili litasisitiza uhifadhi na usambazaji wa mbinu bora, mafunzo na ubunifu kutoka maeneo mbalimbali pamoja na kuanzisha majukwaa ya kubadilishana maarifa kati ya watendaji na watunga sera.

Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni mkakati unaoendeshwa kwa taarifa sahihi, unaoweza kuboreshwa kwa wakati na unaotekelezeka kwa ufanisi zaidi. Kupitia uamuzi unaotegemea tafiti na ujifunzaji endelevu, rasilimali zitaelekezwa kwenye afua zenye matokeo makubwa, hivyo kuharakisha kutokomeza vitendo vya ukeketaji nchini.

## 4.3 Matokeo Muhimu na afua za Kimkakati

**Maeneo ya Matokeo ya Kati (EMK) ya Kimkakati chini ya LK1**

**EMK 1.1: Kuimarika kwa Ulinganifu wa Sera na Sheria za Kitaifa na Mifumo ya Kikanda na Kimataifa ya Haki za Binadamu katika Kuzuia Ukeketaji**




Eneo hili la Matokeo linaweka msingi wa kuanzisha mazingira imara ya kisheria yanayokataza kabisa Ukeketaji nchini. Linasisitiza umuhimu wa kuhakikisha kuwa Sera na Sheria za kitaifa zinaendana kikamilifu na ulinzi na makatazo yaliyoainishwa katika mifumo ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu ikiwemo Mkataba wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake(1979), Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto,(1989) na Itifaki ya Maputo, (2003).

Ingawa Tanzania ina sheria zinazokataza ukeketaji, mapitio endelevu ya mifumo hiyo ni muhimu ili kubaini na kushughulikia mianya, sintofahamu au mapungufu yanayoweza kudhoofisha utekelezaji na ufuatiliaji wa kesi. Hii inajumuisha kurekebisha sheria ili kushughulikia mienendo mipya ya ukeketaji, kama vile ukeketaji wa kuvuka mipakani, pamoja na kuhakikisha kuwa aina zote za ukeketaji zimekatazwa waziwazi bila kutoa nafasi ya tafsiri tofauti. Lengo ni kujenga mfumo wa kisheria usio na mianya na unaopinga ukeketaji katika hali zote.

Ulinganifu huu hauishii kwenye marekebisho ya sheria pekee, bali unahusisha pia usambazaji mpana wa nyaraka za kisheria zilizoboreshwa na kuhakikisha zinaeleweka vyema na wadau wote, wakiwemo maafisa wa mahakama, viongozi wa jamii na wananchi kwa ujumla. Mkakati unajumuisha uandaaji wa miongozo rafiki ya kisheria, sheria ndogo ndogo za mamlaka za serikali za mitaa na maelezo ya ufafanuzi ili kuwezesha utekelezaji wa sheria katika ngazi ya jamii. Hii itahakikisha kuwa sheria hazibaki kuwa nyaraka za kinadharia bali zinakuwa zana za vitendo za ulinzi na kuzuia ukeketaji.

Hatimaye, kuwepo kwa mfumo wa kisheria ulio wazi, jumuishi na unaoeleweka kunatarajiwa kuwazuia wahalifu, kuwawezesha jamii kudai haki na kuwawajibisha wahusika wa vitendo vya ukeketaji, hivyo kuimarisha dhamira ya kutokomeza kabisa ukeketaji.

**Afua za Kimkakati**

- Kuwezesha ulinganifu wa Sera na Sheria za Kitaifa na Mifumo ya Kimataifa ya haki za binadamu (ikiwemo Itifaki ya Maputo, CRC na CEDAW) kupitia mapitio ya sera, msaada wa kitaalamu na mashauriano ya wadau wa kisekta.
- Kufanya mapitio na marekebisho ya mifumo ya kisera na kisheria ili kuhakikisha yanakataza waziwazi ukeketaji na kuendana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.

**Viashiria**

- Idadi ya Sera na Sheria zilizolinganishwa na mifumo ya kimataifa.
- Idadi ya Sera na Sheria zilizopitiwa au kutungwa ili kushughulikia moja kwa moja masuala yanayohusiana na ukekeltaji.

**Matokeo ya Awali ya Utekelezaji**

- Sera na Sheria za kutokomeza ukeketaji zimelinganishwa kikamilifu na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu na kupitishwa rasmi.
- Sera na Sheria zimeboreshwa ili kukataza waziwazi ukeketaji na kuendana na viwango vya Kimataifa.

**EMK 1.2: Kuimarika kwa uwezo wa watendaji wa kisheria na vyombo vya usalama katika kutekeleza na kusimamia kwa ufanisi sheria za kupambana na ukeketaji**

Eneo hili la Matokeo ni la msingi katika kusimamia na kutekeleza Sheria ili kuwasaidia manusura wa ukeketaji. Pamoja na kuwepo kwa sheria imara, ufanisi wake unategemea uwezo wa taasisi na watu binafsi wanaohusika na utekelezaji. Maafisa wa utekelezaji wa sheria na utoaji haki, wakiwemo olisi, Maafisa wa Mahakama, Ustawi wa Jamii na Uhamiaji wanapaswa kujengewa uwezo wa kuweza kutambua aina za ukeketaji na kushughulikia kesi kwa kuzingatia mahitaji ya manusura.

Watendaji husika watapatiwa mafunzo, rasilimali na mifumo ya uratibu yanayowawezesha kutekeleza sheria za kutokomeza ukeketaji, kufanya uchunguzi wa kina, kufuatilia kesi kwa ufanisi na kutoa msaada stahiki kwa manusura. Ili kuhakikisha uendelevu, mafunzo haya yataingizwa katika mitaala ya Taasisi za Kisheria. Hatua hii itaongeza uelewa wa ukeketaji kama ukiukwaji wa haki za binadamu na kujenga uwezo wa kufanya mahojiano yanayomlinda mwathirika, ukusanyaji wa ushahidi na ufuatiliaji wa taratibu za kisheria zinazohusiana na kesi za ukeketaji.

**Afua za Kimkakati**

- Kuimarisha uwezo wa watendaji wa sheria na mifumo ya utekelezaji wa sheria katika kuzuia, utoaji taarifa na mwitikio dhidi ya ukeketaji.
- Kuanzisha na kuimarisha Taratibu za Uendeshaji (*Standard Operating Procedures -SOPs*) kwa ajili ya kushughulikia kesi za ukeketaji ndani ya vyombo vya utekelezaji wa sheria.

**Viashiria**


- Asilimia ya ongezeko la watendaji wa utekelezaji wa sheria waliopata mafunzo kuhusu kuzuia, utoaji taarifa na mwitikio dhidi ya ukeketaji.
- Idadi ya watendaji wa sheria na mifumo ya utekelezaji wa sheria waliojengewa uwezo katika kuzuia, utoaji taarifa na mwitikio dhidi ya ukeketaji.
- Uwepo wa Taratibu za Uendeshaji katika kushughulikia kesi za ukeketaji.

**Matokeo ya Awali Utekelezaji**

- Uwezo wa watendaji wa kisheria na vyombo vya usalama katika utekelezaji wa Sheria za kutokomeza ukeketaji umeimarika.
- Taratibu za Uendeshaji katika kushughulikia kesi za ukeketaji imepitishwa na inatekelezwa.

**Maeneo ya Matokeo ya Kati (EMK) ya Kimkakati chini ya LK2**

**EMK 2.1: Kuongezeka kwa uelewa wa jamii na kukataa ukeketaji kama mila na desturi yenye madhara**




Eneo hili la Matokeo ni msingi wa kutokomeza vitendo vya ukeketaji, kwa kuwa ukeketaji unaendelezwa zaidi na mifumo ya kijamii, mila na desturi katika maeneo yaliyoathirika. Kufikia mabadiliko endelevu kunahitaji zaidi ya uwepo wa sheria; kunahitaji mabadiliko ya kina katika mitazamo, imani na mienendo ya jamii kuhusu ukeketaji. Eneo hili linalenga utaratibu katika kuongeza uelewa wa jamii kuhusu madhara makubwa ya kiafya, kisaikolojia na ukiukwaji wa haki za binadamu unaosababishwa na ukeketaji, sambamba na kupinga hoja za kitamaduni zinazotumiwa kuhalalisha kuendelea kwa vitendo hivyo.

Lengo kuu ni kujenga mazingira ambayo jamii zinatambua wazi kuwa ukeketaji ni kitendo chenye madhara na kuchagua kwa hiari kuachana nacho. Mafanikio ya eneo hili yanategemea juhudi zinazowaleta pamoja watu na makundi mbalimbali ambao wanaelewa madhara ya ukeketaji na kuchukua msimamo wa wazi wa kukataa. Hii inajumuisha kuwawezesha wanawake na watoto wa kike kudai haki zao, kuwaelimisha wanaume na wavulana kuwa washirika muhimu wa mabadiliko na kuwahamasisha viongozi wa jamii kuwa vinara wa mabadiliko.

Jamii zinapopata uelewa mpana wa athari za ukeketaji na kupewa mbadala chanya wa kitamaduni unaoheshimu utambulisho wao bila kuumiza, zina uwezekano mkubwa wa kuachana na ukeketaji kwa pamoja. Hali hii huibua sauti ya pamoja kutoka uelewa wa kawaida hadi msimamo wa wazi wa kukataa ukeketaji na kuleta mabadiliko ya kudumu ya tabia na kujenga mazingira salama kwa vizazi vijavyo bila ukeketaji.

**Afua za Kimkakati**

- Kufanya kampeni za kutokomeza ukeketaji.
- Kuwashirikisha viongozi wa dini na wa kimila katika juhudi za kutokomeza ukeketaji
- Kuhamasisha wanaume na wavulana kuwa vinara wa mabadiliko na kuunga mkono jitihada za kutokomeza ukeketaji.
- Kuwajengea uwezo wanawake na watoto wa kike kuwa vinara wa mabadiliko.

**Viashiria**

- Asilimia ya ongezeko la wanajamii wenye uelewa wa madhara ya ukeketaji na athari zake za kisheria.
- Idadi ya viongozi wa dini na wa kimila wanaohamasisha kikamilifu kutokomeza ukeketaji katika jamii zao.
- Asilimia ya ongezeko la wanaume na wavulana vinara wa kutokomeza ukeketaji.

**Matokeo ya Awali ya Utekelezaji**

- Kampeni za uelewa wa jamii zimefanikiwa kupinga na kubadili mifumo ya kijamii inayounga mkono ukeketaji.
- Viongozi wa kimila na wa dini wamewezeshwa na kuhamasishwa kushiriki mabadiliko katika kukuza mila mbadala zisizohusisha ukeketaji na kuongoza jitihada za kijamii za kutokomeza ukeketaji.
- Wanaume na wavulana vinara wa mabadiliko wanashiriki na kuunga mkono jitihada za kutokomeza ukeketaji.
- Wanawake na watoto wa kike vinara wa mabadiliko wanashiriki na kuunga mkono juhudi za kutokomoeza ukeketaji.

**EMK 2.2: Kuimarika kwa Uwezeshaji wa Kiuchumi na Mifumo ya Msaada wa Kijamii kwa Ngariba na Manusura**

Eneo hili la Matokeo Muhimu ni muhimu katika kuhakikisha uendelevu wa kuacha vitendo vya ukeketaji na kusaidia urejeshwaji kamili wa manusura katika jamii. Ushiriki wa ngariba katika kukeketa mara nyingi husukumwa na motisha ya kiuchumi au hadhi ya kijamii, hali inayofanya iwe vigumu kuacha vitendo hivyo bila kuwepo kwa kipato mbadala kinacho aminika. Aidha, manusura wa ukeketaji hukabiliwa na changamoto za kiafya, kisaikolojia na kijamii zinazohitaji msaada wa kina na endelevu.

Eneo hili linatambua kuwa kutokomeza ukeketaji hakuhitaji tu juhudi za kisheria na uhamasishaji, bali pia kuanzishwa kwa mifumo endelevu ya kiuchumi na ulinzi katika jamii. Afua za uwezeshaji kiuchumi zinalenga ngariba waliobainishwa, kwa kuwawezesha kupata kipato mbadala kama mikopo isiyo na riba ya Serikali za Mitaa au msaada wa kuanzisha shughuli za kiuchumi. Hatua hizi zinasaidia kuondoa msukumo wa kifedha unaoendeleza vitendo vya ukeketaji.

Kwa ujumla, uwezeshaji wa kiuchumi na msaada wa kijamii unalenga pande zote mbili ikiwemo wale wanaohitaji na wanaotekeleza ukeketaji (ngariba) katika kutokomeza vitendo hivi. Kuwezesha ngariba kushiriki katika vyanzo mbadala na endelevu vya kipato kunapunguza idadi ya watoto wa kike wanaofanyiwa ukeketaji, aidha kuwawezesha manusura kwa msaada stahiki kunajenga ustahimilivu na ulinzi wa haki na ustawi wao. Mkakati huu jumuishi ni nguzo muhimu ya kujenga jamii inayo achana kabisa na ukeketaji.

**Afua za Kimkakati**

- Kuwawezesha kiuchumi ngariba waliobainishwa ili kuwasaidia kuingia kwenye shughuli mbadala endelevu za kujipatia kipato.
- Kuanzisha na kuimarisha mitandao jumuishi ya msaada wa kijamii kwa manusura wa ukeketaji.

**Viashiria**


- Idadi ya ngariba waliopata mafunzo ya uwezeshaji kiuchumu na stadi mbadala za kujipatia kipato
- Idadi ya ngariba waliotambuliwa na kuingizwa katika vyanzo mbadala na endelevu vya kiuchumi.

**Matokeo ya Awali ya Utekelezaji**

- Idadi ya mangariba waliopata mafunzo ya uwezeshaji kiuchumu na stadi mbadala za kujipatia kipato.
- Msaada endelevu wa uwezeshaji wa kiuchumi umeongezeka kwa mangariba wa zamani na manusura

**Eneo la Matokeo ya Kati (EMK) la Kimkakati chini ya LK3**

**EMK 3.1: Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma jumuishi za kuzuia, kutoa taarifa na mwitikio kwa manusura**




Eneo hili la Matokeo lina lengo la kuanzisha na kuimarisha mfumo imara na jumuishi wa utoaji huduma unaoshughulikia kwa ukamilifu mnyororo mzima wa kuzuia, utoaji wa taarifa kwa wakati na upatikanaji wa huduma kwa manusura .

Afua za kinga zinalenga kuzuia ukeketaji kabla haujatokea kwa kuyawezesha makundi ya jamii kwa taarifa sahihi, mifumo ya tahadhari ya mapema na majukwaa yanayofikika. Mifumo ya kutoa taarifa inapaswa kuwa salama, ya siri na inayozingatia muktadha wa kitamaduni ili kuhamasisha utoaji wa taarifa kwa wakati na kuimarisha uwajibikaji. Huduma za mwitikio zinaandaliwa kulingana na mahitaji mahususi ya manusura, zikiwemo huduma za haraka za kitabibu, ushauri nasaha na msaada wa kisaikolojia.

Kwa kuunganisha vipengele hivi katika mfumo mmoja unaofanya kazi kwa uratibu wa kisekta, mkakati unajenga mazingira ambayo watoto wa kike wanalindwa dhidi ya ukeketaji, manusura wanapata msaada wenye heshima na unaozingatia utu wao na jamii zinashiriki kikamilifu katika kutokomeza ukeketaji. Mkakati huu wa Kisekta unaimarisha uwezo wa taasisi, unajenga imani kwa jamii na hatimaye unachangia kutokomeza ukeketaji kwa uendelevu.

**Afua za Kimkakati**

- Kuanzisha na kuimarisha nyumba salama, vituo jumuishi na huduma mkoba (*outreach*) vya huduma kwa manusura wa ukeketaji.
- Kuimarisha rufaa na utoaji huduma kwa kuwajengea uwezo watoa huduma za afya, Maafisa Ustawi wa Jamii na wataalamu wa Sheria.
- Kuboresha maudhui yanayolingana na umri kuhusu kinga dhidi ya ukeketaji katika mitaala ya Afya, Elimu na programu za elimu isiyo rasmi.
- Kuandaa na kuingiza rasmi huduma maalum za kuzuia, kutoa taarifa na kukabiliana na ukeketaji katika mifumo ya utekelezaji ili kuhakikisha uthabiti, uwajibikaji na ubora wa huduma katika mikoa yote.

**Viashiria**


- Asilimia ya manusura wa ukeketaji wanaopata huduma jumuishi za kitabibu, kisaikolojia na kisheria.
- Maudhui yalioboreshwa kuhusu kinga dhidi ya ukeketaji katika mitaala ya shule na programu za elimu isiyo rasmi.
- Idadi ya nyumba salama kwa manusura wa ukeketaji zilizoanzishwa na kuimarishwa.
- Idadi ya vituo vya huduma jumuishi za huduma kwa manusura wa ukeketaji zilizoanzishwa na kuimarishwa.
- Idadi ya watoa huduma za afya, Maafisa Ustawi wa Jamii na wataalamu wa Sheria waliojengewa uwezo wa kuimarisha rufaa.
- Idadi ya manusura wa ukeketaji na wasichana walio katika mazingira hatarishi wanaopata huduma za kisaikolojia, kijamii au msaada wa kiuchumi

**Matokeo ya Awali ya Utekelezaji**

- Vituo vya utoaji Huduma Jumuishi, nyumba salama na huduma za mkoba zimeimarishwa ili kutoa huduma zinazofikika na zinazomlenga manusura katika nyanja za kitabibu, kisaikolojia na kisheria.
- Mifumo ya rufaa na uwezo wa watoa huduma za Afya, Maafisa Ustawi wa Jamii na wataalamu wa Sheria umeimarika.
- Maudhui yanayolingana na umri kuhusu kinga dhidi ya ukeketaji yameingizwa katika mitaala Afya, Elimu na programu za elimu isiyo rasmi.
- Huduma maalum za kuzuia, kutoa taarifa na kukabiliana na ukeketaji imeandaliwa na kuingizwa rasmi katika mifumo ya utekelezaji ili kuhakikisha uthabiti, uwajibikaji na ubora wa huduma katika mikoa 13 ya kipaumbele.

**Maeneo ya Matokeo ya Kati (EMK) ya Kimkakati chini ya LK4**

**EMK 4.1: Kuimarika kwa Uratibu na Ushirikiano wa Kisekta miongoni mwa Wadau**




Eneo hili la Matokeo ni nguzo ya msingi katika kuhakikisha uthabiti, ufanisi na tija kwa Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30. Ukeketaji ni tatizo linalochangiwa na mienendo ya kijamii na kitamaduni, hali za kiuchumi pamoja na mifumo ya Kisera na Kisheria, hivyo zinahitaji juhudi za pamoja na shirikishi kutoka kwa wadau mbalimbali. Wadau hawa ni pamoja na Wizara, idara na taasisi za serikali, Asasi za Kiraia, viongozi wa kimila, koo, dini, wadau wa maendeleo, pamoja na vikundi vya kijamii katika ngazi ya jamii.

Bila uratibu madhubuti na ushirikiano wa kweli wa kisekta, afua za kutokomeza ukeketaji ziko katika hatari ya kutotekelezwa ipasavyo, rasilimali kutumika bila tija na athari za jumla kupungua. EMK 4.1 linalenga kujenga mkakati ambapo wadau wote wanatekeleza majukumu yao kwa mshikamano, wakitumia mamlaka yao, utaalamu na mitandao wa kijamii waliyonayo ili kuharakisha kutokomeza ukeketaji nchini kote.

**EMK 4.1: Kuimarika kwa Uratibu na Ushirikiano wa Kisekta miongoni mwa Wadau**

**Afua za Kimkakati**

- Kuimarisha Kikundi Kazi cha Taifa cha kutokomeza ukeketaji.
- Kuimarisha mifumo ya uratibu wa ngazi za Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji/Mtaa.

**Viashiria**

- Idadi ya wanachama wanaohudhuria vikao na wenye uwajibikaji wa Kamati ya Kiufundi ya Kisekta
- Idadi ya mikutano ya wadau yaliyoratibiwa katika ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji/Mtaa.

**Matokeo ya Awali ya Utekelezaji**

- Majukwaa ya uratibu ya kitaifa na ya ngazi za chini yameanzishwa na yanafanya kazi ipasavyo kwa ajili ya kutokomeza ukeketaji.
- Afua za pamoja za kisekta zilizobuniwa na kutekelezwa kupitia mifumo ya uratibu iliyoanzishwa.

**EMK 4.2: Kuongezeka kwa rasilimali fedha na utaalamu endelevu kwa ajili ya kutokomeza ukeketaji**

Eneo hili la Matokeo ni la msingi katika kuhakikisha utekelezaji wenye tija na uendelevu wa Mkakati katika kutokomeza kwa vitendo ukeketaji ambao ni mila yenye mizizi ya muda mrefu. Kunahitaji uwekezaji mkubwa na endelevu katika mageuzi ya kisera na Kisheria, uwezeshaji wa jamii, utoaji wa huduma na uzalishaji wa tafiti na takwimu. Bila rasilimali za kutosha za kifedha na kiufundi, afua zilizopangwa zinaweza zisitekelezeke na kushindwa kuleta matokeo yanayotarajiwa.

Mafanikio ya EMK 4.2 yanategemea kuongeza na kutofautisha vyanzo vya rasilimali. Ingawa mchango wa wadau wa maendeleo unaendelea kuwa muhimu, eneo hili linasisitiza umuhimu wa kuongeza mgao wa bajeti za ndani za serikali na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi. Aidha, linaweka mkazo katika kujenga uwezo wa wadau wanaotekeleza mkakati katika kusimamia rasilimali kwa uwazi, ufanisi na uwajibikaji, ili kila rasilimali itumike kuleta mabadiliko halisi katika jamii.

Kupitia uhamasishaji na matumizi bora ya rasilimali za kifedha na kiufundi, Tanzania itaweza kuhakikisha kuwa dhamira yake thabiti ya kutokomeza ukeketaji inaendana na uwezo wa utekelezaji na hivyo kulinda utu, haki na mustakabali wa watoto wa kike na wanawake kote nchini.

**Afua za Kimkakati**

- Kuandaa na kutekeleza mkakati wa uhamasishaji wa rasilimali kwa ajili ya kutokomeza ukeketaji.
- Ujumuishaji wa afua za ukeketaji katika mipango na bajeti za kisekta za Mikoa 13 ya Kipaumbele, kwa kushirikisha Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ili kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali za Serikali kwa uendelevu katika sekta husika.

**Viashiria**


- Asilimilia ya ongezeko la rasilimali za kifedha zilizohamasishwa ndani ya nchi na kimataifa kwa kutokomeza ukeketaji.
- Asilimia ya ongezeko la mgao wa bajeti za Serikali katika sekta husika kwa utekelezaji wa afua za kutokomeza ukeketaji.
- Uwepo wa mkakati wa uhamasishaji wa rasimali kwa ajili ya kutokomeza ukeketaji.
- Idadi ya taasisi zilizoahidi rasilimali fedha kwa kutokomeza ukeketaji
- Idadi ya programu au miradi ya ukeketaji iliyofadhiliwa
- Idadi ya Mikoa iliyoingiza huduma maalum za kuzuia, kutoa taarifa na kukabiliana na ukeketaji katika mifumo ya utekelezaji ili kuhakikisha uthabiti, uwajibikaji na ubora.

**Matokeo ya Awali ya Utekelezaji**

- Mifumo bunifu ya ufadhili imeanzishwa, ikijumuisha serikali, wadau wa maendeleo na sekta binafsi, kwa ajili ya kufadhili afua za kutokomeza ukeketaji.
- Ongezeko la mgao wa bajeti za Serikali katika sekta husika kwa utekelezaji wa afua za kutokomeza ukeketaji.

**Matokeo ya Kati chini ya LK5**

**EMK 5.1: Kuimarika kwa tafiti na takwimu kwa ajili ya afua na uundaji wa sera za kutokomeza ukeketaji**




Eneo hili la Matokeo ni la msingi katika kuhakikisha kuwa Mkakati unabaki kuwa wenye ufanisi, unaoendana muktadha halisi na unaoweza kujibu changamoto zinazoibuka kwa wakati. Kutokomeza ukeketaji kunahitaji afua ambazo zina matoeko yaliyothibitishwa kupitia tafiti na takwimu sahihi.

EMK 5.1 linalenga kuzalisha, kuchambua na kuratibu matumizi ya tafiti na takwimu ili kuongeza uelewa wa mienendo ya ukeketaji, kubaini vichocheo na vikwazo vya kuachana na mila hii na kutathmini ufanisi wa afua na sera mbalimbali. Kwa kuweka mkazo kwenye uzalishaji wa tafiti, mkakati unaimarisha dhamira yake ya kufanya maamuzi yanayotegemea tafiti na hivyo kuwezesha maboresho endelevu na marekebisho ya kimkakati kuelekea lengo kuu la kutokomeza ukeketaji.

**Afua za Kimkakati**

- Kufanya tafiti za kusaidia uboreshaji wa afua za kutokomeza ukeketaji.
- Kuimarisha mifumo ya na ukusanyaji wa takwimu.

**Viashiria**

- Idadi ya tafiti mahsusi za ukeketaji zilizofanyika.
- Idadi ya mifumo ya takwimu iliyoboreshwa.

**Matokeo ya Awali ya Utekelezaji**

- Sera na programu za kutokomeza ukeketaji zinazozingatia takwimu na tafiti
- Takwimu za ukeketaji zimejumuishwa katika mifumo ya kitaifa.

**EMK 5.2: Kuimarika kwa uwezo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji katika afua za kutokomeza ukeketaji**

Eneo hili la Matokeo ni mahsusi katika kuhakikisha uwajibikaji, uwazi na uboreshaji endelevu wa utekelezaji wa Mkakati. Linaweka mkazo kwenye umuhimu wa mifumo thabiti ya ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji ili kufuatilia maendeleo, kupima matokeo, kubaini changamoto na kurekebisha afua kwa wakati kulingana na takwimu zinazopatikana.

Kwa kuimarisha uwezo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji kwa wadau wote kuanzia vyombo vya kitaifa vya uratibu hadi watekelezaji wa ngazi ya jamii, mkakati unalenga kubadilisha mtazamo wa ufuatiliaji kutoka kutazama shughuli pekee hadi kuzingatia upimaji wa matokeo. Hii itawezesha maboresho ya afua yanayotegemea tafiti, matumizi bora ya rasilimali na kuongeza uwekezaji katika mbinu zilizothibitishwa kuwa na mafanikio.

**Afua za Kimkakati**

- Kubuni na kutekeleza programu mahsusi za kujenga uwezo kwa wadau katika ufuatiliaji, tathmini na matumizi ya takwimu za ukeketaji.
- Kuendesha jukwaa la Kitaifa la kila mwaka la ujifunzaji la wadau wanaotekeleza afua za kutokomeza ukeketaji.
- Kufanya tathmini za kati na za mwisho za utekelezaji wa Mkakati.

**Viashiria**

- Idadi ya wadau waliopatiwa mafunzo ya ufuatiliaji, tathmini na matumizi ya takwimu za ukeketaji.
- Idadi ya wadau walioingiza mifumo ya ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji katika afua zao za kutokomeza ukeketaji.
- Idadi ya mbinu bora za mfano zilizofanya vizuri kwenye utekelezaji.
- Taarifa ya tathmini ya kati na ya mwisho ya utekelezaji wa Mkakati.

**Matokeo ya Awali ya Utekelezaji**

- Mfumo wa kitaifa wa Ufuatiliaji, Tathmini na Ujifunzaji kuhusu ukeketaji umeimarishwa.
- Taarifa za majukwaa ya kujifunza, kushirikishana maarifa na mifumo ya mrejesho wa utekelezaji wa Mkakati.
- Taarifa ya tathmini ya kati na ya mwisho ya utekelezaji wa Mkakati inayoelezea maendeleo ya utekelezaji wa Mkakati.

## 4.4 Nadharia ya mabaadiliko

Nadharia ya Mabadiliko inajengwa kwa namna ambayo afua mbalimbali zitaweza kuleta mabadiliko yanayotarajiwa na kuzingatia kwa kina mlolongo wa kimantiki *(causal pathway)* unaounganisha rasilimali, shughuli na matokeo ili kufikia dira ya Taifa lisilo na ukeketaji. Inaonesha uhusiano wa moja kwa moja kati ya afua, matokeo na athari, huku ikisisitiza uratibu wa kitaifa na ushirikishwaji wa wadau (tazama mchoro hapo juu). Unaanza na shughuli/afua zinazotekelezwa, zikiwemo kuboresha sera na sheria, kufanya kampeni za uhamasishaji, kujenga uwezo wa watendaji na taasisi, pamoja na kuwezesha kiuchumi makundi lengwa. Shughuli hizi zinatarajiwa kusababisha matokeo ya awali, kama vile kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma jumuishi za kuzuia na kushughulikia ukeketaji, kuimarika kwa ushirikiano wa kisekta na kuongezeka kwa uelewa wa jamii.

## *Nadharia ya mabadiliko*

Shughuli/Afua → Matokeo ya Awali → Matokeo ya Kati → Matokeo ya Muda Mrefu → Dira

**Juhudi za Kitaifa zenye rasilimali, shirikishi na jumuishi zinazoratibiwa na kuzingatia usawa wa kijinsia na Haki za Binadamu**

### Shughuli/Afua

- Kupitia Sera na Sheria za Kitaifa
- Kujenga uwezo wa watendaji na mifumo ya utekelezaji wa sheria
- Kuandaa Taratibu za Uendeshaji wa kesi za Ukeketaji

**Matokeo ya Awali:**
- Kuongezeka kwa idadi ya watendaji na wasimamizi wa Sheria waliojengewa uwezo
- Kuboreka kwa Sera na Sheria kulingana na viwango vya Kimataifa

**Matokeo ya Kati:** Kuimarika kwa usimamizi na utekelezaji wa sheria za kutokomeza ukeketaji

---

- Kufanya kampeni za kutokomeza ukeketaji.
- Kuwashirikisha viongozi wa dini na wa kimila
- Kuhamasisha wanaume na wavulana kuwa vinara
- Kuwajengea uwezo wanawake na watoto wa kike vinara
- Kuwawezesha kiuchumi ngariba na manusura.

**Matokeo ya Awali:**
- Kuongezeka kwa idadi ya wanajamii wanaofikiwa nae limu ya kutokomeza ukeketaji
- Kuongezeka idadi ya ngariba na manusura wana osjhiriki shughuli mbadala za kiuchumi

**Matokeo ya Kati:** Kuongezeka kwa wanajamii katika Mikoa ya kipaumbele wanaoamini kuwa ukeketaji unapaswa kutokomezwa

---

- Kuanzisha na kuimarisha mitandao ya msaada kwa manusura
- Kuanzisha na kuimarisha nyumba salama, vituo jumuishi na huduma mkoba
- Kuimarisha rufaa na utoaji huduma
- Kufanya mapitio ya mitaala ya Afya, Elimu na elimu isiyo rasmi.

**Matokeo ya Awali:**
- Kuongezeka kwa idadi ya huduma jumuishi za kuzuia, kutoa taarifa na mwitikio kwa manusura katika mikoa ya kipaumbele

**Matokeo ya Kati:** Kuongezeka kwa wanawake na watoto wa kike wanaotumia huduma za kuzuia, utoaji taarifa na mwitikio

---

- Kutoa mafunzo kwa Kikundi Kazi cha Taifa cha kutokomeza ukeketaji.
- Kutoa mafunzo ya uratibu kwa Mkoa 13, Halmashauri 26, Kata 52 na Vijiji/Mitaa 104.
- Kuandaa na kutekeleza mkakati wa uhamasishaji wa rasilimali kwa ajili ya kutokomeza ukeketaji.
- Kuwezesha Wizara za Kisekta na Mikoa 13 kujumuisha afua za ukeketaji katika mipango na bajeti

**Matokeo ya Awali:**
- Kuongezeka kwa taasisi zinazoshiriki na kutoa taarifa za utekelezaji kwenye Kikundi Kazi cha Taifa
- Kuongezeka kwa idadi ya rasilimali fedha na ufundi kutoka bajeti ya Serikali na mchango wa Wadau

**Matokeo ya Kati:** Kuimarika kwa uratibu, ushirikiano wa kisekta na uhamasishaji wa rasilimali fedha

---

- Kufanya tafiti za kusaidia kutokomeza ukeketaji.
- Kuandaa mfumo rafiki na kutoa mafunzo kwa Kamati tendaji na Mikoa 13 ya ukusanyaji na uchakataji wa takwimu.
- Kuendesha jukwaa la Wadau wa Utekelezaji la Kitaifa la mwaka
- Kufanya tathmini za kati na za mwisho

**Matokeo ya Awali:**
- Uwepo wa tafiti kwa ajili ya programu za kutokomeza ukeketaji
- Idadi ya Wajumbe wa Kamati Tendaji waliojengewa uwezo uwezo wa Ufuatiliaji, Tathmini na Ujifunzaji
- Kufanyika kwa jukwaa la Kitaifa la kila mwaka

**Matokeo ya Kati:** Kuimarika kwa mifumo ya tafiti, ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji

---

**Matokeo ya Muda Mrefu:** Kupungua kwa kiwango cha ukeketaji nchini kwa 50%, kutoka 8% mwaka 2024/2025 hadi 4% ifikapo mwaka 2029/30

**Dira:** Kuwa Taifa ambalo wanawake na watoto wa kike wanaishi bila vitendo vya ukeketaji.

**Ufuatiliaji, tathmini na Ujifunzaji** | **Tathmini ya Kati na ya Mwisho ya Utekelezaji** | **Tathmini ya Athari**

Matokeo haya yatapelekea kuwepo kwa matokeo ya kati, yanayojumuisha mabadiliko ya mitazamo ya jamii dhidi ya ukeketaji, kuongezeka kwa matumizi ya huduma za ulinzi na msaada, pamoja na utekelezaji madhubuti wa sheria. Hatimaye, mnyororo huu wa mabadiliko utasababisha kuwepo kwa matokeo ya muda mrefu (athari) ambayo ni kupungua kwa kiwango cha ukeketaji nchini, kufikia lengo la kupunguza kwa asilimia 50 ndani ya kipindi kilichopangwa na kuchangia kufikia dira ya Mkakati huu. Mchakato huu wote unajengwa katika mifumo imara ya ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji, inayohakikisha kuwa utekelezaji unazingatia takwimu, tafiti, unarekebishwa inapobidi na unaleta matokeo endelevu yanayozingatia haki za binadamu na usawa wa kijinsia. Shughuli hizi zinajadiliwa kwa kina katika Mkakati huu.

# 5




Ulinzi wa mtoto wa kike ni jukumu la kila mmoja wetu

# SURA YA TANO: UTEKELEZAJI, URATIBU, UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MKAKATI

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza mipango ya kiutendaji, muundo wa uongozi na mifumo ya usimamizi inayohakikisha ushiriki wa wadau wote, ikijengwa juu ya uzoefu wa mkakati uliopita. Inasisitiza utekelezaji wa kimfumo, ufuatiliaji endelevu na maboresho yanayotokana na tafiti na maoni ya jamii, huku ikizingatia masuala ya kiutamaduni ya ukeketaji. Aidha, inaweka msingi wa mfumo jumuishi wa ufuatiliaji, tathmini, ujifunzaji na maboresho unaotumia takwimu, mapitio ya mara kwa mara na ushirikishwaji wa jamii ili kuimarisha uwajibikaji na ufanisi. Kwa ujumla, sura hii inaongoza utekelezaji madhubuti wa mkakati na kuweka mazingira wezeshi ya kufikia Tanzania isiyo na ukeketaji ifikapo mwaka 2030.

## 5.2 Mipangilio na Mikakati ya Utekelezaji

### 5.2.1 Uratibu wa Jumla wa Mkakati

Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum itaratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30. Katika jukumu la uratibu, Wizara itatoa mwelekeo wa kisera, itasimamia utekelezaji wa kimkakati na kuhakikisha utekelezaji unaunganisha jitihada za sekta mbalimbali na wadau wote wanaohusika na malengo ya mkakati.

Uratibu wa Wizara utakuwa mhimili wa kujenga mwitikio wa kitaifa ulio mmoja, kupunguza kurudia afua na kuimarisha mifumo ya uwajibikaji wa pamoja. Ili kuwezesha uratibu wenye ufanisi, Wizara itaweka mifumo madhubuti ya mawasiliano na ushirikiano wa kisekta, ikijumuisha mikutano ya Kitaifa ya mara kwa mara, vikundi kazi maalum na majukwaa rasmi ya kubadilishana taarifa, kupanga kwa pamoja na kutatua changamoto.

Mifumo hii itawahusisha wadau wote wa utekelezaji wa mkakati, ikiwemo Wizara, Idara na Taasisi za serikali, Asasi za Kiraia na wadau wa maendeleo, kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji unaoratibiwa na unaolenga matokeo. Ushirikishwaji huu uliopangwa utawezesha matumizi bora ya rasilimali, kuimarisha afua na kuwezesha maoni ya pamoja kwa changamoto zinazoibuka. Kupitia uratibu huu wa kimkakati na wa pamoja, lengo kuu la mkakati la kutokomeza ukeketaji nchini Tanzania litapata msukumo madhubuti wa utekelezaji.

### 5.2.2 Mfumo ulioandaliwa kwa ajili ya mgawanyo wa madaraka na utekelezaji wa mkakati kulingana na mazingira halisi

Mkakati huu unatumia mfumo uliopangwa kwa ajili ya ugatuzi wa madaraka na uzingatiaji wa mazingira halisi, ukigundua kuwa afua madhubuti za kutokomeza ukeketaji lazima ziendane na hali halisi ya kijamii, kiutamaduni, kiuchumi na kijiografia ya jamii mbalimbali nchini. Mkakati unasisitiza uwezeshaji wa mamlaka za ngazi za jamii kuongoza na kuhuisha ajenda ya kitaifa, kuhakikisha kuwa afua zinazoanzishwa zinagusa mahitaji muhimu kulingana na tamaduni husika.

Mfumo huu wa mgawanyo wa majukumu utatekelezwa kupitia taratibu zifuatazo:

**a) Mipango ya Ngazi ya Mikoa na Halmashauri:**

Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya zitahamasishwa na kupewa msaada wa kiufundi kuandaa mipango ya hatua ya kutokomeza ukeketaji kulingana na mazingira yao. Mipango hii haitaishia tu kuakisi mkakati wa kitaifa, bali itaunganisha jitihada za kuzuia na kukabiliana na ukeketaji katika mifumo iliyopo ya serikali za mitaa, mipango ya maendeleo ya mwaka na bajeti. Hii inahakikisha kuwa afua za ukeketaji zinakuwa sehemu ya utawala wa ndani na utoaji wa huduma badala ya kuwa miradi inayojitegemea na hivyo kuimarisha umiliki na uendelevu. Mipango hiyo ya

ndani itaongozwa na takwimu za kiwango cha ukeketaji za mkoa au wilaya husika, mila na desturi na rasilimali zilizopo.

**b) Ushirikishwaji wa Jamii kuendana na mazingira:**

Mkakati unasisitiza kukuza mipango inayoongozwa na jamii yenyewe, ambapo wadau wa ndani ikiwa ni pamoja na viongozi wa mila, viongozi wa dini, makundi ya wanawake, vijana na wanaume wanabainisha vyanzo vya ukeketaji na kubuni mbinu za kutatua kwa pamoja. Hii inahusisha kulinganisha mbinu bora za Kimataifa na za Kitaifa ili kukidhi mahitaji mahususi ya jamii, kanuni za kitamaduni na mienendo ya jamii. Kwa mfano, mikakati ya mawasiliano itatumia lugha za asili na njia za kitamaduni zinazokubalika. Aidha, afua zinaweza kujumuisha sherehe za kimila au majadiliano ya kijamii ili kukuza mila mbadala za kuvusha rika au kupinga mila na desturi vyenye madhara ndani ya jamii.

**c) Uimarishaji wa Uwezo katika Ngazi ya Jamii:**

Nguzo muhimu ya mgawanyo wa madaraka ni kuimarisha uwezo wa kitaasisi na rasilimali watu katika ngazi za jamii. Hii itatekelezwa kupitia mafunzo, ufuatiliaji wa karibu na msaada wa kiufundi endelevu kwa mamlaka za Serikali za Mitaa, Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, watoa huduma za Afya, Maafisa Ustawi wa Jamii, vyombo vya ulinzi na usalama, walimu, pamoja na Asasi za Kiraia za ngazi ya jamii. Lengo ni kuwajengea uwezo wa kutekeleza, kufuatilia na kutoa taarifa kuhusu afua za kutokomeza ukeketaji kwa ufanisi.


## 5.3 Muundo wa Uratibu na Majukumu

Muundo wa uratibu na mgawanyo wa majukumu katika utekelezaji wa Mkakati huu unaakisiwa katika Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA Toleo la Pili), kama inavyooneshwa katika mchoro Hapa chini. Kwa uelewa wa kina zaidi kuhusu mgawanyo wa majukumu, mifumo ya uwajibikaji na taratibu za utekelezaji, inapendekezwa pia kurejea MTAKUWWA Toleo la Pili.

## 5.4 Ushirikiano wa Kisekta: Mikakati ya Ushirikishwaji wa Wadau

Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30 unasisitiza umuhimu wa ushirikiano thabiti wa kisekta na ushirikishwaji jumuishi wa wadau kama nguzo kuu za utekelezaji wenye ufanisi. Afua za Mkakati huu zinatekelezwa na wadau mbali mbali kwa uratibu na ushirikiano katika kufikia matokeo yanayotarajiwa. Wadau hawa na majukumu yao yameainishwa katika jedwali hapa chini.

***Muundo wa Uratibu***



**Jedwali Na. 6: Majukumu na Wajibu wa Wadau**

| S/N | Jina la Mdau | Maelezo ya Majukumu na Wajibu |
|---|---|---|
| 1. | Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) | i. Kuratibu wizara za kisekta zinazohusika katika utekelezaji wa Mkakati |
| 2. | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum | i. Kufanya mapitio ya sera<br>ii. Kuandaa miongozo ya utekelezaji<br>iii. Kutenga bajeti kwa utekelezaji wa afua za ukeketaji<br>iv. Kuimarisha usimamizi wa mifumo ya takwimu<br>v. Kuratibu utekelezaji<br>vi Kuratibu mikutano na vikao vya utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini<br>vii. Kuratibu kampeni za uelimishaji dhidi ya ukeketaji<br>vii. Kuratibu utoaji wa huduma jumuishi za kuzuia, utoaji wa taarifa na mwitikio kwa manusura wa ukeketaji |
| 3. | Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | i. Kuwezesha ujumuishaji wa afua za ukeketaji katika mipango na bajeti za mikoa na serikali za mitaa<br>ii. Kuimarisha mifumo ya utoaji wa taarifa na mawasiliano kutoka ngazi za jamii hadi ngazi ya taifa<br>iii. Kuwasilisha taarifa zilizojumuishwa za utekelezaji katika ngazi ya Serikali za Mitaa kuhusu utokomezaji wa ukeketaji kwa wizara husika<br>iv. Kuratibu wadau katika serikali za mitaa kutekeleza afua za kuzuia na kukabiliana na ukeketaji<br>v. Kufanya ziara za pamoja za usimamizi shirikishi, ufuatiliaji na tathmini katika ngazi ya Serikali za Mitaa |
| 4. | Wizara ya Afya | i. Kuandaa miongozo, taratibu za uendeshaji (SOPs) na nyenzo za mafunzo kwa wahudumu wa afya ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora za afya kwa manusura<br>ii. Kujenga uwezo wa wahudumu wa afya kutoa huduma za kinga, usimamizi jumuishi na mwitikio kwa manusura<br>iii. Kukusanya, kuchambua na kutoa taarifa na takwimu za manusura waliopata huduma<br>iv. Kuandaa na kusambaza zana za ufuatiliaji na tathmini za ukatili dhidi ya wanawake na watoto |
| 5. | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia | i. Kusimamia ubora wa huduma za ustawi na usalama wa mtoto wa kike ndani ya shule<br>ii. Kutoa waraka na miongozo ya ushauri nasaha na elimu ya kuzuia na ulinzi wa mtoto<br>iii. Kuboresha mitaala ya elimu inayojumuisha masuala ya ukeketaji |
| 6. | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi | i. Kuratibu usimamizi na utekelezaji wa sheria dhidi ya ukeketaji<br>ii. Kuandaa na kuboresha miongozi ya usimamizi wa mashauri ya ukeketaji |

| S/N | Jina la Mdau | Maelezo ya Majukumu na Wajibu |
|---|---|---|
| | | iii. Kuratibu kampeni za elimu ya kutokomeza ukeketaji<br>iii. Kuimarisha uwezo wa taasisi za kusimamia na kutekeleza Sheria zinazokataza ukeketaji<br>iv. Kuboresha ufanisi wa Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi |
| 7. | Inspekta Jenerali wa Polisi | i. Ushirikishwaji wa jamii kupitia uhamasishaji, Vitengo vya Huduma za Nje na polisi jamii<br>ii. Utekelezaji wa sheria ikiwemo kukamata, kuchunguza na kufikisha mashitaka ya watuhumiwa wa ukeketaji<br>iii. Mafunzo na kujenga uwezo wa askari kuhusu jinsia na ulinzi wa mtoto<br>iv. Kuandaa na kuratibu mikakati ya kipolisi dhidi ya ukeketaji<br>v. Kuimarisha mifumo ya utoaji wa taarifa na uokoaji |
| 8. | Idara ya Uhamiaji Tanzania | i. Kuzuia ukeketaji wa kuvuka mipaka<br>ii. Kupambana na biashara haramu ya binadamu na watoto<br>iii. Kukuza uelewa kupitia programu ya jamii ya "Mjue Jirani Yako" |
| 9. | Wizara ya Katiba na Sheria | i. Uandaaji na Maboresho ya Sheria zinazokataza ukeketaji<br>ii. Kuandaa miongozo na kanuni za utekelezaji wa Sheria zinazokataza ukeketaji |
| 10. | Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo | i. Kufanya mapitio ya kisera (Sera ya Taifa ya Utamaduni) ili kujumuisha afua za kukabiliana na mila na desturi zenye madhara husussan utekelezaji<br>ii. Kuhamaisha ushiriki wa viongozi wa kimila ili kutokomeza vitendo vya ukeketaji<br>iii. Kujumuisha afua za kukabiliana na ukeketaji kama kipimo cha utendaji (KPI) wa Maafisa Utamaduni katika maeneo yenye mila na desturi zisizofaa ikiwemo ukeketaji<br>iv. Kuhamasisha ushiriki wa wadau kuwekeza katika tafiti zinazohusu mila na desturi zenye madhara zikiwemo ukeketaji<br>vi. Kuratibu na kuandaa afua za utoaji elimu na hamasa ya mabadiliko katika jamii zinazoishi mila nadesturi zenye madhara ikiwemo ukeketaji |
| 11. | Wadau wa Maendeleo wa Kimataifa | i. Washirika katika ushirikiano wa kisekta<br>ii. Kutoa ufadhili wa kifedha<br>iii. Kutoa ushauri wa kiufundi<br>iii. Kuratibu kubadilishana uzoefu wa kimataifa na kukuza ujifunzaji wa pamoja |
| 12. | Asasi za Kiraia, Taasisi za Kidini na Asasi za Kijamii. | i. Kutekeleza afua zenye kuzingatia muktadha wa kiutamaduni za kutokomeza ukeketaji<br>ii. Kuhamasisha jamii kutumia Mila mbadala za kuvusha rika |

| S/N | Jina la Mdau | Maelezo ya Majukumu na Wajibu |
|---|---|---|
| | | iii. Kufanya kampeni za kukuza uelewa na kubadilisha mitazamo hasi ya kijamii<br>iv. Kutoa huduma za moja kwa moja kwa manusura na walio katika hatari<br>v. Kufanya utetezi na ushawishi wa maboresho ya Sera na Sheria |
| 12. | Taasisi za Kitaaluma na Utafiti | i. Kufanya tafiti<br>ii. Utoaji wa mafunzo<br>iii. Kushauri maboresho ya mitaala kulingana na tafiti |
| 13. | Sekta Binafsi | i. Kuchangia rasimali fedha kupitia uwajibikaji wa kijamii wa makampuni<br>ii. Kuandaa na kusambaza teknolojia bunifu zinazosaidia katika kampeni, ukusanyaji na usambazaji wa taarifa<br>iii. Kushiriki katika kampeni za uelimishaji jamii za kutokomeza ukeketaji |
| 14. | Vyombo vya Habari na mitandao ya Kijamii | i. Kurusha kampeni na matangazo ya kutokomeza ukeketaji<br>ii. Kuelimisha umma madhara ya ukeketaji na Sheria husika<br>ii. Kuwezesha mijadala chanya ya umma ya kutokomeza ukeketaji |
| 15. | Jamii | i. Kutoa ulinzi kwa watoto wa kike dhidi ya ukeketaji<br>ii. Kuimarisha mifumo ya kijamii ya kuzuia ukeketaji, utoaji wa taarifa na mwitikio<br>ii. Kushiriki katika kuelimishana katika ngazi ya kaya na jamii kuhusu madhara ya ukeketaji |
| 16. | Wazee wa Mila na Viongozi wa Koo | i. Kufanya ushawishi wa kutokomeza ukeketaji katika mila za kijamii |
| 17. | Wazazi na Walezi | i. Kutoa malezi chanya yanayolinda haki na ustawi wa watoto wa kike na wa kiume<br>ii. Kuzuia watoto wao wa kike kwenda keketwe<br>iii. Kutoa taarifa za viashiria na matukio ya vitendo vya ukeketaji<br>iv. Kuwa vinara wa mabadiliko ya mila zenye madhara kwenye jamii |
| 18. | Watoto na Vijana wa Kike na wa Kiume | i. Kutoa taarifa za viashiria na matukio ya vitendo vya ukeketaji<br>ii. Kuwa vinara wa mabadiliko wa mila zenye madhara kwenye jamii kwa kukataa ukeketaji<br>iii. Kutoa elimu za kuzuia ukeketaji kupitia makundi rika |

## 5.5 Rasilimali Fedha za Mkakati

Utekelezaji wenye mafanikio na endelevu wa Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2025/26–2029/30 unategemea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa rasilimali za fedha za kutosha na halisia. Kwa kutambua vyanzo mbali mbali vya ukeketaji na wigo mpana wa afua zinazohitajika, Mkakati huu unatumia mfumo jumuishi wa ufadhili unaolenga kubainisha na kuendeleza vyanzo mbalimbali vya fedha pamoja na kuhakikisha mgawanyiko mzuri wa rasilimali katika ngazi zote za utekelezaji. Mbinu hii inajiondoa katika utegemezi wa chanzo kimoja cha fedha na badala yake inaweka msingi imara na endelevu wa kifedha unaoweza kuendeleza jitihada za kutokomeza ukeketaji katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mkakati na baada ya mkakati.

### 5.5.1 Dhamira ya Bajeti ya Serikali:

Chanzo cha rasilimali fedha ni kutengwa kwa rasilimali za kutosha kutoka katika Bajeti ya Serikali. Dhamira hii inaakisi umiliki wa kitaifa na dhamira ya kisiasa ya kutokomeza ukeketaji. Fedha zitaelekezwa kupitia Wizara, Idara na Taasisi husika, kuhakikisha kuwa shughuli zinazohusiana na ukeketaji zinajumuishwa katika bajeti za kila mwaka za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Rasilimali hizi zitasaidia mifumo ya uratibu, ujenzi wa uwezo, huduma kwa manusura na programu za ushirikishwaji wa jamii. Ujumuishaji wa rasilimali za ukeketaji katika majukumu ya msingi ya sekta ya umma unahakikisha uendelevu wa muda mrefu na kuhalalisha afua hizi ndani ya mifumo ya kitaasisi.

### 5.5.2 Ushirikiano na Wadau wa Maendeleo wa Kimataifa:

Mkakati unasisitiza umuhimu wa kuhamasisha rasilimali kutoka kwa wadau mbalimbali wa kimataifa, wakiwemo mashirika ya Umoja wa Mataifa, wafadhili na taasisi za kimataifa. Wadau hawa hutoa msaada wa kifedha na wa kiufundi. Ushirikiano utaelekezwa katika kulinganisha misaada ya wafadhili na vipaumbele vya Mkakati, kuratibu vyanzo vya fedha na kupunguza kurudia kwa afua. Mbinu bunifu za ufadhili na mifuko ya kimataifa inayolenga usawa wa kijinsia na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa kike itatumika kuongeza matokeo chanya.

### 5.5.3 Uhamasishaji wa Rasilimali za Ndani:

Asasi za kiraia katika ngazi ya kitaifa na kijamii ni vichocheo muhimu vya uhamasishaji wa rasilimali za ndani. Mkakati unahamasisha upatikanaji wa misaada kutoka kwa taasisi za ufadhili wa kifedha, wafadhili binafsi na michango ya umma. Sekta binafsi pia inahimizwa kuchangia kupitia uwajibikaji wa kijamii wa makampuni, ushirikiano wa kimkakati na uwekezaji wa moja kwa moja katika jitihada za kutokomeza ukeketaji, ikiwemo msaada wa miundombinu kama ujenzi wa Vituo vya Huduma Jumuishi na nyumba salama. Uchangishaji wa fedha unaotegemea jamii utaimarisha umiliki wa kijamii na ushiriki endelevu.

### 5.5.4 Usimamizi wa Fedha kwa Uwazi:

Mfumo wa rasilimali fedha unaweka kipaumbele kwa uwazi, uwajibikaji na ufanisi. Hii inajumuisha miongozo na uwazi wa bajeti, mifumo thabiti ya utoaji wa taarifa za fedha, ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara ya matumizi, pamoja na kujenga uwezo wa wadau wanaotekeleza usimamizi wa fedha. Hatua hizi zinalenga kupunguza matumizi yasiyo sahihi ya rasilimali, kuhakikisha matumizi bora ya fedha na kujenga imani miongoni mwa wadau na wafadhili, hivyo kuchochea uwekezaji endelevu.

### 5.5.5 Mfumo Endelevu wa Rasilimali:

Kwa ujumla, mkakati huu wa ufadhili haulengi tu kupata fedha bali kuweka na kuimarisha mfumo endelevu wa upatikanaji wa rasilimali. Kwa kuunganisha uongozi wa Serikali, ushirikiano wa kimataifa, ushirikiano wa ndani na usimamizi madhubuti wa fedha. Mkakati unahakikisha kuwa kila afua iliyopangwa ina rasilimali za kutosha ili kuweka msingi wa kutokomeza ukeketaji wa kudumu na kulinda haki na ustawi wa wanawake na watoto wa kike nchini.

## 5.6 Mpango jumuishi wa kujenga uwezo wa rasilimali watu

Utekelezaji madhubuti wa Mkakati huu unategemea uwepo wa rasilimali watu wenye uwezo, waliopata mafunzo stahiki na wanaoungwa mkono ipasavyo katika ngazi zote. Kwa kutambua kuwa mafanikio ya mkakati wowote yanategemea uwezo wa wale wanaoutekeleza, Mkakati huu unaweka mkazo mkubwa katika mpango jumuishi wa kujenga uwezo wa rasilimali watu. Mpango huu unalenga kuhakikisha kuwa wadau wote kuanzia watunga sera wa kitaifa hadi watendaji wa ngazi za msingi wanakuwa na maarifa, ujuzi na mitazamo inayohitajika ili kuzuia ukeketaji, kulinda wasichana walio katika hatari ya kukeketwa na kusaidia manusura. Mpango huu hauishii kwenye mafunzo pekee bali unajumuisha maendeleo endelevu ya kitaaluma, uratibu na uandaaji wa mazingira wezeshi ya utendaji yenye kuchochea dhamira na ufanisi katika kutokomeza ukeketaji.

Sehemu muhimu ya mpango huu ni mafunzo lengwa na programu za uhamasishaji zinazolenga mahitaji tofauti ya makundi ya kitaaluma na wadau wa kijamii. Kwa maafisa wa Serikali katika ngazi ya kitaifa, kikanda na wilaya, mafunzo yanajumuisha utungaji wa sera, upangaji wa programu, upangaji bajeti kwa afua za ukeketaji na uratibu madhubuti wa ushirikiano wa kisekta. Kwa watoa huduma kama Wahudumu wa Afya, Afisa Ustawi wa Jamii, Walimu na Vyombo vya Dola, mafunzo yatazingatia utambuzi wa kesi za ukeketaji, utoaji wa huduma zinazomlenga manusura, taratibu za kisheria, masuala ya maadili na mawasiliano yanayozingatia muktadha wa kitamaduni. Wadau wa ngazi ya jamii, wakiwemo Viongozi wa Kimila na Kidini, Wahudumu wa Afya ya Jamii na Wajumbe wa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto watapatiwa mafunzo ya uhamasishaji wa jamii, mawasiliano ya mabadiliko ya tabia, mbinu mbadala za mila za kuvusha rika na njia bora za rufaa ili waweze kuendesha mabadiliko kutoka ndani ya jamii zao.

Zaidi ya mafunzo rasmi, Mpango wa Kujenga Uwezo unajumuisha mikakati ya ujifunzaji endelevu, kubadilishana maarifa na msaada wa rika kwa rika. Hii inahusisha uanzishaji wa majukwaa ya kubadilishana uzoefu mara kwa mara kati ya watekelezaji wa sekta na ngazi mbalimbali, ziara za mafunzo katika maeneo yenye mafanikio na uandaaji wa nyenzo na vifaa vya rejea vinavyopatikana kwa urahisi. Programu za malezi ya kitaaluma zitaunganisha wataalamu waliobobea na viongozi chipukizi katika harakati za kutokomeza ukeketaji, ili kurahisisha uhamishaji wa kubadilishana uzoefu wa taasisi na ujuzi. Aidha, mpango unahimiza ujumuishaji wa maudhui ya kuzuia na mwitikio wa ukeketaji katika mitaala ya taasisi za mafunzo ya kitaaluma kama vyuo vya tiba, uuguzi na ustawi wa jamii ili vizazi vijavyo vya wataalamu viwe na ujuzi.

## 5.7 Mpango Wa Usimamizi wa Takwimu, Taarifa na Mawasiliano

Kutokomeza ukeketaji kwa ufanisi kunategemea afua zilizoundwa vizuri na uwepo wa Mpango madhubuti na unaobadilika wa utunzajai wa takwimu, taarifa na mawasiliano. Kama sehemu ya Mkakati huu, mpango wa usimamizi ni nguzo ya kuhakikisha kuwa maamuzi yote kuanzia utungaji wa sera hadi utekelezaji katika ngazi za jamii yanazingatia ushahidi na yanajibu mahitaji. Mpango unaeleza mbinu ya kimfumo ya ukusanyaji, uchambuzi, usambazaji na matumizi ya takwimu zinazohusiana na ukeketaji na hivyo kuchagiza utoaji taarifa endelevu kwa ajili ya kuboresha afua za kimkakati. Mtiririko mzuri wa taarifa ni muhimu katika kufuatilia maendeleo, kubaini changamoto mpya na mafanikio, hivyo kuimarisha uwajibikaji na kuongeza ufanisi wa Mkakati.

Chanzo cha mpango huu ni kuwa na mfumo jumuishi wa ukusanyaji wa takwimu unaokusanya taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu viwango vya ukeketaji, mienendo na ufanisi wa afua. Hii inajumuisha kutumia mifumo iliyopo ya kitaifa kama TDHS na Utafiti kuhusu Ukatili dhidi ya Watoto Tanzania, pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa takwimu katika ngazi za kitaifa na jamii. Vyanzo muhimu vitajumuisha mifumo ya taarifa za Afya, rejista za Ustawi wa amii, kumbukumbu zaPolisi, Elimu, Mahakama na mipango ya ufuatiliaji wa kijamii. Mkazo utawekwa katika uchambuzi wa takwimu kwa kuzingatia umri, jinsia, eneo na sifa nyingine muhimu ili kuhakikisha makundi yaliyo katika mazingira hatarishi yanawakilishwa ipasavyo. Aidha, ukusanyaji wa takwimu za ubora utaendelezwa ili kubaini

vichocheo vya msingi vya ukeketaji, mitazamo ya jamii na mienendo ya mabadiliko ya kanuni za kijamii na hivyo kukamilisha takwimu na taarifa sahihi.

Mpango wa mawasiliano utatekelezwa ili kuongeza uelewa wa jamii kuhusu madhara ya ukeketaji, kuimarisha kanuni chanya za kijamii na kusambaza visa vya mafanikio. Hii itahusisha matumizi ya vyombo mbalimbali vya habari, programu za uhamasishaji wa jamii na kampeni za utetezi wa umma ili kuchochea mjadala wa kitaifa na kudumisha dhamira ya muda mrefu ya kutokomeza ukeketaji nchini.

## 5.8 Ufuatiliaji, tathmini, ujifunzaji na uboreshaji

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati huu utakuwa mchakato endelevu na uliopangwa, unaolenga kuhakikisha kuwa afua zote zinatekelezwa kwa wakati, rasilimali zinatumika kwa ufanisi na matokeo yanalingana na malengo ya kimkakati na shabaha za kitaifa. Wizara yenye dhamana ya Wanawake na Watoto wa Kike katika jukumu lake la uratibu, itashirikiana na wizara za Kisekta, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi za Kiraia kuendesha mfumo jumuishi wa ufuatiliaji.

Mafanikio na uwezo wa Mkakati huu unategemea kwa kiasi kikubwa uwepo wa mfumo madhubuti na endelevu wa Ufuatiliaji, Tathmini, Ujifunzaji na Uboreshaji. Mfumo huu hauishii katika uwajibikaji bali hutumika kama chombo hai cha usimamizi wa kimkakati, kinachokuza utamaduni wa maamuzi yanayoongozwa na tafiti na takwimu na kuhakikisha afua zinaendelea kuwa sahihi na zenye matokeo katika mazingira yanayobadilika. Kupitia ufuatiliaji wa maendeleo, tathmini ya ufanisi, ukusanyaji wa mafunzo na marekebisho ya mapema, Mkakati unalenga kuongeza uwezekano wa kufikia lengo la kutokomeza ukeketaji nchini.

### 5.8.1 Mbinu za Ufuatiliaji

Mbinu za ufuatiliaji ndani ya Mkakati zimeundwa kama mchakato endelevu na wenye mabadiliko, unaolenga kufuatilia maendeleo ya utekelezaji, kubaini changamoto mpya na kutoa mrejesho wa kila siku au wa kila mwezi kwa ajili ya usimamizi unaobadilika. Mbinu hii inahakikisha usimamizi wa kina kuanzia ngazi ya kitaifa hadi ngazi za msingi, ikiwemo Serikali za Mitaa. Lengo kuu ni kuhakikisha afua zinaendelea kwa mwelekeo sahihi, matumizi bora ya rasilimali na mwitikio unaoendana na muktadha unaobadilika wa kutokomeza ukeketaji nchini.

Shughuli mahsusi za ufuatiliaji zitajumuisha tathmini, mapitio shirikishi na ukusanyaji wa takwimu wa kimfumo. Ufuatiliaji wa kila robo mwaka kwa mamlaka husika na kamati za kiufundi katika maeneo ya utekelezaji na jamii zitawezesha mawasiliano ya moja kwa moja kwa watekelezaji na wanufaika. Mikutano ya mapitio ya robo mwaka na ya mwaka katika ngazi ya kitaifa, kikanda na wilaya itawakutanisha wadau wakuu kuchambua taarifa za maendeleo, kujadili changamoto na kupanga hatua za marekebisho kwa pamoja. Mfumo madhubuti wa utoaji wa taarifa utaunganishwa katika mfumo uliopo wa usimamizi wa mashauri, kuhakikisha mtiririko wa takwimu na taarifa za simulizi kutoka ngazi za chini (kijiji/mtaa) hadi ngazi za juu za uratibu (Wilaya, Mkoa na Taifa) na kutoa taswira kamili ya utekelezaji na masuala yanayoibuka.

Ili kuimarisha ufanisi na uchambuzi, Mkakati utatumia zana na teknolojia za kisasa za ukusanyaji na usimamizi wa takwimu. Mfumo wa ufuatiliaji wa jamii utaimarishwa ili kuwezesha ukusanyaji wa taarifa kwa wakati. Programu za ukusanyaji wa takwimu kwa njia ya simu zitatumika ili kuongeza ubora na kasi ya ukusanyaji taarifa. Dashibodi jumuishi ya mtandaoni itaonesha viashiria muhimu vya utendaji vinavyohusiana na viwango vya ukeketaji, maarifa, mitazamo, matumizi ya huduma na utekelezaji wa sera. Takwimu zilizochanganuliwa kwa makundi mbalimbali zitafuatiliwa kwa makini ili kubaini tofauti na kuelekeza afua lengwa. Mbinu hii ya ufuatiliaji inayotegemea tafiti na takwimu inawezesha maamuzi sahihi, kubaini mafanikio yanayoweza kuigwa na kushughulikia changamoto kwa wakati.

**Jedwali Na. 7: Vipengele Muhimu vya Mbinu za Ufuatiliaji**

| Mbinu ya Ufuatiliaji | Maelezo | Mzunguko | Wahusika Wakuu | Lengo |
|---|---|---|---|---|
| Ziara | Uchunguzi wa moja kwa moja na ushiriki katika maeneo ya utekelezaji wa afua. | Mwezi/robo mwaka | Timu za Taifa, Mkoa, Wilaya na Asasi za Kiraia | Kuthibitisha utekelezaji wa shughuli, kubaini changamoto za ngazi ya utekelezaji na kukusanya taarifa za ubora. |
| Mikutano ya Mapitio | Majadiliano yaliyoandaliwa kuhusu taarifa za maendeleo na changamoto. | Robo mwaka na mwaka | Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Programu, Kamati ya Kitaifa ya Kiufundi, Kamati za Halmashauri, Vikundi Kazi vya Kiufundi. | Kuchambua utendaji, kuwezesha utatuzi wa changamoto kwa pamoja na kutoa taarifa za usimamizi unaobadilika. |
| Mfumo wa Utoaji Taarifa | Uwasilishaji wa taarifa za takwimu na simulizi kwa utaratibu. | Mwezi, robo mwaka na mwaka | Ngazi za Kijiji/Mtaa, Kata, Wilaya na Mkoa; Wizara, Idara na Taasisi za Serikali; Wanachama wa mitandao ya Asasi za Kiraia | Kufuatilia maendeleo dhidi ya Viashiria Muhimu vya Utendaji na kutoa takwimu kwa watoa maamuzi. |
| Zana/Teknolojia za Takwimu | Matumizi ya programu za simu na dashibodi za mtandaoni kwa takwimu za wakati halisi. | Endelevu | Wakusanyaji na watumiaji wote wa takwimu | Kuongeza usahihi wa takwimu, ufanisi, upatikanaji wa taarifa na uchambuzi kwa wakati. |
| Takwimu Zilizochanganuliwa kwa Makundi | Ukusanyaji wa takwimu zilizogawanywa kwa umri, jinsia, eneo na vigezo vingine. | Endelevu | Wakusanyaji wote wa takwimu | Kubaini tofauti na mapungufu, kuhakikisha ujumuishwaji na kuongoza afua mahususi za kutokomeza ukeketaji. |

### 5.8.2 Taratibu za Tathmini

Tathmini imebuniwa kama mchakato makini na wa mara kwa mara wa kupima umuhimu, ufanisi, tija, athari na uendelevu wa afua zinazolenga kutokomeza ukeketaji. Matokeo ya tathmini ya mkakati uliopita yatatumika kama taarifa za msingi. Mfumo wa tathmini unajikita katika tathmini mbili kuu ambazo ni tathmini ya katikati ya kipindi na tathmini ya mwisho wa kipindi.

Tathmini ya katikati ya kipindi, inayofanyika takribani nusu ya kipindi cha utekelezaji wa miaka mitano ya Mkakati, itatumika kama hatua muhimu ya kimkakati ya kupima mwelekeo wa utekelezaji. Lengo lake kuu ni kubaini kama Mkakati unaelekea kufikia malengo yake, kutambua matokeo ya awali, kubainisha maeneo yenye maendeleo makubwa, pamoja na kuonesha changamoto au vikwazo

vinavyojitokeza. Tathmini hii ya kimaendeleo itawezesha kufanya marekebisho kwa wakati muafaka, usimamizi unaobadilika, upangaji upya wa rasilimali na uboreshaji wa mbinu za utekelezaji katika kipindi kilichobaki.

Tathmini ya mwisho wa kipindi, itakayofanyika mwishoni mwa utekelezaji wa Mkakati, itatoa tathmini ya kina na ya jumla kuhusu utendaji na mchango wa Mkakati katika juhudi za kitaifa za kuachana na ukeketaji. Tathmini hii itapima kiwango ambacho malengo ya Mkakati yamefikiwa, athari zake kwa kiwango cha ukeketaji, maarifa, mitazamo na mienendo ya jamii, pamoja na uendelevu wa afua na jitihada za kujenga uwezo zilizotekelezwa.

Tathmini zote mbili zitatekelezwa na wataalamu huru wa tathmini ili kuhakikisha uadilifu, kutokuwa na upendeleo na uaminifu wa matokeo. Mbinu mchanganyiko zitatumika zikijumuisha takwimu ikiwemo viwango vya ukeketaji, matumizi ya huduma, mitazamo ya jamii na uzoefu wa wadau. Mbinu hii itatoa uelewa mpana na wa kina kuhusu mafanikio, changamoto na masomo yaliyopatikana.

Matokeo na mapendekezo ya tathmini yatasambazwa kwa wadau wote wa kisekta ili kuyaingiza katika uundaji wa sera, upangaji wa programu zijazo na juhudi za kukabiliana na ukatili wa kijinsia.

**Jedwali Na. 8: Vipengele Muhimu vya Taratibu za Tathmini**

| Aina ya Tathmini | Muda (makadirio) | Lengo Kuu | Maeneo ya Kuzingatiwa | Watekelezaji | Matokeo/Matumizi |
|---|---|---|---|---|---|
| Tathmini ya Katikati ya Kipindi | Katikati ya utekelezaji wa Mkakati (Miaka miwili na miezi sita) | Kimaendeleo: Kupima maendeleo ya awali, kubaini changamoto na kuwezesha marekebisho | Matokeo ya awali, ufanisi wa utekelezaji, umuhimu wa afua, vikwazo vinavyojitokeza, mapendekezo ya kiutendaji | Wataalamu huru wa tathmini | Mapendekezo yanayotekelezeka kwa usimamizi unaobadilika na uboreshaji wa programu kwa miaka iliyobaki |
| Tathmini ya Mwisho wa Kipindi | Mwisho wa Mkakati (Mwaka 5) | Muhtasari: Kupima kiwango cha kufikiwa kwa malengo, matokeo ya jumla na uendelevu | Utekelezaji wa malengo, athari kwa viwango vya Ukeketaji na mitazamo, ufanisi, umuhimu, uendelevu na masomo yaliyopatikana | Wataalamu huru wa tathmini | Ripoti za kina; matokeo kucahngia maboresho ya sera za baadaye, programu na uhamasishaji wa rasilimali; uwajibikaji |

### 5.8.3 Ujifunzaji na Uboreshaji wa Utekelezaji wa Mkakati

Ujifunzaji umejumuishwa kama mchakato endelevu na unaojirudia katika mzunguko wa Mkakati. Hii inahakikisha kuwa taarifa zinazopatikana kupitia ufuatiliaji na tathmini hazibaki kwenye taarifa, bali zinakusanywa kwa utaratibu, kuchambuliwa kwa kina, kusambazwa na kutumika kuboresha utekelezaji wa Mkakati. Mwelekeo huu unakuza mbinu inayobadilika na inayojifunza, badala ya utekelezaji mgumu unaozingatia mpango wa awali bila kuzingatia mabadiliko ya mazingira.

Mkakati utaendelea kuimarisha mifumo ya ujifunzaji kupitia mikutano ya mara kwa mara ya kujifunza katika ngazi za Taifa, Mkoa na Wilaya. Mikutano hii itawawezesha watekelezaji, washirika na wanufaika kuchambua taarifa za ufuatiliaji, kujadili matokeo ya tathmini na kubadilishana uzoefu. Ziara za kujifunza baina ya wadau na maeneo yenye mafanikio zitahamasishwa ili kuruhusu ujifunzaji wa moja kwa moja kutoka kwenye mbinu bora zilizothibitika.

Mkakati pia utatekeleza mfumo wa urasimishaji wa nyaraka, kuhakikisha kuwa tafiti, taarifa za mafanikio, bunifu na changamoto zinarekodiwa na kuhifadhiwa katika mifumo inayofikika kirahisi. Taarifa hizi zitatoa msingi thabiti wa uchambuzi wa kina na marekebisho ya wakati muafaka ya programu.

Lengo kuu la ujifunzaji ni kubadilisha maarifa yaliyopatikana kuwa maboresho ya utekelezaji na kusaidia kuboresha afua zijazo za kutokomeza ukeketaji. Mbinu bora na bunifu zitasambazwa kupitia majukwaa ya maarifa mtandaoni, Waraka wa Sera, taarifa za mada mahsusi na warsha lengwa, ili kuwafikia wadau wote husika.

**Jedwali Na. 9: Vipengele Muhimu vya Mchakato wa Ujifunzaji na Uboreshaji**

| Kipengele/Mfumo | Maelezo | Lengo | Muda | Matokeo |
|---|---|---|---|---|
| Matukio ya Ujifunzaji/Warsha | Majukwaa yaliyoandaliwa kwa wadau kujadili matokeo ya ufuatiliaji na tathmini, kubadilishana uzoefu na kubainisha masomo waliyojifunza. | Kuwezesha tafakuri ya pamoja, utatuzi wa changamoto na utambuzi wa mbinu bora. | Robo mwaka, mwaka na inapohitajika. | Masuala ya ujifunzaji, marekebisho yaliyokubaliwa na mitandao ya wadau iliyoimarishwa. |
| Kubadilishana uzoefu kwa makundi rika | Ziara na kubadilishana uzoefu kati ya watekelezaji kutoka maeneo tofauti. | Kukuza ujifunzaji wa pamoja kutokana na afua zilizofanikiwa na kuimarisha utatuzi wa changamoto za kiutendaji. | Kulingana na mahitaji yanapobainishwa. | Utekelezaji wa mikakati iliyothibitika, mbinu bora za utekelezaji zilizoimarishwa. |
| Kuorodhesha masuala ya ujifunzaji | Kurekodi tafiti, taarifa za mafanikio, changamoto na hatua za marekebisho zilizochukuliwa. | Kujenga hazina thabiti ya maarifa kwa ajili ya uboreshaji endelevu na rejea za baadaye. | Endelevu. | Makala, tafiti na ushawishi wa sera. |
| Mizunguko ya Mrejesho | Taratibu za kuwasilisha maarifa kutoka ufuatiliaji, tathmini na matukio ya ujifunzaji kwenda katika usanifu na | Kuhakikisha ujifunzaji unaathiri moja kwa moja marekebisho ya programu na maboresho ya kimkakati. | Endelevu. | Programu zinazoitikia mazingira, ufanisi ulioongezeka na matokeo. |

| Kipengele/Mfumo | Maelezo | Lengo | Muda | Matokeo |
|---|---|---|---|---|
| | utekelezaji wa programu. | | | |
| Usambazaji wa Maarifa | Kushirikisha maarifa yaliyorekodiwa kupitia majukwaa mbalimbali (mitandao, taarifa, vipeperushi, makala fupi za Kisera). | Kufanya masomo yafikike kwa wadau wengi zaidi na kuarifu wadau wa kitaifa na ngazi za msingi. | Kadri zinavyoandaliwa. | Maamuzi yanayotegemea ushahidi, urudufu wa mbinu zilizofanikiwa, ushahidi kwa utetezi. |

### 5.8.4 Uchambuzi wa Hatari za Kimkakati na Hatua za Kukabiliana Nazo

Uandaaji wa Mkakati ulihusisha uchambuzi wa kimkakati, uliojengwa juu ya mafunzo yaliyopatikana kutokana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mkakati ya awali. Uchambuzi huu umebaini kuwa zipo changamoto kadhaa muhimu zinazotarajiwa kuendelea kujitokeza na hivyo kuhitaji uangalizi na hatua mahsusi ili kuhakikisha ufanisi na uendelevu wa Mkakati huu mpya.

Eneo mojawapo lenye changamoto la kimkakati linahusiana na utekelezaji wa mifumo ya Kisera na Kisheria. Pamoja na kuwepo kwa mfumo imara wa kisheria unaokataza ukeketaji, utekelezaji wa sheria bado unakabiliwa na changamoto. Aidha, sera zilizopitwa na wakati, kama vile Sera ya Maendeleo ya Mtoto ambayo haijafanyiwa mapitio kwa zaidi ya miaka 15, pamoja na mianya iliyopo katika sheria, vinaendelea kudhoofisha ulinzi na utekelezaji wa sheria. Hatari nyingine inatokana na kutokuwepo kwa ulinganifu kati ya sheria za kitaifa na mifumo ya kikanda, hali inayochanganya jitihada za kukabiliana na ukeketaji wa kuvuka mipaka.

Changamoto za kijamii na kitamaduni ni eneo lingine ikiwamo uwepo wa upinzani wa kitamaduni dhidi ya kuachana na ukeketaji bado umekita mizizi katika jamii nyingi na mara nyingi huimarishwa na mifumo ya mfumo dume na ukosefu wa usawa wa kijinsia. Suala linaloibuka ni kuongezeka kwa ukeketaji wa kitabibu na ukeketaji wa kificho ambapo baadhi ya jamii huendeleza vipengele vya kimila huku zikikwepa makatazo ya kisheria, hali inayofanya kugundua na kushughulikia matukio ya ukeketaji kuwa vigumu zaidi. Mbinu za ukeketaji zinazobadilika zinahitaji mikakati inayozingatia muktadha wa kitamaduni, badala ya utekelezaji wa sheria pekee na kushughulikia kwa kina shinikizo za kijamii na mifumo ya imani. Aidha, kiwango kidogo cha uelewa na elimu kwa umma kinaendelea kuwa hatari, kwa kuwa kinaruhusu taarifa potofu na upinzani kuendelea kujengeka katika ngazi ya jamii.

Changamoto za kiutendaji na kifedha ni miongoni mwa masuala muhimu ya kuzingatia. Upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka vyanzo vya ndani na vya nje bado ni mdogo, huku afua za kutokomeza ukeketaji kutopewa kipaumbele cha kutosha katika Mipango na Bajeti za serikali. Mifumo ya kielektroniki ya takwimu isiyo na ufanisi wa kutosha kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini unawakilisha hatari ya kimkakati. Bila miundombinu imara ya takwimu, inakuwa vigumu kufuatilia maendeleo, kubaini mwenendo wa ukeketaji na kufanya maamuzi yanayotegemea ushahidi, hali inayopunguza uwezo wa programu kujibu mabadiliko kwa wakati. Kuendelea kuwepo kwa ukeketaji wa kuvuka mipaka kunazidisha hatari hizi, kwani usafirishaji wa watoto wa kike kuvuka mipaka ya kitaifa hudhoofisha jitihada za ndani na kuhitaji majibu ya kikanda yaliyoratibiwa kwa karibu.

**Jedwali Na 10: Uchambuzi wa Hatari za Kimkakati na Hatua za Kukabiliana nazo**

| Eneo la Hatari | Changamoto Kuu ya Kimkakati | Matokeo | Uwezekano | Mikakati ya Kukabiliana |
|---|---|---|---|---|
| Kisera na Kisheria | Utekelezaji na usimamizi wa Sheria usio kidhi haja na mahitaji | Hupunguza uwajibikaji; husababisha mwanya wa vitendo vya ukeketaji kuendelea; hupunguza imani ya umma katika mfumo wa utekelezaji na usimamizi wa Sheria | Wastani hadi Juu | • Kuhamasisha utokomezaji wa ukeketaji kama kipaumbele kwa vyombo vya dola.<br>• Kuendelea kuwajengea uwezo Polisi, Waendesha ashtaka na ahakama kuhusu Sheria za ukeketaji na mbinu zinazomlenga manusura.<br>• Kuimarisha mifumo ya utoaji taarifa na uwajibikaji kwa mashauri ya ukeketaji.<br>• Kuimarisha uratibu kati ya Sekta ya Sheria na Sekta ya Hifadhi ya Jamii. |
| Kisera na Kisheria | Sera zilizopitwa na wakati na mianya ya kisheria | Mapungufu ya ulinzi wa kisheria hupunguza ufanisi wa mfumo wa sheria na huruhusu kuendelea kwa vitendo vya ukatili bila njia bayana za kisheria za kushughulikia | Wastani | • Kufanya mapitio ya sera na sheria zote husika za kitaifa (mf. Sera ya Maendeleo ya Mtoto) ili ziendane na muktadha wa sasa wa ukeketaji.<br>• Kulinganisha sheria za kitaifa na mifumo ya kikanda (Afrika Mashariki na Umoja wa Afrika) na viwango vya kimataifa vya kupiga marufuku ukeketaji. |
| Kijamii na Kitamaduni | Upinzani wa kitamaduni na kijamii (mila zilizokita mizizi, mfumo dume) | Hupunguza kasi ya kutokomeza ukeketaji; huendeleza vitendo kizazi hadi kizazi; huibua upinzani dhidi ya afua | Juu | • Kuimarisha mijadala ya kijamii inayozingatia muktadha wa kitamaduni, ikiwashirikisha viongozi wa kimila na dini, wanaume na wavulana vinara.<br>• Kukuza mienendo chanya ya kijamii kupitia kampeni endelevu za uhamasishaji kwa umma kwa kutumia |

| Eneo la Hatari | Changamoto Kuu ya Kimkakati | Matokeo | Uwezekano | Mikakati ya Kukabiliana |
|---|---|---|---|---|
| | | | | wahamasishaji wa ndani ya jamii.<br>• Kuandaa na kusambaza simulizi mbadala zinazopinga imani potofu za kitamaduni bila kutenga jamii. |
| Kijamii na Kitamaduni | Kuibuka kwa vitendo vilivyojificha na taratibu za kuvusha rika zinazohusisha ukeketaji | Husababisha utambuzi na ufuatiliaji wa matukio ya ukeketaji kuwa mgumu; hukwepa makatazo ya kisheria; hujenga taswira potofu ya kuachana na ukeketaji | Juu | • Kufanya tafiti za kina kubaini mabadiliko ya vitendo vilivyojificha na taratibu mbadala zinazohusisha ukeketaji.<br>• Kuandaa zana na viashiria mahsusi vya kubaini na kutoa taarifa kuhusu aina hizi mpya.<br>• Kuimarisha mifumo ya ulinzi na utoaji wa taarifa inayotegemea jamii.<br>• Kuelimisha jamii kuhusu tofauti kati ya taratibu za kitamaduni zisizo na madhara na vitendo hatarishi vinavyojificha. |
| Kijamii na Mawasiliano | Uelewa mdogo wa umma na elimu hafifu kuhusu madhara ya ukeketaji | Huendeleza taarifa potofu; huimarisha upinzani wa kijamii; hupunguza ushiriki wa jamii katika afua | Wastani | • Kutekeleza kampeni lengwa, endelevu na zinazofikika kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo redio, maigizo ya kijamii, mitandao ya kijamii, makala na vipeperushi.<br>• Kujumuisha elimu ya ukeketaji katika mitaala rasmi na isiyo rasmi.<br>• Kuwawezesha waelimishaji wa jamii na vinara wa kwenye jamii kusambaza taarifa sahihi. |
| Kifedha na Uendeshaji | Uhaba wa rasilimali fedha | Hupunguza kasi ya utekelezaji na uendelevu wa afua za kutokomeza ukeketaji; | Juu | • Kuongeza utengaji wa bajeti ya ndani kwa afua za kutokomeza ukeketaji katika Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa. |

| Eneo la Hatari | Changamoto Kuu ya Kimkakati | Matokeo | Uwezekano | Mikakati ya Kukabiliana |
|---|---|---|---|---|
| | | hupunguza wigo wa programu | | • Kuongeza vyanzo vya mapato kwa kushirikisha wadau wa maendeleo na sekta binafsi.<br>• Kubainisha gharama na matokeo ya afua ili kuhamasisha uwekezaji zaidi wa rasilimali fedha.<br>• Kuhakikisha ukeketaji unajumuishwa kama eneo la kipaumbele katika mipango ya maendeleo ya taifa na MTEF. |
| Taarifa na Takwimu | Mifumo ya takwimu za kielektroniki kwa ufuatiliaji na tathmini | Huathiri ufuatiliaji wa maendeleo; huzuia uchambuzi wa mwenendo; hupunguza maamuzi yanayozingatia takwimu | Wastani | • Kuwekeza katika kuendeleza na kutekeleza mfumo thabiti wa kitaifa wa kielektroniki wa ufuatiliaji na tathmini ya ukeketaji.<br>• Kuimarisha uwezo wa ukusanyaji, uchambuzi na utoaji wa taarifa za takwimu katika ngazi zote.<br>• Kuhakikisha takwimu zinaainishwa kubaini mienendo na makundi hatarishi.<br>• Kuanzisha mifumo ya mapitio ya mara kwa mara ya takwimu kwa maboresho ya kimkakati. |
| Mipakani | Ukeketaji wa kuvuka mipaka (usafirishaji wa wasichana kuvuka mipaka kwa ajili ya ukeketaji) | Huathiri mafanikio ya utekelezaji wa sheria za kitaifa; hufanya ufuatiliaji kuwa mgumu; huendeleza vitendo nje ya udhibiti wa taifa | Wastani | • Kuimarisha ushirikiano wa kijumuia wa kikanda na makubaliano na nchi jirani katika jitihada za kutokomeza ukeketaji.<br>• Kuanzisha mipango ya pamoja ya utekelezaji, itifaki za kubadilishana takwimu na mikakati shirikishi ya kuzuia ukeketaji katika maeneo ya mipakani.<br>• Kuongeza ulinzi na ufuatiliaji katika maeneo yanayotambulika kama |

| Eneo la Hatari | Changamoto Kuu ya Kimkakati | Matokeo | Uwezekano | Mikakati ya Kukabiliana |
|---|---|---|---|---|
| | | | | vihatarishi vya ukeketaji wa kuvuka mipaka.<br>• Kufanya kampeni za pamoja za uhamasishaji katika maeneo ya mipaka. |

# VIAMBATISHO



# VIAMBATISHO

## Kiambatisho Na. 1: Jedwali la Matokeo

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Lengo Kuu la Jumla:** Kupunguza kiwango cha ukeketaji nchini kwa 50% kutoka 8% (2024/2025) hadi 4% (2029/30) | % ya upungufu wa wasichana wenye umri wa miaka 0–14 waliokeketwa | 8% | 7% | 6% | 5% | 4% | 4% | 4% | Tafiti za Kitaifa za TDHS-MIS | Mara moja | Taarifa rasmi za TDHS–MIS (taarifa za mwisho, taarifa za awali, jedwali za takwimu); machapisho ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Wizara ya Afya | UNICEF Tanzania; UNFPA Tanzania; Asasi za kiraia za ndani/kimataifa (mf. NAFGEM, LHRC, Hope for Girls and Women Tanzania, Plan International n.k.) |

**Lengo la Kimkakati la I (LK1) – Kuimarisha Utekelezaji wa Mifumo ya kisera na kisheria**

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Tokeo la Kati 1.1:** Kuimarika kwa ulinganifu wa Sera na sheria za Kitaifa na Mifumo ya Kikanda na Kimataifa ya Haki za Binadamu | Idadi ya sera na sheria za kitaifa zilizoendanishwa na mifumo ya kimataifa | 2 | 1 | 2 | 2 | 1 | 1 | 6 | Mapitio ya kisheria; nyaraka za sera | Kila mwaka | Gazeti Rasmi la Serikali; taarifa za uchambuzi wa kisheria | Wizara ya Katiba na Sheria; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake | Asasi za Kiraia (CSOs); Bunge |

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| katika kuzuia ukeketaji | | | | | | | | | | | | na Makundi Maalum | |
| | Idadi ya sera na sheria zilizopitiwa au kutungwa ili kushughulikia moja kwa moja masuala yanayohusiana na ukekeltaji. | 1 | 1 | 1 | 2 | 1 | 1 | 6 | Mapitio ya kisheria; nyaraka za sera | Kila mwaka | Sheria husika kuwepo; Gazeti Rasmi la Serikali; taarifa za uchambuzi wa kisheria; tafiti; Sheria ya Ushahidi; Sheria ya Ulinzi wa Mashahidi; Sheria ya Mtoto | Wizara ya Katiba na Sheria; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | Asasi za Kiraia; Bunge |
| **Tokeo la Kati 1.2:** Kuimarika kwa uwezo wa kiutendaji kwa wasimamizi wa sheria na vyombo vya usalama katika kutekeleza na kusimia kwa ufanisi sheria za | % ya ongezeko la watendaji wa utekelezaji wa sheria waliopata mafunzo kuhusu kuzuia, kutoa taarifa na kuchukua hatua za mwitikio dhidi ya ukeketaji | 90% | 15% | 15% | 15% | 20% | 20% | 85% | Taarifa za mafunzo | Kila mwaka | Orodha za mahudhurio; matokeo ya tathmini kabla/baada ya mafunzo | Mahakama; Jeshi la Polisi; Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | Taasisi za mafunzo/Wawezeshaji wa Kitaifa |

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| kupambana na ukeketaji | | | | | | | | | | | | | |
| | Idadi ya watendaji wa Sheria na mifumo ya utekelezaji wa Sheria waliojengewa uwezo katika kuzuia, utoaji taarifa na mwitikio dhidi ya ukeketaji | 518 | 90 | 90 | 90 | 90 | 90 | 450 | Taarifa za mafunzo | Kila mwaka | Orodha za mahudhurio; matokeo ya tathmini kabla/baada ya mafunzo | Mahakama; Jeshi la Polisi; Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | Taasisi za mafunzo |
| | Asilimia ya ongezeko la kesi za ukeketaji zilizochunguzwa, kufikishwa mahakamani na kupatikana na hatia | TBD | 80% | 80% | 85% | 90% | 95% | 95% | Kumbukumbu za mahakama | Kila robo mwaka | Hukumu za mahakama; kanzidata za ufuatiliaji wa mashauri | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; Mahakama | Jeshi la Polisi |
| | Uwepo wa Taratibu za Uendeshaji katika kushughulikia kesi za ukeketaji | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 3 | Taarifa za usambazaji | Mara moja | Hati ya miongozo iliyoidhinishwa | Mahakama; Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | Wizara ya Katiba na Sheria |
| **Lengo la Kimkakati la II (LK2) - Kuwezesha Jamii na Watu Binafsi Kuachana na Ukeketaji** | | | | | | | | | | | | | |

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Tokeo la Kati 2.1:** Kuongezeka kwa uelewa wa jamii na kukataa ukeketaji kama mila na desturi yenye madhara | % ya ongezeko la wanajamii wenye uelewa wa madhara ya ukeketaji na athari zake za kisheria | 37% | 15% | 10% | 20% | 15% | 15% | 75% | Tafiti za jamii | Kila baada ya miaka miwili | Taarifa za tafiti | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) | Asasi za Kiraia; Viongozi wa Jadi na wa Kidini |
| | Idadi ya viongozi wa dini na wa kimila wanaohamasisha kikamilifu kukomesha ukeketaji katika jamii zao | 45 | 80 | 100 | 180 | 90 | 300 | 750 | Taarifa za matamko ya jamii kutoka kwa viongozi wa eneo | Kila mwaka | Taarifa za matukio; taarifa za vyombo vya habari | Viongozi wa Jadi na wa Kidini; Asasi za Kiraia | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| | % ya ongezeko la wanaume na wavulana vinara wa kutokomeza ukeketaji | TBD | 5% | 10% | 15% | 18% | 22% | 70% | Tafiti za jamii | Kila baada ya miaka miwili | Taarifa za tafiti | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; OWM-TAMISEMI | Asasi za Kiraia; Viongozi wa Jadi na wa Kidini |
| **Tokeo la kati 2.2:** Kuimarishwa kwa uwezeshaji wa kiuchumi na msaada wa kijamii | Idadi ya ngariba waliopata mafunzo ya uwezeshaji kiuchumu na stadi mbadala za kujipatia kipato | 18 | 18 | 18 | 18 | 18 | 18 | 90 | Taarifa za mafunzo | Kila baada ya miezi sita | Vyeti vya mafunzo | Wizara ya Maendeleo ya Jamii; OWM-TAMISEMI | Wizara na Tasisi za Kisekta, Wadau wa Maendeleo, Taasisi Da dini na Mashirika |

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| kwa wakeketaji (ngariba) na manusura | | | | | | | | | | | | | yasio ya Kiserikali |
| | Idadi ya ngariba waliotambuliwa na kuingizwa katika vyanzo mbadala na endelevu vya kiuchumi | 18 | 18 | 18 | 18 | 18 | 18 | 90 | Taarifa za shughuli | Kila baada ya miezi sita | Taarifa za Kila mwaka za Utekelezaji | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; OWM-TAMISEMI | Wizara na Tasisi za Kisekta, Wadau wa Maendeleo, Taasisi Da dini na Mashirika yasio ya Kiserikali |

**Lengo la Kimkakati la III (LK3) – Kuimarisha Upatikanaji wa Huduma Huduma Bora za Kuzuia, Kutoa Taarifa na mwitikio**

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Tokeo la Kati 3.1:** Kuimarishwa kwa upatikanaji wa huduma jumuishi za kuzuia, kutoa taarifa na mwitikio kwa manusura | % ya manusura wa ukeketaji wanaopata huduma jumuishi za kitabibu, kisaikolojia na kisheria | 87% | 15% | 20% | 15% | 20% | 20% | 90% | Tafiti za watumiaji wa huduma; takwimu za usimamizi wa kesi | Kila mwaka | Tafiti za kuridhika kwa wateja; taarifa za matumizi ya huduma | Wizara ya Afya; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; OWM-TAMISEMI | Wadau wa Maendeleo, Taasisi za dini, Asasi za Kiraia |
| | Maudhui yalioboreshwa kuhusu kinga dhidi ya | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | Taarifa za programu; mapitio ya mitaala | Kila mwaka | Nyaraka za mitaala; taarifa za shule | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Asasi za Kiraia | Shule; Vituo vya Elimu ya Jamii |

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ukeketaji katika mitaala ya shule na programu za elimu isiyo rasmi. | | | | | | | | | | | | |
| | Idadi ya nyumba salama kwa manusura wa ukeketaji zilizoanzishwa na kuimarishwa | 18 | 4 | 6 | 8 | 8 | 8 | 52 | Taarifa ya Mwaka ya Kikundi Kazi kutoka Sekretariati | Kila Mwaka | Taarifa ya Tathmini ya Kati ya Utekelezaji wa Mkakati | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Sekretariati) | Wizara za Kisekta na Wadau wa Maendeleo, mashirika yasiyo ya Kiserikali, Jamii |
| | Idadi ya vituo vya huduma jumuishi za huduma kwa manusura wa ukeketaji zilizoanzishwa na kuimarishwa | 33 | 2 | 3 | 5 | 5 | 4 | 52 | Taarifa ya Mwaka ya Kikundi Kazi kutoka Sekretariati | Kila Mwaka | Taarifa ya Tathmini ya Kati ya Utekelezaji wa Mkakati | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Sekretariati) | Wizara za Kisekta na Wadau wa Maendeleo, mashirika yasiyo ya Kiserikali, Jamii |
| | Idadi ya watoa huduma za afya waliopata mafunzo ya kuzuia, kuchuja, kutoa taarifa na huduma zinazomlenga | 225 | 140 | 140 | 140 | 140 | 140 | 600 | Taarifa ya Utekelezaji ya kamati Tendaji ya Mkakati | Kila Robo Mwaka | Taarifa za Mafunzo | Taasisi za Mafunzo ya Afya; Asasi za Kiraia | Wizara za Kisekta na Wadau wa Maendeleo, mashirika yasiyo ya Kiserikali, Jamii |

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | manusura wa ukeketaji | | | | | | | | | | | | |
| | Idadi ya vituo vya utoaji huduma vya kisekta vilivyoimarishwa | 4 | 5 | 5 | 5 | 5 | 5 | 25 | Taarifa za maboresho ya miundombinu; sajili za vifaa | | Taarifa ya Tathmini ya Kati na ya Mwisho ya Mkakati | Wizara ya Afya; LGAs | Wizara za Serikali; LGAs; Asasi za Kiraia |
| | Idadi ya manusura wa ukeketaji na wasichana walio katika mazingira hatarishi wanaopata huduma za kisaikolojia, kijamii au msaada wa kiuchumi | 33 | 3,000 | 4,000 | 5,000 | 1,500 | 1,500 | 15,000 | Taarifa ya Utekelezaji ya Kikundi kazi cha Kitaifa cha Kisekta cha Mkakati | Kila Robo Mwaka | Taarifa ya Utekelezaki ya Mwaka | OWM-TAMISEMI, | Wizara za Kisekta;; Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; Taasisi za Dini |

**Lengo la Kimkakati la IV (LK4) - Kuimarisha Uratibu, Ushirikiano wa Kisekta na Uhamasishaji wa Rasilimali**

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Tokeo la Kati 4.1:** Kuimarika kwa uratibu na ushirikiano wa kisekta miongoni mwa wadau | Idadi ya wanachama wanaohudhuria vikao na wenye uwajibikaji wa Kamati ya Kiufundi ya Kisekta | 18 | 50 | 50 | 50 | 50 | 50 | 250 | Taarifa za vikao; kumbukumbu za mahudhurio | Kila robo mwaka | Kumbukumbu za vikao; taarifa za utekelezaji | Wizara (zinazohusika) | Asasi za Kiraia; LGAs |

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya majukwaa ya wadau yaliyoratibiwa katika ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji/Mtaa | 4 | 32 | 32 | 32 | 32 | 32 | 160 | Taarifa za shughuli | — | Taarifa za utekelezaji | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum | Asasi za Kiraia; LGAs |
| **Tokeo la Kati 4.2:** Kuongezeka kwa rasilimali fedha na utaalamu endelevu kwa ajili ya kutokomeza ukeketaji | % ya ongezeko la rasilimali za kifedha zilizohamasishwa ndani ya nchi na kimataifa kwa kutokomeza ukeketaji | 0.5% | 2% | 3% | 4% | 4% | 4% | 17% | Taarifa za kifedha | Kila mwaka | Makubaliano ya wafadhili; taarifa za bajeti | Wizara ya Fedha; Asasi za Kiraia | Wadau wa Maendeleo na Masjhirika yasiyo ya Kiserikali |
| | % ya ongezeko la mgao wa bajeti ya Serikali katika sekta husika kwa kutokomeza ukeketaji | 0.5% | 2% | 3% | 4% | 4% | 4% | 17% | Taarifa fupi za bajeti | Kila mwaka | Mapitio ya taarifa fupi za bajeti | Wizara ya Fedha; Wizara husika | Bunge |
| | Uwepo wa mkakati wa uhamasishaji wa rasimali kwa ajili ya kutokomeza ukeketaji. | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | Taarifa ya Mwaka ya Kikundi Kazi kutoka Sekretariati | Kila Mwaka | Taarifa ya Tathmini ya Kati na ya Mwisho ya Utekelezaji wa Mkakati | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Sekretariati) | Kikundi Kazi cha Kitaifa cha Kisekta cha Utekelezaji wa Mkakati, Wadau wa maendeleo an Mashirika |

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | yasiyo ya Kiserikali |
| | Idadi ya taasisi zilizoahidi rasilimali fedha kwa kutokomeza ukeketaji | 2 | 5 | 5 | 5 | 5 | 5 | 25 | Taarifa za kifedha | Kila mwaka | Makubaliano ya wafadhili; taarifa za bajeti | Wizara ya Fedha; Asasi za Kiraia | Wadau wa Maendeleo |
| | Idadi ya programu au miradi ya ukeketaji iliyofadhiliwa | 0 | 1 | 1 | 1 | 2 | 1 | 6 | Kumbukumbu za maombi ya miradi | Kila mwaka | Maombi yaliyowasilishwa; tuzo za ruzuku | Asasi za Kiraia; Taasisi za Serikali | Wafadhili |
| | Idadi ya Mikoa iliyoingiza huduma maalum za kuzuia, kutoa taarifa na kukabiliana na ukeketaji katika mifumo ya utekelezaji ili kuhakikisha uthabiti, uwajibikaji na ubora. | 0 | 0 | 13 | 0 | 0 | 0 | 13 | Taarifa ya Mwaka ya Kikundi Kazi kutoka Sekretariati | Kila Mwaka | Taarifa ya Tathmini ya Kati na ya Mwisho ya Utekelezaji wa Mkakati | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Sekretariati) | Kikundi Kazi cha Kitaifa cha Kisekta cha Utekelezaji wa Mkakati |

**Lengo la Kimkakati la V (LK5) - Kuimarisha Tafiti na Kujifunza**

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Tokeo la Kati 5.1:** Kuimarika kwa uwezo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji katika afua za | Idadi ya tafiti mahsusi za ukeketaji zilizofanyika | 2 | 0 | 1 | 1 | 1 | 1 | 5 | Taarifa za utafiti; hifadhidata za machapisho | Kila mwaka | Machapisho ya utafiti; taarifa za sera | Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS); Taasisi za Utafiti; Vyuo Vikuu | Wasomi; Asasi za Kiraia |

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| kutokomeza ukeketaji | | | | | | | | | | | | | |
| | Idadi ya mbinu bora (best practices) zilizobainishwa, kuandikwa na kusambazwa | 9 | 9 | 9 | 9 | 9 | 9 | 45 | Taarifa za majukwaa | Kila mwaka | Mifumo ya mtandaoni; kumbukumbu za Jamii za Mazoezi (CoP) | Wizara ya Habari; Taasisi za Utafiti; Asasi za Kiraia | Wasomi |
| | Dashibodi ya kitaifa ya ukeketaji kuwepo | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | Taarifa za mfumo | Mara moja | Mapitio ya mfumo wa hifadhidata | Wizara ya Afya; NBS | — |
| **Tokeo 5.2:** Kuimarika kwa uwezo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji katika afua za kutokomeza ukeketaji | Idadi ya wadau waliopatiwa mafunzo ya ufuatiliaji, tathmini na matumizi ya takwimu za ukeketaji | 0 | 140 | 140 | 140 | 140 | 140 | 700 | Nyaraka za programu | Kila mwaka | Mipango ya M&E; jedwali za viashiria | Taasisi zote zinazotekeleza; Asasi za Kiraia | Wizara za Serikali; Asasi za Kiraia |
| | Idadi ya wadau walioingiza mifumo ya ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji katika afua zao za kutokomeza ukeketaji. | 2 | 5 | 5 | 5 | 5 | 5 | 27 | Taarifa za mafunzo | Kila mwaka | Orodha za mahudhurio; tathmini za umahiri | NBS; Taasisi Tekelezaji | Wizara za Serikali; Asasi za Kiraia |
| | Jukwaa la Kitaifa la kila mwaka la ujifunzaji la wadau | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | Taarifa za majukwaa | Kila mwaka | Mifumo ya mtandaoni; kumbukumbu za | Wizara ya Habari; Taasisi za Utafiti; Asasi za Kiraia | Wasomi |

| Matokeo | Kiashiria | Takwimu ya Msingi | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | Lengo | Chanzo cha Taarifa | Marudio | Njia za Uhakiki | Wahusika | Wadau |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | wanaotekeleza afua za kutokomeza ukeketaji | | | | | | | | | | Jamii za Mazoezi (CoP) | | |
| | Taarifa ya tathmini ya kati na ya mwisho ya utekelezaji wa Mkakati. | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | Tathmini ya Kati na ya Mwisho ya Utekelezaji wa Mkakati | Mwaka wa Tatu na wa Tano wa Utekelkezaji | Wizarta ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum | Wajumbe wa Kikundi Kazi cha Taifa cha Kisekta cha Utekelezaji wa Mkakati | Wizara za Kisekta na Wadau wa Maendeleo, Taasisi zisizo za Kiserikali, Jamii |

***Tanbihi: M = Mwaka**

## Kiambatisho Na. 2: Mpango Kazi Wenye Makadirio ya Gharama

| Matokeo/Shughuli | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Lengo la Kimkakati I (LK1): Kuimarisha Utekelezaji wa Sera na Mfumo wa Kisheria** | | | | | | |
| **Matokeo ya Kati 1.1:** Kuimarika kwa Ulinganifu wa Sera na Sheria za Kitaifa na Mifumo ya Kikanda na Kimataifa ya Haki za Binadamu katika Kuzuia Ukeketaji | 720,000,000 | 200,000,000 | 245,000,000 | 80,000,000 | 50,000,000 | 1,295,000,000 |
| **Afua ya Kimkakati 1.1.1:** Kuwezesha ulinganifu wa Sera na Sheria za Kitaifa na Mifumo ya Kimataifa ya haki za binadamu (ikiwemo Itifaki ya Maputo, CRC na CEDAW) kupitia mapitio ya sera, msaada wa kitaalamu na mashauriano ya wadau wa kisekta. | 330,000,000 | 40,000,000 | 30,000,000 | 30,000,000 | 0 | 430,000,000 |
| **Afua ya Kimkakati 1.1.2:** Kufanya mapitio na marekebisho ya mifumo ya kisera na kisheria ili kuhakikisha yanakataza waziwazi ukeketaji na kuendana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu | 390,000,000 | 160,000,000 | 215,000,000 | 50,000,000 | 50,000,000 | 865,000,000 |
| **Matokeo 1.2:** Kuimarika kwa uwezo wa watendaji wa kisheria na vyombo vya usalama katika kutekeleza na kusimamia kwa ufanisi sheria za kupambana na ukeketaji i | 230,000,000 | 225,000,000 | 130,000,000 | 175,000,000 | 30,000,000 | 790,000,000 |
| **Afua ya Kimkakati 1.2.1:** Kuimarisha uwezo wa watendaji wa sheria na mifumo ya utekelezaji wa sheria katika kuzuia, utoaji taarifa na mwitikio dhidi ya ukeketaji | 135,000,000 | 190,000,000 | 105,000,000 | 155,000,000 | 30,000,000 | 615,000,000 |

| Matokeo/Shughuli | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Afua ya Kimkakati 1.2.2:** Kuanzisha na kuimarisha Taratibu za Uendeshaji (*Standard Operating Procedures -SOPs*) kwa ajili ya kushughulikia kesi za ukeketaji ndani ya vyombo vya utekelezaji wa sheria | 95,000,000 | 35,000,000 | 25,000,000 | 20,000,000 | 0 | 175,000,000 |
| **Jumla ya LK1 (SO1)** | **950,000,000** | **425,000,000** | **375,000,000** | **255,000,000** | **80,000,000** | **2,085,000,000** |
| **Lengo la Kimkakati II (LK2): Kuwezesha Jamii na Watu Binafsi Kuachana na Ukeketaji** | | | | | | |
| **Matokeo 2.1:** Kuongezeka kwa uelewa wa jamii na kukataa ukeketaji kama mila na desturi yenye madhara | 1,789,000,000 | 2,943,000,000 | 1,300,000,000 | 767,000,000 | 412,000,000 | 7,211,000,000 |
| **Afua za Kimkakati 2.1.1:** Kufanya kampeni za kutokomeza ukeketaji | 210,000,000 | 207,000,000 | 185,000,000 | 182,000,000 | 167,000,000 | 951,000,000 |
| **Afua ya Kimkakati 2.1.2:** Kuwashirikisha viongozi wa dini na wa kimila katika juhudi za kutokomeza ukeketaji | 88,000,000 | 200,000,000 | 70,000,000 | 70,000,000 | 70,000,000 | 498,000,000 |
| **Afua ya Kimkakati 2.1.3:** Kuhamasisha wanaume na wavulana kuwa vinara wa mabadiliko na kuunga mkono jitihada za kutokomeza ukeketaji.i | 315,000,000 | 250,000,000 | 130,000,000 | 230,000,000 | 130,000,000 | 1,055,000,000 |
| **Afua ya Kimkakati 2.1.4:** Kuwajengea uwezo wanawake na watoto wa kike kuwa vinara wa mabadiliko | | | | | | |
| **Matokeo 2.2:** Kuimarika kwa Uwezeshaji wa Kiuchumi na Mifumo ya Msaada wa Kijamii kwa Ngariba na Manusura | 567,000,000 | 1,337,000,000 | 570,000,000 | 160,000,000 | 30,000,000 | 2,664,000,000 |

| Matokeo/Shughuli | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Afua ya Kimkakati 2.2.1:** Kuwawezesha kiuchumi ngariba waliobainishwa ili kuwasaidia kuingia kwenye shughuli mbadala endelevu za kujipatia kipato | 175,000,000 | 575,000,000 | 265,000,000 | 65,000,000 | 15,000,000 | 1,095,000,000 |
| **Afua ya Kimkakati 2.2.2:** Kuanzisha na kuimarisha mitandao jumuishi ya msaada wa kijamii kwa manusura wa ukeketaji. | 217,000,000 | 187,000,000 | 40,000,000 | 30,000,000 | 0 | 474,000,000 |
| **Jumla ya LK2** | **2,181,000,000** | **3,705,000,000** | **1,605,000,000** | **862,000,000** | **427,000,000** | **8,780,000,000** |
| **Lengo la Kimkakati la III (LK3): Kuimarisha Upatikanaji wa Huduma Jumuishi dhidi ya Ukeketaji** | | | | | | |
| **Matokeo 3.1:** Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma jumuishi za kuzuia, kutoa taarifa na mwitikio kwa manusura | **17,000,000** | **287,000,000** | **347,000,000** | **152,000,000** | **17,000,000** | **820,000,000** |
| **Afua ya Kimkakati 3.1.1:** Kuimarisha mifumo ya rufaa na utoaji wa huduma kwa kuwajengea uwezo watoa huduma za afya, maafisa ustawi wa jamii na watendaji wa sheria ili kutoa huduma jumuishi, zinazomlenga mhanga, za kitabibu, kisaikolojia-kijamii na kisheria kwa manusura wa ukeketaji | 17,000,000 | 202,000,000 | 152,000,000 | 152,000,000 | 17,000,000 | 540,000,000 |
| **Afua ya Kimkakati 3.1.2:** Kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na mashirika ya kiraia ili kuingiza maudhui yanayofaa kwa umri kuhusu kuzuia ukeketaji katika mitaala ya shule na programu zisizo rasmi za elimu, sambamba na kuwajengea uwezo walimu kuwasilisha maudhui hayo kwa ufanisi na kuwezesha majadiliano salama na yenye taarifa sahihi | - | 85,000,000.00 | 195,000,000.00 | - | - | 280,000,000.00 |
| **Jumla ya LK3 (SO3)** | **17,000,000** | **287,000,000** | **347,000,000** | **152,000,000** | **17,000,000** | **820,000,000** |
| **Lengo la Kimkakati IV (LK4): Kuimarisha Uratibu, Ushirikiano wa Kisekta na Uhamasishaji wa Rasilimali** | | | | | | |

| Matokeo/Shughuli | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Matokeo 4.1: Uratibu na ushirikiano wa kisekta ulioimarishwa miongoni mwa wadau** | **544,000,000** | **340,000,000** | **260,000,000** | **260,000,000** | **260,000,000** | **1,664,000,000** |
| **Afua ya Kimkakati 4.1.1:** Kuimarisha Kikundi Kazi cha Taifa cha kutokomeza ukeketaji | 80,000,000 | 60,000,000 | 60,000,000 | 60,000,000 | 60,000,000 | 320,000,000 |
| **Afua ya Kimkakati 4.1.2:** Kuimarisha mifumo ya uratibu wa ngazi za Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji/Mtaa | 464,000,000 | 280,000,000 | 200,000,000 | 200,000,000 | 200,000,000 | 1,344,000,000 |
| **Matokeo 4.2: Kuongezeka kwa rasilimali fedha na utaalamu endelevu kwa ajili ya kutokomeza ukeketaji** | **256,000,000** | **179,000,000** | **150,000,000** | **148,000,000** | **103,000,000** | **836,000,000** |
| **Afua ya Kimkakati 4.2.1:** Kuandaa na kutekeleza mkakati wa uhamasishaji wa rasilimali kwa ajili ya kutokomeza ukeketaji. | 95,000,000 | 60,000,000 | 30,000,000 | 30,000,000 | 25,000,000 | 240,000,000 |
| **Afua ya Kimkakati 4.2.2:** Ujumuishaji wa afua za ukeketaji katika mipango na bajeti za kisekta kwa kushirikisha Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ili kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali za Serikali kwa uendelevu katika sekta husika. | 161,000,000 | 119,000,000 | 120,000,000 | 118,000,000 | 78,000,000 | 596,000,000 |
| **Jumla ya LK4 (SO4)** | **800,000,000** | **519,000,000** | **410,000,000** | **408,000,000** | **363,000,000** | **2,500,000,000** |
| **Lengo la Kimkakati la V: Kuimarisha Uzalishaji wa Ushahidi, Usimamizi wa Maarifa na Kujifunza** | | | | | | |
| **Matokeo ya 5.1: Kuimarika kwa tafiti na takwimu kwa ajili ya afua na uundaji wa sera za kutokomeza ukeketaji** | **198,000,000** | **10,000,000** | **151,000,000** | **8,000,000** | **6,000,000** | **373,000,000** |

| Matokeo/Shughuli | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Afua za Kimkakati 5.1.1:** Kufanya tafiti za kusaidia uboreshaji wa afua za kutokomeza ukeketaji. | 55,000,000 | 0 | 55,000,000 | 0 | 0 | 110,000,000 |
| **Afua za Kimkakati 5.1.2:** Kuimarisha mifumo ya na ukusanyaji wa takwimu. | 143,000,000 | 10,000,000 | 96,000,000 | 8,000,000 | 6,000,000 | 263,000,000 |
| **Matokeo 5.2: Kuimarika kwa uwezo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji katika programu za kutokomeza ukeketaji** | **414,000,000** | **270,000,000** | **282,000,000** | **251,000,000** | **195,000,000** | **1,412,000,000** |
| **Afua ya Kimkakati 5.2.1:** Kubuni na kutekeleza programu mahsusi za kujenga uwezo wa wadau kuhusu ufuatiliaji, tathmini na matumizi ya taarifa za ukeketaji | 202,000,000 | 155,000,000 | 160,000,000 | 145,000,000 | 115,000,000 | 777,000,000 |
| **Afua ya Kimkakati 5.2.2:** Kufanya tathmini za kati na za mwisho za utekelezaji wa Mkakati | | | 48,000,000 | | 40,000,000 | 88,000,000 |
| **Afua ya Kimkakati 5.1.3:** Kuendesha jukwaa la Kitaifa la kila mwaka la ujifunzaji la wadau wanaotekeleza afua za kutokomeza ukeketaji. | | 115,000,000 | 112,000,000 | 116,000,000 | 10,000,000 | 547,000,000 |
| **Jumla ya Lengo la Kimkakati V (SO5)** | **612,000,000** | **280,000,000** | **433,000,000** | **259,000,000** | **201,000,000** | **1,785,000,000** |
| | | | | | **JUMLA KUU** | **15,970,000,000** |

## Kiambatisho Na. 3: Muhtasari wa Bajeti

| Matokeo/Shughuli | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Lengo la Kimkakati I (LK1): Kuimarisha Utekelezaji wa Sera na Mfumo wa Kisheria** | | | | | | |
| **Matokeo ya Kati 1.1:** Ulinganifu ulioboreshwa wa Sera na Sheria za kitaifa na Kuimarika kwa Ulinganifu wa Sera na Sheria za Kitaifa na Mifumo ya Kikanda na Kimataifa ya Haki za Binadamu katika Kuzuia Ukeketaji | 720,000,000 | 200,000,000 | 245,000,000 | 80,000,000 | 50,000,000 | 1,295,000,000 |
| **Matokeo 1.2:** Uwezo ulioboreshwa wa vyombo vya utekelezaji wa sheria kutekeleza na kusimamia kwa ufanisi sheria zinazohusiana na ukeketaji | 230,000,000 | 225,000,000 | 130,000,000 | 175,000,000 | 30,000,000 | 790,000,000 |
| **Jumla ya LK1 (SO1)** | **950,000,000** | **425,000,000** | **375,000,000** | **255,000,000** | **80,000,000** | **2,085,000,000** |
| **Lengo la Kimkakati II (LK2): Kuwezesha Jamii na Watu Binafsi Kuachana na Ukeketaji** | | | | | | |
| **Matokeo 2.1:** Uelewa wa jamii umeongezeka kuhusu ukeketaji kama tendo lenye madhara | 1,789,000,000 | 2,943,000,000 | 1,300,000,000 | 767,000,000 | 412,000,000 | 7,211,000,000 |
| **Matokeo 2.2:** Uwezeshaji wa kijamii na kiuchumi umeimarishwa kwa mangariba na viongozi wa kimila ili kuachana na vitendo vya ukeketaji | 567,000,000 | 1,337,000,000 | 570,000,000 | 160,000,000 | 30,000,000 | 2,664,000,000 |
| **Jumla ya LK2** | **2,181,000,000** | **3,705,000,000** | **1,605,000,000** | **862,000,000** | **427,000,000** | **8,780,000,000** |
| **Lengo la Kimkakati la III (LK3): Kuimarisha Upatikanaji wa Huduma Bora za Kuzuia, Kutoa Taarifa na Mwitikio dhidi ya Ukeketaji** | | | | | | |
| **Matokeo 3.1:** Upatikanaji ulioboreshwa wa huduma jumuishi za kuzuia, kutoa taarifa na kuitikia masuala ya ukeketaji | **17,000,000** | **287,000,000** | **347,000,000** | **152,000,000** | **17,000,000** | **820,000,000** |
| **Jumla ya LK3 (SO3)** | **17,000,000** | **287,000,000** | **347,000,000** | **152,000,000** | **17,000,000** | **820,000,000** |
| **Lengo la Kimkakati IV (LK4): Kuimarisha Uratibu, Ushirikiano wa Kisekta na Uhamasishaji wa Rasilimali** | | | | | | |

| Matokeo/Shughuli | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Matokeo 4.1:** Uratibu na ushirikiano wa kisekta ulioimarishwa miongoni mwa wadau | **544,000,000** | **340,000,000** | **260,000,000** | **260,000,000** | **260,000,000** | **1,664,000,000** |
| **Matokeo 4.2:** Kuongezeka kwa rasilimali za kifedha endelevu kwa ajili ya kutokomeza ukeketaji | **256,000,000** | **179,000,000** | **150,000,000** | **148,000,000** | **103,000,000** | **836,000,000** |
| **Jumla ya LK4 (SO4)** | **800,000,000** | **519,000,000** | **410,000,000** | **408,000,000** | **363,000,000** | **2,500,000,000** |
| **Lengo la Kimkakati la V: Kuimarisha Uzalishaji wa Ushahidi, Usimamizi wa Maarifa na Kujifunza** | | | | | | |
| **Matokeo ya 5.1:** Kuimarika kwa msingi wa ushahidi kwa ajili ya upangaji wa programu na uundaji wa sera za kutokomeza ukeketaji | **246,000,000** | **20,000,000** | **161,000,000** | **18,000,000** | **16,000,000** | **461,000,000** |
| **Matokeo 5.2:** Kuimarika kwa uwezo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji katika programu za kutokomeza ukeketaji | 366,000,000 | 260,000,000 | 272,000,000 | 241,000,000 | 185,000,000 | 1,324,000,000 |
| **Jumla ya Lengo la Kimkakati V (SO5)** | **612,000,000** | **280,000,000** | **433,000,000** | **259,000,000** | **201,000,000** | **1,785,000,000** |
| | | | | | **JUMLA KUU** | **15,970,000,000** |

UNFPA

Funded by
the European Union

SUOMI
FINLAND

EMBASSY
OF IRELAND

Sema